2016

UUMBAJI HADI KRISTO.

1

SOMO LA 1

Kutanguliza Biblia; Mungu pekee; Mungu aliumba viumbe vya kiroho naLusifa aliasi.

Utangulizi Wa Biblia.

A. Kusudi la somo letu.

- **Yoshua 1:8; Zaburi 1:1-3-** Kusudi la somo letu hili ni kujenga msingi dhabiti wa Biblia, kuanzia uumbaji kuelekea hadi kufa, kuzikwa na kufufuka kwa Kristo ili kuipa nguvu Imani yetu kwake Mungu,Yesu Kristo na kwa neno .

B. Mungu ndiye mtazamo wa somo letu.

- Mungu atakuwa mtazamo wa somo letu; Yeye ni nani, na kile anachokifanya kwa kuwa yeye ndiye mhusika mkuu wa Biblia na alikiandika kitabu hiki (**Biblia**) ili tukaweze kumfahamu.

C. Biblia ni kitabu muhimu Sana duniani.

- **2 Timotheo 3:16** ”**Kila andiko lina pumzi ya Mungu**.” Mungu aliwanenea watu walioitwa manabii ujumbe maalumu aliotaka uandikwe.Wakati mwingine alinena kwa sauti, wakati mwingine kwa maono, na wakati mwingine aliuweka ujumbe moja kwa moja katika mawazo yao. **2 Petero 1:20-21**
- Je, umewahi gundua ya kwamba Biblia ndio kitabu cha kipekee ambacho kiliandikwa na Mungu? Kiliandikwa Kwa takribani miaka **1600** na watu zaidi ya arobaine lakini bado ingali na ule umoja kamili tangia mwanzo hadi mwisho kwa sababu Mungu ndiye mwandishi mkuu.

D. Biblia ni ujumbe wa Mungu kwa ulimwengu.

- Biblia ni ujumbe wa Mungu kwa ulimwengu na alichagua kutumia wayahudi ili wawe kama vifaa vya kupasia ujumbe wake kwa ulimwengu. Wote ambao Mungu aliwatumia kuandika neno lake walikuwa wayahudi isipokuwa tu **(Luka)**.

E. Biblia ni hadithi ya Mungu.

- **Yeremia 9:23-24** - Je, twamjua Mungu vyema kiasi kipi? Yeye ni mkuu kiasi kipi? Je, alikuwa na mwanzo? Je, atakuwa na mwisho? Je, yeye alitoka wapi?

Mungu Pekee.

A.Mungu ni wa milele…Hakuwa na mwanzo na Hatakuwa na mwisho.

- Lengo letu leo ni kuona kuwa Mungu alikuwepo kabla ya vyote na kuweka msingi wa ukuu wake.
- Tukianzia pale mwanzo. **Mwanzo 1:1** “Hapo mwanzo Mungu…” kitu cha kwanza kabisa ambacho Mungu Anataka tujue ni kuwa kila kitu kilikuwa na mwanzo. Mungu pekee ndiye Hakuwa na mwanzo **(“Hapo mwanzo Mungu”)**
- Hapakuwepo wakati wowote ambapo Mungu hakuwepo. Hakuumbwa wala kuzaliwa. Amekuwa hai daima na hatakufa **1 Tim 1:17;6:16**

B. Mungu ni utatu.

- Wazo jingine kumhusu Mungu ni kwamba ni wa milele.**Mwanzo 1:26** tulipojifunza neno la Mungu, ni wazi kuwa ingawa kuna Mungu mmoja tu, kuna utu utatu ambao wote ni Mungu kwa usawa (**utatu) Mat 28:19 2 Wakorintho 13:14.**
- Utatu ni zaidi ya ufahamu wetu; mifano yote ya kibinadamu huvunjika (yai , jua nk) Hata hivyo , ukweli wa kushangaza wa utatu ni baadhi ya vitu vingi vinavyo tuonyesha ukuu wa Mungu.(Hakuna aliye kama Yeye)

C. Mungu ni Roho

- Jambo jingine kuu kumhusu Mungu ni kwamba Yeye ni Roho**. Yoh 4:24** - Yeye hana mwili na mifupa kama sisi wanadamu tulivyo.

D. Mungu hana upunguvu.

- Tabia nyingine ya Mungu ni kuwa hana upunguvu. Anajua kila kitu. (**Warumi 11:33,34**) Yuko kila pahali wakati wote (**Yeramia 23:23, Zab 139:7-12)**
- Ni jambo lisiloweza kubainika kwetu kuweza kuelewa yule ambaye hana mwanzo wala mwisho na yuko katika hali ya utatu katika mmoja. Hatuwezi hata kudhani yule ambaye hana mwili wa kawaida na yupo kila pahali kila wakati na anajua kila kitu.
- Mungu wetu ametukuka zaidi ya kila kitu tunachoweza kufikiri. Neno ambalo hutumika kueleza utukufu wa Mungu wa milele ni mfalme (**Mtawala wa uwezo wote**.)

Mungu aliumba viumbe vyote vya kiroho. .

A. Mungu aliumba viumbe vyote vya kiroho

- Kabla hatujaangalia jinsi Mungu wetu wa ajabu alivyo umba vitu vyote tuvionavyo, hebu tuchukue muda mchache kushiriki nawe kidogo kuhusu ulimwengu wa kiroho tusioweza kuuona.
- Hapo mwanzo Mungu aliumba viumbe vyote vya kiroho.
- Kuna maneno mengi ambayo yametumika katika Biblia kuelezea hivi viumbe vya kiroho; Roho, Malaika, makerubi, maserafi.
- **Mwanzo 1:1**- Viumbe vyote vya kiroho viliumbwa wakati huu kabla ya mwanzo, hakuna aliyekuwa akiishi. Mungu aliwapa uzima kwanza kisha, wakashuhudia uumbaji mwingine. **Ayubu 38:1-7.**
- **Nehemia 9:6**-_Tunasoma kuwa viumbe vyote vya kiroho vinamwabudu Mungu. Mungu ni mkuu kuliko mapepo na malaika wote. Aliishi kabla yao na aliwaumba. Watu wengi kanisani mwetu wana mawazo ya juu sana kuhusu malaika na viumbe vya kiroho; wanaongelea malaika na mapepo kana kwamba hao ndio Mungu. (**Malaika na viumbe vya kiroho sio Mungu; vinamwabudu Mungu.)**
- **Jambo lingine tunaloweza kufikiria ni** – Alipoviumba viumbe vya kiroho, Aliamua kutovipa miili ya kawaida.

- Kwa kuwa mapepo haina miili ya kawaida, wanaweza kwenda popote wanapotaka, mapepo hawapo kila mahali kila wakati Kama Mungu. Waweza tu kuwa mahala pamoja kwa wakati mmoja.
- Ingawa mapepo hawana miili ya kawaida kama sisi, waweza kubadilika waweza kubadili na kuwa na maumbile mengine kama wanyama , wanadamu nk.kwa wakati tofauti**. Waebrania 13:2.**

B. Viumbe vya kiroho viliumbwa kumtumikia Mungu.

- Je, unafikiri ni kwa nini Mungu aliumba viumbe vya kiroho**…**? **Zaburi 103:20-21 _**ili wampende na kumtumikia. Mwanzo viumbe vyote vya kiroho vilikuwa malaika wa Mungu.

C. Mungu aliumba viumbe vya kiroho sawa, wenye nguvu na hekima

- **Ezekieli 28:15**- _Mungu aliumba viumbe vya kiroho na malaika sawa. Hakuna aliyekuwa muovu.
- **Zaburi 103:20**-_Pia aliumba viumbe vyote vya kiroho vyenye hekima kuu na nguvu.

D. Maelezo kuhusu Malaika.

- Neno malaika linapatikana mara 34 katika vitabu 66. Linatumika mara 275.
- Je, kuna malaika wa kiume na wakike? na je, wao waweza kuoana? Je, wao waweza kufa? **Luka 20:34-36**
- Je, wao hula, ikiwa wao hula, hula nini? Siwezi kulijibu swali hili kweli. Lakini hapa kuna kifungu cha kufarahisha**; Zaburi 78:23-25**.
- Je, kunao malaika wa ulinzi?
- Je, kuna viwango tofauti tofauti vya malaika?

A. Malaika mkuu:- Yuda 9
B. Malaika mkuu:- Danieli 10:13
C. Malaika watawala:-Waefeso 3:10
D. Maserafi – Wanaabudu Mungu:-Isaya 6:1-3
E. Makerubi – Walinzi wa utukufu wa Mungu . Mwanzo 3:22-24.
F. Malaika wateule. 1 Tim 5:21-

- Malaika ni :
  A. Werevu :-1 Petero 1:12
  B. Wanahisia:-Luka 2:13
  C. Wana nia:-Yuda 6
  D. Wana nguvu nyingi. 2 Petero 2:11

E. Viumbe vya kiroho/mapepo ni wengi.

- Je , ni wangapi ? **Ufunuo 5:11, Waebrania 12:22**
- Malaika wote waliishi na Mungu mbinguni hapo mwanzo.
- Hatujui hakika mbinguni ni wapi! Lakini ni mahali halisi, pametajwa mara nyingi katika neno la Mungu, na ndiko makazi ya Mungu.
- Hata ingawa yupo kila mahali wakati wote, mbinguni ndipo makao yake**. Zaburi 11:4**

Lusifa aliasi .

A. Nafsi halisi mbele ya Mungu mbinguni.

- Mungu hakuumba malaika wote wenye sura moja. Wengine walikuwa watanashati, wenye hekima na akili nyingi kuliko wengine.
- Malaika mkuu aliitwa Lusifa, inayomaanisha, nyota ya asubuhi, na Mungu Alimpa Lusifa mamlaka na nguvu yote, juu ya malaika wengine wote. **Ezekieli 28:17.**

B. Kuasi kwa Lusifa.

- Lusifa alitaka kuwa Kama Mungu na kuchukua nafasi Yake. Alikuwa wa kwanza kutenda uovu na kuasi Mungu. **Isaya 14:12-15.**

C. Malaika wengine walimfuata Lusifa katika uasi.

- **Mat 25:41, Luka 8:20,Waefeso 6:12, 2 Petero 2:4**
- Malaika wengi wa Mungu walimfuata Lusifa, kiongozi wao.
- Hili lingetendeka aje? Hatuelezwi chochote isipokuwa Biblia inatueleza wazi kuwa Mungu Anaruhusu viumbe zake kufanya uamuzi.
- Tafathali weka maanani kuwa hakuna chochote kati ya hayo kilicho mtia Mungu hofu, Alifahamu kile ambacho shetani na malaika wengine walikuwa wanafikiria. **Waebrania 4:13**.

D. Mungu aliwafukuza shetani na wafuasi wake kutoka mbinguni.

- **Isaya 14:12-15, Ezekieli 28:16, 17, Yuda 6** – Mungu alimtoa Lusifa na wafuasi wake kutoka nafasi zao mbinguni, aliwarusha chini. Wao si watumishi wa Mungu tena.
- Kila mara wapo kinyume cha Mungu. **Ayubu 1:6-7; 2:1&2**. Ingawa ni hivo Shetani anaweza kumfikia Mungu lakini hayupo tena mbinguni.

E. Mungu aliandaa ziwa la moto kwa Lusifa na wafuasi wake.

- Mungu aliandaa mahala pabaya sana pa hukumu ya milele panapoitwa ziwa la moto kwa Lusifa na wafuasi wake.
- Kila mara Mungu Huwaadhibu wale wanaomuasi**. Ufunuo 20:10; mathayo 25:41**.

F. Lusifa na malaika wake wanamchukia Mungu.

- Kwa sababu ya haya yote, Lusifa na wafuasi wake wanamchukia Mungu.
- Lusifa sasa anaitwa Shetani maana yake adui, mshitaki; na wafuasi wake wanaitwa mapepo. Ni wachangamfu na wanatenda kazi ulimwenguni humu.
- Kumbuka **Ayubu 1 na 2** – Shetani anasema kuwa alikuwa akienda huku na kule duniani na akitembea juu na chini ndani mwake.
- Katika jamii zetu, Shetani anapata umakinifu mwingi kutoka kwa wengi. Michezo ya kuigiza na vitabu juu yake vinaandikwa. Miziki, michezo na kuabudu Shetani kunatolewa kwake na wapumbavu**. 2 Wakorintho 11:13-14** . Tutaongelea Zaidi juu ya haya katika masomo mengine baadaye.

SOMO LA 2

Uumbaji – Mwanzo 1:1- Mwanzo 2:4

Uumbaji. .

A. Utangulizi.

- Katika somo hili tutakuwa tukitazama uumbaji.

B. Hapo mwanzo.

- **Mwanzo 1:1 –** Maelezo mengi yanajitokeza kuhusu kilichotikea hapo mwanzo.Kuna maalezo mengi kuhusu jinsi ulimwengu uliumbwa. (Mulipuko mkali, kustawi toka umbo moja hadi lingine, nk.) Pia kuna maelezo mengi kuhusu jinsi maisha yalianza.
- Wengi wa wana akiolojia na wanasayansi wamekashifu kitabu cha Mwanzo wakieleza kuwa katika mawazo yao ni masimulizi tu na yasiyo dhibitishwa.Ingawaje hivi maajuzi walidhibitisha ukweli maelezo yanayo unga mkono maandiko katika kitabu cha mwanzo kuhusu uumbaji. Biblia si masimulizi tu bali ni hadithi ya ukweli.
- Neno mwanzo linamaanisha mwanzo wa kila kitu. Na hakuna chochote wala yeyote **(isipokuwa Mungu**) alikuwepo kabla ya mwanzo.

C. Uumbaji wa dunia.

- **Mwanzo 1:1** – Inasema, "**Hapo mwanzo Mungu aliiumba mbingu na nchi. "** Neno kuumba linamaanisha kutengeneza pasipo chochote. Ni kweli Mungu alitengeneza mbingu na nchi pasipo na chochote. **Waebrania 11:3.**
- **Mwanzo 1:2** – hebu fikiria jinsi hili lilikuwa. Hakuna mwangaza, maji kila mahali, hakuna uzima na roho wa Mungu akaanza kutembea juu ya maji.
  Neno kutembea linatafusiriwa kama kutingiza.
  Tafakari juu ya haya katika mawazo yako: Mungu, Roho mtakatifu akiwa anatembea huku na huku juu ya maji, akitingiza kwa nguvu za ajabu akiumba vitu vyote. Na katika mstari wa 3 , Mungu alisema , **"…kuwe na nuru…"** na kukakuwa na nuru na **(ufahamu kuwa sio jua bali ni nuru)**
- **Zaburi 29** – Inasema kuwa, "…sauti ya Bwana ni yenye nguvu, Mungu wa utukufu anatisha…"
- Kwa miongo michache iliyopita, mwanadamu angekundua mengi zaidi kuhusu ulimwengu kuliko alivyokundua hapo mwanzoni. Hebu nishiriki nasi orodha kadhaa kuhusu ulimwengu huu wa ajabu ,
- Iwapo tungekuwa tukisafiri kwa mwendo wa mwangaza, **(Maili 186 000 kwa sekunde)** tungezunguka dunia mara saba kwa sekunde. Kwa mwendo huo tungeweza kuifikia nyota iliyokaribu sana kwa miaka mine ; na miaka **59 000** kufikia mwisho wa sayari yetu dunia , na miaka **750 000** hadi kwa sayari inayo fuata . Sayari tuliomo ina nyota bilioni 200 kwa ujumla ndani mwake, miliono moja ndani ya hizo nyota zinatoshana na jua, ambalo ni nyota ya kipimo cha kadri, kuna nyota nyingi zaidi angani kama tu tulivyo na mchanga katika bahari zote humu duniani.
- Kwa hivyo Mungu alinena na vyote vilivyoumbwa vikaonekana. Siku ya pili akaumba hewa inayotuzunguka na anga. Siku ya tatu, ardhi, na mimea inayo onekana. Siku ya nne, jua, mwezi

na nyota vikaweza kuonekana. Siku ya tano, Mungu alinena na idadi kubwa zaidi ya wanyama ikaonekana. Aliumba kila aina ya wanyama na uwezo wa kuzaana wa aina yake tu. (mbwa wana kelbu na paka wana vipusi**) Mwanzo 1:3-25**.

- Ni muhimu kufahamu kuwa, baada ya kuorodhesha vyote alivyoumba Mungu, kila siku inasema, **"…Mungu akaona kuwa ni vyema…"**
- Mungu Mwenyewe ni mwenyewe ni mwema, Mkamilifu, Mtakatifu na Mwenye haki. Hawezi kutenda chochote ambacho si jema.
- Kifungu hiki pia kinasisitiza ufahamu wa nguvu za Mungu. Ili sisi wanadamu tukaweze kufanya ama kutengeneza kitu, lazima tufahamu kwanza kujitengeneza.
  Haikuwa hivyo na Mungu, yeye anajua kila kitu, kwa hivyo hakujua tu kutengeneza/kuumba bali alifahamu jinsi ya kuviumba pia.
- Hatuhitaji kujifunza kutengeneza kitu kabla ya kukitengeneza tu bali lakini tunahitaji karibia kila kitu cha kutengenezea. Lakini Mungu alitumia nini kuumba dunia na vyote vilivyomo? **HAKUNA**. Aliumba kila kitu bila chochote kwa kuwa kweli ni Mkuu.

D. Kuumbwa kwa mwanadamu.

- Halafu **Mwanzo 1:26** – tunaona kilele cha uumbaji. Mungu kwa upendo, ukamilifu na kwa usawa ipasavyo akaumba kila kitu kwa matayarisho ya uumbaji wake wa mwisho. (**Msimamizi wa viumbe Vyake**). **Waefeso 2:10**.
- Hebu fikiria jinsi ilivyo jamii inapotarajia mtoto wa kwanza. Wanamtengenezea chumba na kutayarisha kila kitu kabla ya kuwasili ili kumleta nyumbani mahali ambapo mahitaji yake yote yaweza kushughulikiwa mahali maalumu pakupendeza na palipotayarishwa tu kwa ajili ya mtoto yule. (vivyo hivyo Mungu aliandaa kila kitu kwa ajili ya Adamu.)
- **Mwanzo 1:26** – Inamaana gani kuwa Mungu alimuumba Adamu kwa umbo Lake? Hatuongelei juu ya mwili. Mbona? Mungu ni Roho.
- Mwanadamu aliumbwa katika umbo la Mungu katika nafsi na roho. Mungu aliamua kuwa tukaweze kuwa na nia hisia na mawazo kama umbo lake; ili tukaweze kumjua Mungu , tuwe na mawazo kama yake na tufanye maamuzi kama yeye . Ili Mungu akaweze kuwasiliana nasi na pia hata kutufurahia.

E. Bustani la Edeni.

- **Mwanzo 2:8** – Mungu aliandaa bustani la kupendeza kwa Adamu kwa kuwa alimpenda. Alipomaliza kuliandaa alimweka Adamu pale. Hakumuuliza Adamu kama angependa kuwa pale bali alimchukuwa tu na kumweka hapo.
- Kwa kuwa Mungu ndiye aliyemuumba alikuwa na uhuru wa kumweka popote alipotaka na kumwamuru afanye kile angetaka. Adamu alikuwa wa Mungu, je, na sisi? **Kumb. la Torati 12:7,8.**
- **Mwanzo 2:9 – 16 na 17** – Mungu aliumba miti miwili muhimu zaidi katika bustani hili la Edeni na akampa Adamu maagizo. Hakumwachia Adamu mwenyewe kuamua ni mambo yapi yaliyo kuwa halali na yale maovu. Alinena naye kifasaha sana na akamkanya kile ambacho hakikuwa halali na la sivyo angekufa.
- Vivyo hivyo Mungu anatuonya kupitia kwa neno lake. Hajatuachia sisi wenyewe kuamua kilicho baya na jema.
- Ingawa Mungu alijua kile kilicho kuwa jema kwa Adamu, aliamua kumpa uamuzi iwapo atatii ama hatatii ni juu yake mwenyewe. Angekula kutoka mti wa uzima na aishi milele au kutoka kwa mti wa kufahamu yaliyomema na mabaya na afe .
- Je, Mungu alimaanisha nini alipomwambia Adamu kuwa angekufa. (Kufa = kutengana)

1. Adamu angetenganishwa na Mungu. (**Kifo cha kiroho**). Ni nini kilichotendeka kwa Lusifa na malaika walipotenda dhambi…?

2. Hakungekuwa na kifo cha kiroho tu kwa Adamu, bali hata kifo cha mwili hata kama kifo cha mwili hakikuwa cha ghafla. , lakini ni kama tu jani la mti huanguka kutoka mtini likiwa kijani kibichi na kisha kuyeyuka pole pole hadi kufa kwa kuwa limetenganishwa na chanzo chake cha uzima.

3. Kifo cha tatu ambacho Adamu angepokea kwa kutotii ingekuwa kutenganishwa na Mungu milele katika ziwa la moto. Mahali pale pale pa mateso ya kikatili alipotengewa shetani na wafuasi wake**. Ufunuo 20:10, Mathayo 25:41**.

- Mungu alimhakikishia Adamu vyema zaidi Kama tu anavyotuhakikishia, kuwa mshahara wa dhambi ni mauti. **Warumi 6:23; Mithali 16:25.**

F. Mungu anamuumba Hawa.

- **Mwanzo 2:18** Mungu aliamua kuwa Adamu hataishi pekee yake. Alikuwa amemuumba na alijua kilicho bora kwake. Kama awali, Mungu hakumuuliza bali alimfanyia uamuzi kwa sababu alijua Adamu hangekuwa na furaha akiwa pekee yake.
- Sasa Mungu akamfanya mke wa kwanza kama kibawa kwa Adamu kwa sababu anampenda. **Mwanzo 2:23 na 24.**

G. Hitimisho.

- Ndoa haikuvumbuliwa na mwanadamu, bali iliumbwa na Mungu. (**enenda mkaishi pamoja)** Ndoa ilikuwa mpango halisi kwa Adamu na Hawa. Mungu alikuwa amewapa kila walichohitaji. Alikuwa rafiki yao aliwapenda na walifurahi sana. Alikuwa amewazingira na urembo na utele. Wangeweza kuwasiliana na Mungu moja kwa moja. Alikuwa amewafanya watawala juu ya vyote alivyoumba. Kazi yao haikuwa ngumu, pia hakukuwa na magonjwa. Nafasi ya ajabu aje unayoweza kuwemo…!

SOMO LA 3

Kuanguka kwa mwanadamu. Mwanzo 3:1- , 3:8

Kuanguka kwa mwanadamu. .

A. Utangulizi.

- Maisha katika bustani yalikuwa ya kupendeza kwa Adamu na Hawa kwa sababu kila kitu kilikuwa sawa. Lakini, je, adui mkuu wa Mungu, Shetani, alikuwaje?

B. Shetani, mdanganyifu na mharibifu.

- Shetani alijua ilani ya Mungu kwa Adamu kuhusu mti wa kujua mema na mabaya.
- Kwa kuwa Shetani alikuwa adui wa Mungu, alitaka kuharibu mwanamumme na mwanamke ambao Mungu alikuwa amewaumba na kuwapenda.

C. Shetani alijifanya nyoka kumfanya asitambulikane na Hawa Ili amdanganye.

- **Mwanzo 3:1** – huyu hakuwa tu nyoka akiongea na Hawa. Shetani mwenyewe alikuwa ameingia katika kiumbe hiki na alikuwa anajifanya nyoka sasa ili akaweze kumdanganya Hawa.
- Nyoka alikuwa mwerevu zaidi kuliko kiumbe kile ambacho Mungu aliumba. Shetani ni mwerefu na mdanganyifu**. 2 wakorintho 11:3, Ufunuo 12:9.**
- Je, wafikiria kuwa Hawa alikuwa na ufahamu wowote kuwa ni shetani aliyekuwa akiongea naye kupitia kwa nyoka? La! Hakuwa amekula kutoka kwa mti na hivo hakujua lolote lililo mbovu. Kifungu cha kufurahisha**: Warumi 16:19-**
- Shetani si mdanganyifu tu bali ni mwongo pia. **Yohana 8:44**
- Zaidi tunapoendelea kujifunza kutoka kwa neno la Mungu, ndivyo tunapoendelea kufahamu zaidi jinsi Shetani alivyomdanganyifu na mwovu.
- Anajaribu kufanya lililonzuri kuonekana baya. (**Kuwaadhibu watoto**), na anajaribu kufanya kiovu kuonekana kizuri. **(Kuavya mimba) 2 Wakorintho 11:13-15.**

D. Shetani bado anawadanganya watu.

- **2 Wakorintho 2:11**:- yatueleza kuwa tusipuuze mbinu za shetani. Moja kati ya mbinu za Shetani ni uongo ndani ya mawazo yetu. Yeye ni mwerevu zaidi na haturuhusu kujua ya kwamba mawazo yetu yanatoka kwake**. Yohana 13:1,2**
- Shetani anaweza kuweka wazo katika fikira zetu lakini hawezi kusoma fikira zetu.
- Nia ya Shetani na mbinu zake za ujanja ni sawa na jinsi zilivyokuwa katika bustani la Edeni angali anaendelea kuwadanganya watu na kuwaharibu.
- Kumbuka **Yohana 8:44** – Shetani ni mwongo/muuaji.
- Shetani anaweza kuongea nasi hata kama tunaomba au kusoma Biblia.
- Aweza kuweka wazo/swali mawazoni mwetu kuhusu ukweli wa neno la Mungu jinsi vile alimfanya Hawa . Hahitaji mtu yeyote kumjua Mungu…anachukia Mungu na neno lake hata kama anajua ni ukweli.

E. Kudanganywa kwa Hawa.

- **Mwanzo 3:1** – Mbona Shetani alimuuliza Hawa swali hili? Kwani hakujua tayari jibu sahihi? (**Alikuwa anajaribu Hawa kumhadaa, ili kujua kile Hawa alikuwa anajua**.) Pia alikuwa anatumia neno hili kutia shaka neno la Mungu … ambayo ni mojawapo ya njia zake anayoipenda.

- **Mwanzo 3:2-3** Awa alichanganyikiwa na Shetani alijua hilo. **Mwanzo 2:17** – Mungu hakuwahi sema kuwa "msiuguse" Jambo lingine la kufikiria ni kuwa Mungu hakuwahi kuwa ameongea na Hawa moja kwa moja kuhusu mti wa kujua mema na mabaya. Amri yake alimpa Adamu lakini ilimhusu Hawa pia, kwa hivyo Adamu alimwambia Hawa kile ambacho Mungu alikuwa amemwelezea.
- Ni sawa nasi leo hii pia, Mungu alinena neno lake kwa watu miaka elfu iliyopita lakini bado inatuhusu leo hii.
- **Mwanzo 3:4-5** – Shetani sasa haleti shaka tena bali anamwita Mungu muongo; Lakini ni nani mwongo hasaa**? Yohana 8:44**
- Tunaona kuwa Shetani alimwasi Mungu alipotaka kuchukua nafasi yake , sasa anamwambia Hawa pia aweze kumuasi kama yeye alivyofanya kwa kula tunda alilokatazwa ili awe kama Mungu kwa kujua mema na maovu.
- Fikiria juu ya hili, Mungu hakuwaumba Adamu na Hawa ili waishi kwa fikira zao.
- Hawakustahili kujua lolote kuhusu uovu. **Warumi 16:19**. Wangeamini tu kile Mungu alisema. (**Je, na sisi leo hii?**) **Mithali 3:5-6** – tunastahili kuelekezwa na neno la Mungu kama tu Adamu na Hawa.
- **Mwanzo 3:16** – Shetani alimdanganya Hawa na akamwamini kuliko alivyoamini Mungu na hivyo wakala tunda alilokatazwa na Mungu. **(Hawa alidanganywa**)

F. Uasi wa Adamu .

- Kwa upande mwingine , Adamu huku akijua kile alichosema Mungu , **(bila kudanganywa**) kwa hiari aliamua kumuasi Mungu na kula tunda kutoka kwa mti wa kujua mema na mabaya aliokatazwa na Mungu…**1 Tim 2:14**

G. Matokeo ya uasi wa Adamu.

- **Mwanzo 3: 7, 8** – Mungu alisema ni nini kingetendeka iwapo wangekula lile tunda walilokatazwa? Kifo!
- Lakini hawakuanguka chini na kufa papo hapo kifo cha kawaida. Je, wafikiri kuwa neno la Mungu si kweli na Shetani alikuwa haki?
- La, jinsi tulivyo jadili hapo mwanzoni kifo kinamanisha kutenganishwa na hivyo tunaona katika msitari wa 8 kuwa walitenganishwa na Mungu papo hapo (kifo cha kiroho). Mungu daima hutenda kulingana na Neno lake. Hasahau kuadhibu kutotii**. Isaya 59:2**
- Kwa kuwa Mungu ni mtakatifu na mwenye haki , anachukia kile kisicho cha haki na kuadhibu kutotii kwa amri na mauti. **Warumi 6:23**
- Kwa kuwa Adamu na Hawa hawakutii na kumwamini Mungu, walikatwa/kutenganishwa na Mungu kutoka kwa urafiki waliokuwa nao pale awali. Uhusiano wao na Mungu ulikufa.
- Waliweza kushirikiana na adui wa Mungu, Shetani, nao pia sasa wakawa adui wa Mungu. Hebu tafakakari jinsi ilivyokuwa kwake Mungu.
- Hebu fikiria jinsi ingekuwa vibaya rafiki yetu tuliyempenda kushirikiana na adui yetu alituchukia na aliyetaka kutuua. Vivyo hivyo ndivyo ilivyo kuwa na Mungu. Tuko katika umbo Lake.

H. Ishara za kutenganishwa na Mungu.

- Hebu tukatazame kilichotendeka walipotenganishwa na Mungu.
- Nia zao kuhusu miili zao ilibadili, **(msitari wa 7).** Sasa walifahamu kuwa walikuwa uchi.
- Kabla ya kutotii walikuwa uchi na hawakuwa na haya. **Mwanzo 2:25** ,lakini sasa wakiwa wametenganishwa na Mungu , mawazo yao hayakutawaliwa na Mungu tena ,**Warumi 8:6**
- Mawazo yao yakawa maovu na nia zao kuhusu miili yao sasa ikabadili – waliaibika kwa kuwa uchi.
- Hawakumwamini Mungu kuwapa mahitaji yao tena. **Mwanzo 3:7b**

- Sasa walijaribu kujitimizia mahitaji yao wenyewe.
- Hawakuwa wakimjali Mungu tena bali waliingiwa ubinafsi.
- Walijaribu kuishi maisha ya kujitegemea bila ya kumjali Mungu.
- Jambo lingine la kufikiria ni; kabla hawajala kutoka kwa mti huo, Biblia inasema kuwa, walikuwa uchi lakini hawakuwa na haya. Lakini baada ya kutenda dhambi, wakaanza kuaibika Kwa kuwa uchi. Kwa hivyo walijaribu kusuluhisha shida yao iliyosababishwa na dhambi kwa kujivisha matawi.
- Lakini Mungu hakukubali suluhisho lao la dhambi waliyotenda,. Watu wengi leo hii wanajaribu kusuluhisha shida zao maishani mwao na kufikiri kuwa wanaweza kufanya wenyewe wakubalike na Mungu…kwa kutenda mema ama kuwa washiriki wa kanisa. ama kwa kuwa wazazi wazuri ama kwa kuwa wananchi wanaotii sheria za nchi kikamilifu.
- Hapa kuna ishara zingine za kutengana kwao na Mungu.
  1. Kabla hawajala tunda lililokatazwa na Mungu, walimpenda Mungu na walikuwa wanamtarajia kila mara awatembelee; Lakini sasa mawazo yao yalikuwa yamebadilika na walijificha. **Mwanzo 3:8-9**
  2. Kabla , walikuwa wana nia moja na Mungu , lakini sasa walikuwa na nia moja na na Shetani ...Hawangemjua na kumuelewa Mungu tena , bali sasa walimwogopa . Sasa walikuwa chini ya utawala wa Shetani.

I. Hitimisho.

- Watoto wetu kwa hiari wanapokataa kututii kwa hiari, je, watataka kuwa karibu nasi…? Je, wanaweza kututazama usoni na wakafurahia kututazama?
- Dhambi husababisha uoga na kuwafanya watu wamgeuke Mungu. **Zaburi 40:12**
- Wakati Mungu aliwaumba Adamu na Hawa, hawakuogopa chochote.
- Hawakuwa na chochote cha kuogopa kwa kuwa Mungu alikuwa rafiki yao.
- Dunia nzima ilikuwa nzuri na ya kupendeza.
- Magonjwa na vifo havikuwepo.
- Lakini sasa tangu Adamu na Hawa walipomuasi Mungu, kumekuwa na uoga wa kila aina mioyoni mwa waume kwa wake. **Mithali 28:1** Muovu hukimbia pasipo kufukuzwa, lakini mwadilifu ni kama simba mwenye uhakika.

SOMO LA 4

Matokeo ya dhambi za mwanadamu – Mwanzo 3:9/3:23

Matokeo ya dhambi za mwanadamu.

A. Mungu alimwita Adamu.

- **Mwanzo 3:9;** - Rudia msitari wa nane mbona Mungu alimwita Adamu
- Je, Hakujua mahala alipokuwa amejifija?
- Nilifikiri Mungu yuko kila mahali na alijua kila kitu.
- Je, yeye hangemwona?
- Mbona Alimwita? Naamini kuwa ingawa Mungu alitaka kuwaadhibu Adamu na Hawa kwa ajili ya dhambi yao, bado alikuwa anawapenda na hivyo aliwapa fursa ya mwisho wakubaliane naye kuliko Shetani, **(2 Petero 3:9)** – Mungu ni mvumilivu na hataki yeyote apotee.
- Wajua Mungu habadili; Angali vivyo hivyo alivyokuwa bustani.
- Angali anawaita waume kwa wake…Mko wapi? Ili kuwapa nafasi ya kutubu na wakubaliane naye.
- Labda si sauti inayosikika kama ilivyokuwa Kwa Adamu, lakini angali anaita. Njia moja kati ya zile anazoitia ni kupitia kwa maumbile **(Zab 19:1-4, 36:9, warumi1:18,).**
- Njia nyingine anazoitia ni kupitia kwa neno lake na watu wengine (wahudumu nk).
- Adamu, uko wapi?

B. Mwanadamu lazima amjibu Mungu.

- Kwa hivyo Mungu aliita Adamu ili kumpa nafasi ya kubadili mawazo yake. **Mwanzo 3:10, 11** – Iliwabidi Adamu na Hawa wamjibu Mungu kwa kile walikuwa wamefanya (Alikuwa amewaumba na walikuwa wake). Nasi pia tuliumbwa na Mungu na ni wa Mungu. Na siku moja , kila mmoja ambaye jina lake halitakuwa limeandikwa katika kitabu cha uzima cha mwanakondoo watalazimika kumjibu kwa kila kitu walichosema na kutenda . **Ufunuo 20:11-12 ,21-27 ,Mat 7:22 – 23**
- **Hebu tufuate mtiririko hapa , Mwanzo 3:8-13** – Ghafla , kukawa na uoga , kujificha , kuwa na hatia ,kutotulia ,na hivyo kulaumiana .
- Katika msitari wa **12**, Adamu anamlaumu nani? (Hawa , lakini Mungu pia) – Mawazo yoyote? Wengine wamesema kuwa Adamu alikula kwa sababu alimpenda Hawa sana.
- Iwapo alikula tunda lililokatazwa kwa sababu alimpenda sana, kitu kimetendeka kwa huo upendo mkamilifu. Ni nini hicho? Dhambi, upendo halisi wa Adamu kwa Hawa sasa umechafuliwa.

C. Hukumu ya Mungu.

- Sasa Mungu anaanza kupeana hukumu; kuanzia kwa nyoka, **Mwanzo 3:14**, Mungu alilaani nyoka kwa sababu alikuwa ametumiwa na Shetani.
- Hatujaambiwa jinsi nyoka alivyokuwa kabla Shetani hajamtumia, mbali na **Mwanzo 3:1 –** Inasema alikuwa mjanja sana. Lakini kitu kimoja tunachokijua ni kuwa hakutambaa kwa tumbo lake Mungu alipomuumba.

- **Mwanzo 3:15** – Katika kifungu hiki, Mungu anaahidi kuwa atamtuma mkombozi, adui wa Shetani, ambaye atamshinda shetani na amkomboe mwanadamu. Kutoka kwa nguvu za shetani.
- Mungu alipanga kuwa mkombozi aliyeahidiwa atakuwa mwana wa mwanamke bikira. Je, tunajuaje haya? Mbengu yake; Mwanadamu kawaida huwa na mbegu kila mara.
- Pia fahamu, yeyote ambaye kisigino chake kimeumwa huishi, lakini kichwa kikiumizwa (**nakala ya NIV inasema kupondwa**) sehemu nyingine ya mwili haiwezi kuishi.
- Shetani angepigana na mkombozi na kumjeruhi, lakini, yule aliyeahidiwa siku moja angemumaliza Shetani.
- Tumeona kuwa Mungu aliwaadhibu wale waliomuasi , **(Adamu na Hawa papo hapo walipokea kifo cha kiroho – kutengana na Mungu)**

D. Rehema za Mungu.

- Lakini sasa tunaona kuwa Mungu kwa upendo wake mkuu kwa mwanadamu ni wa rehema na anaahidi kumtengenezea njia kwa kumtuma mkombozi kwamba aweze kuokolewa kutoka kwa hukumu aliyoistahili **Yakobo 2:13** – kumbuka kuwa " rehema inashinda hukumu ."
- Mungu angewaacha Adamu na Hawa wafe tu, na waende katika hukumu ya milele (kuzimu) ambayo ndiyo hukumu waliyoistahili, lakini badala yake aliahidi mkombozi ambaye angeweakomboa pamoja na wanadamu wote kutoka kwa utawala wa shetani na awarejeshe kwake. Mungu ni wa Rehema. Bwana ni wa neema na mwingi wa rehema si mwepesi wa hasira , na mwenye fadhili kuu **. Zab 145:8-9, Maombolezo 3:22, 23. Zab 136.**

E. Hukumu ya Mungu Kwa mwanadamu: laana ya Mungu kwa mwanamke.

- Mungu kwa rehema zake , atamtuma mkombozi atengeneza njia kwa mwanadamu japo kwa mwanamke , **(Mwanzo 3:16) :** ndio Mungu ni wa rehema ; ndio Mungu ni wa kusamehe ; ndio atamtuma , kifungu hiki kinaeleza wazi kuwa kuna matokeo halisi ya dhambi .
- Hawa na wanawake wote wa baadaye watahisi uchungu wanapojifungua.
- Tamaa yake ya asili itakuwa kumtawala mumewe, lakini mume atakuwa na mamlaka juu yake **1 Wakorintho 11:3;** kujitiisha kwa hiari kwake kuliharibika.

F. Hukumu ya Mungu kwa mwanadamu.

- Sasa matokeo ya dhambi ya Adamu.
- **Mwanzo 3:17-18** – kwa sababu Adamu alimsikiliza mkewe, Mungu alisema kuwa kutakuwa na baadhi ya matokeo ya dhambi ya asili.
- Je, waona nini katika vifungu hivi?
  1. Ardhi kulaaniwa – Siku zote za maisha yake atakula kwa jasho lake.
  2. Miiba na kwekwe kufanya kazi iwe ngumu.
  3. Jasho
  4. Kifo cha kimwili.
- Adamu hangeishi tena kwenye mazingira makamilifu.
- Hata Leo tunaishi kwa ulimwengu unao endelea kuumia kwa sababu ya laana. **Warumi 8:19-22.**
- Pia nasi tunaumia kila mara tunapambana na magonjwa , uchungu , udhaifu ,uchungu wakati wa kujifungua , kazi ngumu ,hali ngumu za kazi ,wadudu , kwekwe , miiba na dhiki .
- Na kama hayo hayatoshi, tokeo la mwisho la dhambi ya Adamu ni kwamba miili yetu, lazima ife na kurejea tena mavumbini ambako ilitoka.

G. Adamu na Hawa ndio wazazi wa watu wote.

- Haya ni matokeo ya kuasi Mungu.

- **Mwanzo 3:20 –** Hata ingawa watu huongea lugha tofauti na wana rangi tofauti ya ngozi, sisi sote tulitoka kwa wazazi wale wale. – Adamu na Hawa .Hapa tunaona kuwa Hawa ndiye mama wa wote. **Matendo ya mutume 17:26.** Mungu amefanya kutoka kwa mtu mmoja (Adamu) mataifa ya watu wote waishio humu duniani.
- Kwa kuwa sisi sote ni uzao wa Adamu, sote tunakufa kimwili na kiroho kwa sababu ya Adamu. **War 5:12.**
- Dhambi ya Adamu ilianzisha msururu wa machonzi utakao endelea hadi milele kwa wengine. Wengine ni akina nani? Wale hawajaokoka.

H.Jaribio la mwanadamu kufunika dhambi zake lakataliwa na Mungu.

- **Mwanzo 3:21** – Kwa kuwa Adamu na Hawa hawakumtii Mungu, fikira zao zilichafuliwa, kama vile upendo wa Adamu kwa Hawa na waliaibika Mungu kuwaona wakiwa uchi.
- Kwa hivyo walijitengenezea mavazi kutoka kwa majani ya mti (**Mwanzo 3:7)**. Mungu alitaka wajue hakuna chochote, wangefanya kwa nguvu zao. Lakini jitihada zao hazikukubalika na Mungu. Njia ya mwanadamu haikubaliki na Mungu. Njia ya Mungu pekee ndiyo inakubalika. **Isaya 55:8-9**
- Je, wajua kuwa watu siku hizi bado wanafanya vitu vingi kujaribu kufanya wakubalike na Mungu? Tunajaribu kuzifunika dhambi zetu kama Adamu na Hawa.
- Lakini haikubali. Tunaweza tu kumwendea Mungu kulingana na masharti yake, hatakubali chochote tutakacho kifanya, haijalishi kuwa zitakuwa za kufikiria kiasi kipi, wala kidini kiasi gani ama gharama ipi, nguvu zetu zitakavyoonekana.

I. Mungu aliwafukuza Adamu na Hawa kutoka Bustani la Edeni.

- Kumbuka **Warumi 6:23 –** Mshahara wa dhambi ni mauti. Mauti ndiyo adhabu ya dhambi, na hakuna njia ingine ya kulipa.
- Mungu alimuua mnyama na kuwavisha ngozi kuonyesha kuwa kuasi kwao kulileta mauti duniani.
- Mungu ni wa upendo , wa rehema na neema , kwa hivyo Alimuua mnyama ili kumvalisha Adamu na Hawa hata ingawa hakustahili hilo , bali ili wakubalike kwake…Ingawa **!!!**
- **Mwanzo 3:22-23** – Mungu hakutaka Adamu na Hawa wajue maovu; walistahili tu kujua mema. **Warumi 16:19**
- Mungu alijua yaliyokuwa maovu na mema ,Adamu na Hawa hawakustahili kujua , walikuwa na Mungu ili akawaelekeze , hapakuwa na haja ya hao wenyewe kujua.
- Ingawa, waliasi na sasa wakatupwa nje ya Bustani la Edeni. Kwa nini? Ni kwa nini iliwabidi kutoka katika bustani la Edeni?
- Ili wasile kutoka kwa mti wa uzima wakapate uzima wa milele tena. Hili hakika lilikuwa tendo la rehema za Mungu.
- Mungu hakutaka mwanadamu aishi milele katika hali hii ya dhambi. Hebu fikiria jinsi dunia ingekuwa kama wanadamu wote waliotenda dhambi wangekuwa hadi leo hii.

J. Hitimisho.

- Hebu fikiria hili, Mwanzo Mungu aliwaweka katika Bustani na akawaruhusu wale hata kutoka kwa mti wa uzima. Kwa kuwa sasa walikuwa wenye dhambi. Aliwaweka nje ili kuwazuia kutokana na mti wa uzima. **Warumi 6:23**
- **Mwanzo 3:24 –** Alimfukuza mwanadamu kivipi? **(Inaonekana kana kwamba Adamu hakutaka kutoka.)**
- Malaika na mishale ya moto waliwekwa kuhakikisha kuwa Adamu na Hawa hawarejei tena.
- Kama wangejaribu kurudi makerubi wangewauwa kwa mishale ya moto.

- Hakuna chochote ambacho wangefanya, wakati Mungu aliwaweka nje ya bustani la Edeni, hawakuwa na njia nyingine ya kurejea tena. Sasa wangehukumika na matokeo ya dhambi zao, waishi hadi uzeeni na wafe.

SOMO LA 5

Kaini na Habili – mwanzo 4:1 - , 4:24 –

Kaini na Habili. .

A. Utangulizi.

- Je dhambi ina madhara gani?
- Itakuaje mtu akikataa kumtii Mungu na kutomwamini.
- Je, twaweza kusema iyo ni sawa kwa yeyote inavyompendeza.
- Je, dhambi ya mtu yaweza kuwaadhiri wengine?
- Je, mtu yeyote aweza kutenda chochote ili kulipia dhambi zake?
- Je, ni kweli kuwa kila mwanadamu ajiumbie njia yake ya kumfikia Mungu?
- Je, Mungu aweza kukubali kujitolea kwetu kwa bidi?

B. Madhara ya dhambi ya Adamu

- **Mwanzo 4:1-2 –** Kaini na Habili wote walizaliwa nje ya bustani la Edeni mbali na mti wa uzima.Kwa nini? Kwa sababu baba yao alitenda dhambi na akaondolewa kwenye bustani.
- Kwa hivyo wote wawili walizaliwa wenye dhambi wakiwa chini ya uongozi wa Shetani, kwa sababu Adamu baba yao alikuwa mwenye dhambi.
- Tumeliongelea swala hili mara kadhaa.
- Nasi sote tumezaliwa katika asili ya dhambi (**nafsi ya ndani ipendayo uovu**). Uovu wa ndani tunaozaliwa nao.
- Sisi kizazi kimoja kirefu cha wenye dhambi kuanzia kwa Adamu. **War 5:19**
- Kumbuka hili, tu wenye dhambi kwa sababu tulizaliwa wenye dhambi wala sio kwa matendo ya dhambi tutendayo.
- Tumegundua kuwa Mungu ndiye mpeanaji wa uzima, ilhali hatukuzaliwa tukiwa rafiki ama na umoja na Mungu. Bali tulizaliwa tukiwa maadui na Mungu. **War 5:6-10.**
- Zaidi ya hayo, Shetani amechukuwa nafasi ya Mungu na kufanyika baba wa kiroho wa mwanadamu wa asili. **Yoh 8:40-44 –**
- Watu wengi wanafikira kuwa watu wote ni wana wa Mungu, hili ni wazo la kufariji na kupendeza sana na kuonekana la kiungu zaidi, lakini ni uongo wa shetani.
- Mafundisho kama haya ni kinyume na mafundisho kamili ya Biblia.
- Ni kweli Mungu alituumba lakini hatukuzaliwa wana wa Mungu, bali wana wa Shetani tukiwa tumetengwa mbali kabisa na Mungu.
- **Tanbihi:** Adamu na Hawa walikuwa wanadamu halisi na dhambi yao ina madhara makubwa sana kwa wanadamu wote.
- Dhambi yao iliwaadhiri wanao kwa sababu ya dhambi ya Adamu na Hawa haingewezekana tena kwa Kaini na Habili kurejea kwenye Bustani ili wawe na ushirika pamoja na Mungu.
- Wote sasa walikuwa wenye dhambi; Adamu, Habili na Kaini.
- Hakuna lolote ambalo wangefanya wala kumlipa Mungu kwa sababu ya dhambi zao.

C. Mungu anamtengenezea mwanadamu njia.

- Lakini kupitia kwa rehema, neema na upendo wa Mungu kwao, aliamua kuweka njia kwa mwanadamu kumfikia.
- Hii haikuwa njia ya mwanadamu bali ya Mungu.

D. Mungu aliwaeleza kile walipaswa kukitenda wakati wanaenda kumwabudu.

- Biblia inatupa sababu nzuri ya kuamini kuwa Adamu na Hawa walielezwa kilichowapasa kukitenda ikiwa wangetaka kuja kwake, nao pia wakawaelezea wanao Kaini na Habili.
- Hili ndilo ambalo lazima Adamu na Hawa waliwaelezea wanao.
- Mkienda kwa Mungu, beba kondoo kama dhabihu.
- Kondoo auwawe huku ukihakikisha kuwa damu inatoka nje.
- Sasa tunajua kuwa damu ya kondoo haiwezi kulipia fidia kwa dhambi ya mwanadamu, **Waeb 10:4 –** Lakini ni kwa nini Mungu aliwambia wauwe kondoo?
- Kwa sababu Mungu alitaka waendelee kukumbuka kuwa mshahara wa dhambi ni mauti.
- Alitaka waendelee kujua kuwa wakifa wataingia katika hukumu ya milele ikiwa Mungu mwenyewe hangewaokoa.
- Ikiwa wangekubaliana na Mungu, kuwa wao ni wenye dhambi na Mungu pekee wa kuwaokoa, basi iliwapasa walete kondoo na auwawe jinsi Mungu alisema. **War 17:11, Waeb 9:22 –**

E. Kaini na Habili walienda wote kumtolea Mungu dhabihu.

- **Mwanzo 4:3-5 –** Kaini na Habili wote waliamini kuwa Mungu alikuwepo (tunajuaje hili?). wote walienda kumtolea Mungu dhabihu, lakini je, kumwamini Mungu na kumtolea kile tunachofikiria ni kizuri kwetu chaweza kutufanya tukubalike na Mungu? **Yakobo 2:19 –**

F. Sadaka ya Habili na Mungu.

- Tunaona katika **mwanzo 4:4 –** kuwa **ilikubaliwa** Habili alimleta kondoo mmoja kama dhabihu mbele za Mungu.
- Alikuwa kondoo mzaliwa wa kwanza jinsi vile Mungu alitaka.
- Tena nataka kusema kuwa, ni muhimu kufahamu kuwa damu ya mnyama haiwezi kutusamehe dhambi. Mungu hakukubali kondoo wa Habili kama fidia ya dhambi zake. Lakini, Mungu alimsamehe Habili ni kwa kuwa aliamini katika njia ya Mungu. Alimtumainia Mungu aliyeahidi wazazi wake mkombozi atakaye kuja wakati mmoja **Waeb 10:6, 11:6a,10:38 -**

G. Sadaka ya Kaini ilikataliwa na Mungu.

- **Mwanzo 4:5 –** Kaini alileta mazao ya shambani kama dhabihu. Hata hivyo Mungu hakumkubali Kaini wala dhabihu yake.Vyote vinavyoanza na mwanadamu, haikubaliki na Mungu. Kaini hakumwamini Mungu! Hakutumainia njia aliyopewa na Mungu.
- Kumbuka kuwa Mungu alikataa majani ya miti ambayo Adamu na Hawa walijishonea kama nguo. Kwa kuwa alitaka wajue kuwa hawangejitengenezea njia yao ya kukubalika na Mungu.
- Sasa Mungu alikataa dhabihu ya Kaini kwa sababu hii. Nataka kusisitiza kuwa imani ndiyo sababu ya dhabihu ya Kaini kukubalika na kutoamini ndiyo sababu ya matendo ya Kaini; hili sio swala la kutii bali hili ni zaidi **Yakobo 2:17-18 –**
- **Waeb 11:4 –** tambua kuwa imani ndiyo iliyoleta utofauti kati ya Kaini na Habili.
- Mungu hajabadili; Yeye ni yule yule hata leo hii; ingawa hatuamuru sisi kutoa sadaka ya kondoo, bado ameweka njia moja ya pekee kwetu sisi kumfikia. Nasi pia ni lazima tumwendee kwa njia tunayopaswa la sivyo, atukatae kama tu alivyokataa Kaini na sadaka yake. **Yoh 14:5-6**
- Kumbuka tulisema kuwa ikiwa tawi la mti litakatwa, litanyauka polepole na kukauka kwa kutengwa na mti uliolipa uhai. Itakuwa aje tukijaribu kuunganisha tawi lililokufa kwa mti? Kama tutafunga tawi lililokufa katika mti je hili tawi laweza kunawiri tena? Je, majani yatabadili kuwa kijani kibichi na yaanze kukua? La, haiwezekani kuunganisha tawi lililokauka kwa mti ili likaweza kustawi tena.

- Lakini ni kama watu hutumia muda wao mwingi duniani wakijaribu kujiunganisha wenyewe na Mungu. Baadhi ya njia zinazotumika na wanadamu ambazo huonekana kuwa za kidini: kwenda kanisani, kutoa pesa kanisani,kutenda mambo mazuri, kuwa watu wazuri**, Isaya 64:6** – kwa maana sisi sote tumekuwa kama mtu aliye mchafu, na matendo yetu yote imekuwa kama nguo iliyotiwa najisi.
- Kwa kuwa wanadamu wote huzaliwa wenye dhambi, wote tumetengwa kutoka kwa chanzo cha uzima ambacho ni Mungu, na hakuna chochote ambacho tunaweza kutenda cha kuturejesha kwa Mungu. Dhambi imetutenga kutoka kwa Mungu kama tu tawi lililokatwa kutoka kwa mti **Isaya 59:2 –** maovu yenu yamewafarikisha nyinyi na Mungu wenu.
- Hivyo ndivyo ilivyokuwa na Adamu, Hawa, Kaini na Habili. Kwa kuwa Adamu na Hawa hawakumtii Mungu, wote walitenganishwa na Mungu.
  Kumbuka **War 5:12 –** kwa mtu mmoja dhambi iliingia duniani na kwa dhambi hiyo mauti ikawafikia watu wote.

H. Mungu awaza na Kaini mwenye hasira.

- **Soma Mwanzo 4:6-7 –** hata ingawa Kaini alikataa kumtii Mungu na kwa uhiari akaenenda katika njia zake, Mungu aliwaza naye.kwa sababu ya rehema na upendo wa Mungu, alinena na Kaini na kujaribu kumrejesha kwake kwa njia inayostahili**. Mithali 1**[22-23]
- Mungu alimtaka Kaini kutambua kuwa pia yeye angekubalika kama nduguye, Habili kwa kuliamini neno la Mungu, kutoa sadaka ya damu na kumtumainia Mungu pamoja na ahadi zake za kuleta mkombozi.

I. Kaini alikataa kumsikiliza Mungu na akamuuwa Habili.

- **Soma Mwanzo 4:8 –** Hasira ilimuingia Kaini akakataa kumtii Mungu. Alikuwa akimsikiliza shetani kama mamaye na babaye walivyofanya katika Bustani la Edeni.
- Je, unafikiria ni nani aliyeweka mawazo ya kuuwa Habili katika mawazo ya Kaini? Shetani. **1 Yoh 3:12 –**
- Mwanzoni, Shetani aliwauwa wazazi wa Kaini. Aliwaambia hamtakufa ila mtakuwa sawa kama yeye. Msimsikilize Mungu, yeye anataka kuficha tunda nzuri msile. Lakini Shetani alijua wazi kuwa iwapo Adamu na Hawa watalila tunda hili la mti wa mema na mabaya, wangekufa. Shetani alitaka Adamu na Hawa wafe, na alitaka Kaini amuuwe Habili. Shetani ni muuwaji.
- Shetani anawachukia watu wote na atawadanganya ili kutuongoza sisi sote katika hukumu ya milele mahali ambapo yeye anaenda.

J. Hukumu ya Mungu kwa Kaini.

- **Mwanzo 4:9 –** Ingawa Mungfu aliuliza swali hili, je, hakujua kuwa Kaini alikuwa amemuuwa Habili? Ukweli Mungu alijua. Alimwona akiuwa.
  Mungu ako kila mahali kila wakati na anajua yote**. Mithali 15:3 –** macho ya Bwana Mungu yapo kila mahali; yanachunguza mabaya na mema.
- **Mwanzo 4:10-15 –** kwanza lazima tuelezee alama ya Kaini, sio alama juu ya Kaini, ila ilikuwa nadhiri ya Mungu kuwa angemhifadhi dhidi ya yeyote ambaye angejaribu kumuuwa. Mungu ndiye hulipa kisasi cha dhambi**. War 12:19 –** msijilipisie kisasi.
- Uovu wote kinyume na watu, ni kinyume na Mungu**. Zab 51:4 -** nimekutenda dhambi wewe pekee yako.
- Mungu ni muumba wa watu wote, watu wote ni wa Mungu (**Ezekieli 18:4**) kwa hivyo huadhibu yeyote anayenena au anayemtendea mwenzake jambo lolote ovu.
- Hii haimanishi kuwa, Mungu analipisha kisasi papo hapo kwa kila uovu, lakini malipo yote ya dhambi hatimaye hulipwa kwa Mungu**. Mhubiri 8:11 –**

- Kumbuka mshahara wa dhambi ni mauti. Hamna malipo mengine yoyote yanayoweza kukubalika.
- **Mwanzo 4:16 –** bado Kaini hangemsikiliza Mungu.
- Aliondoka akamwacha Mungu akafuatana na Shetani.

K. Uzao wa Kaini ulipenda vitu vya kawaida.

- Uzao wa Kaini ulifuata mfano wake. **Mwanzo 4:17-24 –** kama vile tunavyoona kwenye vifungu hivi, Mungu hakuwa na nafasi maishani mwao. Waliishi bila kufikiria lolote kumhusu Mungu. Bali, maisha yao yalidhamini mambo ya kawaida. Walijenga miji, walifuga ng'ombe, walitengeneza vyombo mbalimbali pamoja na ala za muziki.
- Hivi vitu vyote havina shida yoyote; shida iliyokuwa ni kwamba walijishughulisha navyo zaidi na kumsahau Mungu.
- Walitumia wakati mwingi na fikira kujishughulisha na mambo waliyotaka kufanya wao wenyewe.
- Waliongozwa na Shetani.
- Madhara makubwa yaliyoje kutomwamini na kutomtii Mungu yaliyoletwa ulimwenguni kwa tendo la dhambi ya Adamu na Hawa; uzao wao wote walizaliwa wenye dhambi, wakiwa wametengana na Mungu na hawangeyasikiliza maneno yake. Kama matokeo, wana wa Kaini pamoja na wanao pia walienda njia zao badala ya njia ya Mungu.
- Kuna funzo kwetu kwa hili pia ikiwa sisi ambao ni wazazi tutakataa kweli ya Mungu na tukatae kumsikiliza Mungu watoto wetu pia watakataa kumsikiliza.
- Kwa nini kuna wakristo wengi wachanga ambao ni waasi? **1 Petero 5:2-3**

L. Mungu alipeana Sethi kwa nafasi ya Habili.

- Mungu aliwapa Adamu na Hawa mtoto mwingine kwa nafasi ya Habili. Kumbuka, katika bustani Mungu aliahidi kumleta mkombozi ambaye angemshinda Shetani.
- Huyu mkombozi ilikuwa azaliwe kwa uzao wa Habili aliyemwamini Mungu.
- Lakini Shetani alimwelekeza Kaini kumuuwa Habili, kwa nini? Kuharibu mpango wa Mungu wa kumleta mkombozi.
- Hata hivyo, huu haukuwa mwisho wa mpango na ahadi ya Mungu. Mungu hufanya yote anayoahidi, yeye haachi wala habadili mawazo yake. Kwa sababu ya mambo ambayo Shetani anafanya.
  Kwa nafasi ya Habili, Mungu aliwapa Adamu na Hawa mtoto wa kiume (Sethi)
- Sasa kumbuka kuwa pia Sethi alizaliwa mwenye dhambi akiwa ametengana na Mungu lakini alimtumainia Mungu kama vile Habili alivyofanya.

SOMO LA 6

Mungu aleta gharika duniani – Mwanzo 5:1, 8:2

Mungu aleta gharika duniani.

A. utangulizi.

- Katika somo lililopita tuliona baada ya kuanguka kwa mwanadamu. Matokeo mabaya ya dhambi yalipitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Adamu, Hawa,Kaini, Habili**. War 5:12 –**

B. kutoka kwa Adamu hadi Nuhu.

- Tunaenda kutazama mwanzo 5 na tuone vizazi kutoka kwa Adamu na Hawa hadi kwa nuhu na gharika.
- Kutoka kwa Adamu hadi kwa Nuhu kulikuwa na wanaume kumi katika uzao wa Sethi waliomwamini Mungu na kuendelea kumtazamia Mungu kumleta mkombozi aliyeahidi katika bustani mwa Edeni. Tunawaona wametajwa katika **Mwanzo tano** (tazama majina na maana yake na ujumbe ambao Mungu alikuwa akipitisha kupitia kwao).
- Sethi (ameteuliwa), Enoshi (mtu wa mwili), Kenani (Huzuni), Mahalaleli (Mungu wa Baraka), Yaredi (alishuka chini), Henoko (akifundisha), Metuzela (kifo chake kitaleta), lameki (wakusononeka), Nuhu (faraja).
- Tukiweka majina haya kaitka sentesi, itasomeka hivi, **“imeteuliwa kwa mtu wa mwili huzuni lakini Mungu wa Baraka atashuka chini, akifundisha kuwa katika kifo chake kitaletea mwenye kusononeka faraja.”**

C. Ulimwengu wakati wa Nuhu.

- Kile ambacho tunataka tusome kinatuelezea kuhusu neema ya Mungu kwa Nuhu na wanawe wakiume watatu Shemu, Hamu na Yafethi na familia zao.
- Hadithi ya Nuhu ilitendeka miaka 1500 au zaidi baada ya uumbaji wa Adamu, wakati wa Nuhu, Shemu, Hamu na Yafethi, tulikuwepo na watu wengi walioshi ulimwenguni. **Mwanzo 6:1 –** tuchukulie kuwa hesabu ukuaji wa tarakimu ni kama wa sasa, inamaanisha watu walikuwa takribani bilioni tatu na zaidi walioishi ulimwenguni wakati ule.
- Lakini wengi zaidi walipendezwa tu kufanya yale waliowaza kuwa mema kwao wakati huo.
- Walitawaliwa na uasherati. **Mwanzo 6:2 –**
- Hawakuwaza lolote kuhusu jinsi ya kumpendeza Mungu.
- Mungu aliwaona na akachukia dhambi lakini aliwapenda watu na aliwataka watubu (wabadili mawazo yao**) 2 Petro 3:9**
- Mungu aliwataka watu wakati wa Nuhu wabadili mawazo yao.
- Alitaka wakubali kuwa walikuwa wamekosa.
- Alitaka wamwamini.
- Aliendelea kuwaelezea lakini hawakumsikiliza**. Mithali 1:24-32**
- **Mwanzo 6:3** – Mungu aliwadhahatarisha kuwa hangeendelea tu kuwapa ujumbe huu.
- Kama wataendelea kumpuuza siku moja angeliwapeana kwa Shetani na awaadhibu.
- Wazo; Mungu hunena nasi kupitia kwa neno lake.
- Alisema atawapa miaka 120 ya kubadili mawazo yao la sivyo Mungu awaadhibu.
- Wazo la kufurahisha ni kwamba Mungu hunena nasi kupitia kwa neno lake; lakini shetani naye hunena nasi kama tu alivyonena na Hawa akisema usimsikize Mungu.

- Hata hivyo, tukikataa kumsikiza Mungu na Roho wake ambaye amekuwa akitunenea anaweza kunyamaza, huenda hataendelea kutushawishi ili tumwamini Mungu atatuwachilia twende njia yetu. **War 1:18-32**. Gundua Mungu aliwaacha katika tamaa za mioyo yao waufuate uovu wao katika **msitari wa 24,26 na 28.**

D. Uovu ulioenea.

- **Mwanzo 6:5-11 –** watu wengi walifuata njia sisizo za kiungu, za Kaini. Waliendelea zaidi na zaidi katika dhambi. Walikataa kuamini ujumbe wa Mungu na kumtumainia katika rehema yake.
- Kumbuka watu hawa walizaliwa wenye dhambi na wakapenda dhambi zao. **Waeb 11:25 –**
- Mungu alinena na watu wakati wa Nuhu kupitia kwa manabii.
- Mmoja katika kizazi cha Sethi, Henoko alikuwa nabii wa Mungu. **Yuda 14-16**
- Nabii mwingine wa Mungu aliitwa Nuhu. **2 Petro 2:5 –** nataka kuelezea hivi kuhusu watu wa nyakati za Nuhu hawakuwa na la kujitetea kuhusu tabia zao. Mungu aliendelea kuwaonya mara kwa mara kupitia kwa manabii, Henoko na Nuhu.
- Walikuwa wakimwasi Mungu tu.
- **Mwanzo 6:5 –** inatueleza kuwa kila mawazo ya mwanadamu awazayo moyoni daima ni mbaya.
- Mawazo yao iliekemea vitu vya asili kwa miili yao na kujitakia maendeleo ya kibinafsi.
- Walikuwa na kiburi, ubinafsi na wakujisifu, walikuwa na wivu na chuki kwa wengine. Walikuwa na ugomvi na kupigani, walikuwa wenye fujo na wengi walikuwa wauwaji. Waliendelea kwa ujanja, uongo na kudanganya mmoja kwa mwingine. Walifanya biashara bila huruma na kuwaibia wengine. Walieneza fitina wakawa na tamaa ya anasa**. 2 Tim 3:1-5.** (Tazama, katika "nyakati za mwisho" ya kila majira, yote huishia katika dhambi na hukumu ya Mungu.)

E.Mungu aliuona ulimwengu usio amini na dhambi yake.

- **Mwanzo 6:11,12 –** Mungu aliona dhambi zao zote .
- Huenda waliuficha uongo wao, uasherati, wizi na uuwaji wengine wasione, lakini hakuna lolote lililofichwa kwa Mungu. Yeye aliona yote.
- Hatuwezi kumficha Mungu lolote, **Waeb 4:13 –** mambo yote yako wazi machoni pa Mungu.

F.Mungu aliamua kuangamiza Ulimwengu.

- **Mwanzo 6:6, 7 –** watu walikuwa waovu kiasi kwamba Mungu akisema, atawaangamiza pamoja na kila kitu alichoumba ulimwenguni.
- Kumbuka katika bustani, Mungu aliwanenea, Adamu na Hawa kuwa msipoamini na kutii mtakufa. Mtatengana nami. Walikataa kuamini na wakafa jinsi tu Mungu alisema. Pia aliwaelezea wazi Kaini na Habili kuwa kama walitaka kumwendea na wakubalike, ilikuwa lazima wamletee kondoo na wamwage damu yake , Mungu alimaanisha kile alichosema na kwa hivyo alikataa sadaka ya Kaini kwa kuwa Kaini alijifanyia kwa njia yake . Sasa kwa wakati wa Nuhu Mungu alisema anaenda kuuangamiza ulimwengu mzima na wanadamu wote kama hawangeziacha njia zao mbovu. Hivi havikuwa vitisho tu.
- Ni mara ngapi huwa tunatoa vitisho wakati tumekasirika na kusahau baada ya kupoa?
- Mungu sio kama sisi. Yeye hufanya yote anayosema.

G. Nuhu anapata Neema machoni pa Bwana.

- Hata hivyo, kwa sababu ya upendo na rehema ya Mungu, kuna mtu mmoja pamoja na jamii yake ambaye Mungu hakuwa anaenda kumwangamiza.
- **Mwanzo 6:8-10 –** kumbuka Nuhu alizaliwa mwenye dhambi chini ya utawala wa Shetani kama uzao wote wa Adamu.
- Hakusitahili kuokolewa na Mungu.

- Hata hivyo Nuhu alimwamini Mungu na kumjia kama vile Habili, Sethi na Henoko, akileta damu ya wanyama**. Mwanzo 8:20 –**
- Kumbuka lazima mwanadamu awe na imani ili ampendeze Mungu. **Waeb 11:6** – lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu**. Waeb 10:38** –
- Nataka kueleza hivi; tunasema mara nyingi kuwa jukumu letu la pekee ni kuamini na hapa kuna mtu mwenye dhambi, Nuhu aliyeamini tu na sasa kwa neema na rehema za Mungu alisamehewa na Kukubalika na Mungu.

H. Mungu alimpa Nuhu maagizo.

- **Mwanzo 6:13 –** Mungu alimwambia Nuhu kuwa anaenda kuleta gharika ambayo itaifunika nchi yote, lakini hakusema tu kuwa, "Nuhu, ninaenda kuuhukumu ulimwengu. Naenda kuleta gharika kuu na ni afadhali utende jambo kuhusu hili. Anza kujenga safina."bali Mungu alimpa maagizo ya jinsi ya kujenga safina. **Mwanzo 6:14-21 –**
- Kumbuka baada ya Adamu na Hawa kutenda dhambi walijitengenezea mavazi wenyewe. Mavazi waliyojitengenezea hayakukubalika na Mungu. Mavazi yao yalikuwa yawe ambayo Mungu alitaka. Sadaka ya Kaini na Habili ilibidi iwe kulingana na mapenzi ya Mungu. Vivyo hivyo safina ilikuwa ijengwe kwa mpango wa Mungu.
- Mungu alijua kabisa vile safina ilitakikana kujengwa, na kwa hivyo alimpa Nuhu maagizo kwa makini.
- Kumbuka, aliumba ulimwengu; aliziweka sheria za kuelekeza vyote vinavyoelea, kwa hivyo hakuwa na shida ya kutengeneza safina kubwa.
- Ningependa kushiriki utafiti kadhaa kuhusu safina. Safina ilikuwa chombo kamili kilichostahili. Umbo, futi miatatu urefu wa safina futi hamsini upana wake, na futi thelathini kwenda juu kwake. Ingeweza kubeba takribani tani 14,000. Ilikuwa na uwezo wa kubeba magari iliyoundwa kwa vyuma vya reli tani takribani 522. Kila gari likibeba kondoo 240. Inasemekana kuwa tulikuwa na aina 17600 ya wanyama, inayofikisha hesabu ya 45,000 nambari ambayo huenda Nuhu aliweka kwenye safina. Kuna jambo moja ambalo tunatakiwa kukumbuka jinsi mungu alimweleza Nuhu kujenga safina.
- Mungu alimweleza kuweka mlango mmoja tu katika upande wake**. Ms 16.**
  Ilitakikana kuwa na njia moja tu ya kuingia ndani. Kila mtu na kila mnyama ambaye angeokolewa dhidi ya hukumu ya Mungu alikuwa aingie kwenye safina kupitia mlango mmoja, walikuwa waingie kwa njia ya Mungu, **Yoh 10:7-9,14:6, Mathayo 7:13,14.**
- Kulikuwepo safina moja pekee ambamo watu wote wangeokolewa kutokana na hasira ya Mungu na kulikuwepo na mlango mmoja tu wa kuingia kwenye safina.

I. Nuhu alimtii Mungu.

- **Mwanzo 6:22 –** Nuhu alimwamini Mungu. Alimtumainia Mungu na kumtegemea kwa wokovu wake pamoja na jamii yake. **Waeb 11:7 –**
- Kumbuka, hakukuwa kumewahi kunyesha ulimwenguni, hata mafuriko haikuwahi kuwepo. Hadi wakati huu, maji ulimwenguni yalikuwa yanatokana na ukungu ukipanda katika nchi, ukitia maji katika uso wote wa ardhi.**Mwanzo 2:6 –**
- Licha ya hayo, Nuhu aliamini kuwa Mungu hawezi danganya wakati anasema ataleta mvua na mafuriko. Nuhu alimwamini Mungu kwa hivyo akatii na kujenga safina kama vile Mungu alikuwa amesema, fikiria yale ambayo angeyapitia**, "Nuhu,unasema kutanyesha?!"**

J. Mungu alimwambia Nuhu kuleta jamii yake, wanyama, pamoja na ndege kwenye safina.

- **Mwanzo 7:1-5; Yakobo 2:18 –** nitakuonyesha imani yangu kwa matendo.

- Kumbuka jinsi Nuhu alivyomwamini Mungu **(mwanzo 7:5 -)** aliwatahadharisha watu kuhusu hukumu ya Mungu iliyokuwa inakuja, lakini watu hawakuamini maneno ya Mungu.
- Walikataa kukubaliana naye kuwa walikuwa wamekosa na walistahili ghadhabu ya Mungu.
- Hawakumtumainia Mungu kwa ahadi ya siku moja kumleta mkombozi, wala hawakumwamini Mungu kuwa angeiharibu nchi kwa gharika kuu.
- Mungu aliwavumilia kwa miaka 120 iliwabadili nia zao lakini sasa hangengojea tena, ulikuwa wakati wa Mungu kuachilia ghadhabu yake.
- Hata hivyo, Nuhu alipata neema machoni pa Mungu. **Mwanzo 6:8 –**
- Mungu hakumwokoa Nuhu eti kwa kuwa alikuwa anaishi vizuri.
- Mungu alimwokoa kwa sababu ya imani yake… alimtumainia Mungu.

K. wote waliingia kwa mlango mmoja.

- **Fungua sasa katika mwanzo 7:15-16 –** Nuhu pamoja na jamii yake yote waliingia kwenye safina kupitia mlango mmoja. Hii ndiyo iliyokuwa njia ya pekee ambayo kila mmoja angeweza kuokolewa kutokana na gharika pamoja na hasira ya Mungu kuelekea dhambi. Wanyama wote pia waliingia kwenye safina kwa kutumia mlango mmoja.

L. Mungu alifunga safina.

- Baada ya vyote kuingia ndani, ni nani aliufunga mlango? Mungu (**ms 16**) kwa nini hangeufunga mlango?
- Mungu hakuwa na wakati zaidi wa kungoja watu wabadili mawazo yao na kuamini. (baada ya kuhubiri miaka 120 na kumwaga moyo wake kwa watu. Sidhani kama Nuhu angewafungulia). Mungu aliufunga mlango kama wakati umeisha.
- Hata kama wangelia na kuhurumisha nje hawangeingia kwenye safina. Nuhu hangewaruhusu waingie kwa sababu ni Mungu aliyewafungia nje. Hawangepata tena njia ya kuwaokoa.
- Wakati Mungu aliwaondoa Adamu na Hawa kutoka bustani mbali na mti wa uzima, je, walikuwa na njia ya kurudi tena? La, haikuwepo. Wakati Mungu anaamua ni wakati wa kuadhibu ulimwengu hakuna njia ya kuhepa.

M. Mungu aliwaangamiza wote waliokuwa nje ya safina.

- **Mwanzo 7:17-23 –** Baada ya Mungu kuufunga mlango wa safina, aliachilia mvua. Kumbuka Mungu anatawala uumbaji wote. Yeye ndiye aliviumba vyote na anavitawala.
- Maji yalikuwa mengi kiasi cha kuufunika ulimwengu wote. Hata na milima mirefu. Je, maji haya yote yalitoka wapi?
- Je, unakumbuka vile ulimwengu ulikuwa mwanzoni baada ya Mungu kuumba? Kulikuwa na giza na maji yalifunika ulimwengu mzima.Siku ya kwanza, Mungu aliumba nuru. Siku ya pili alitengeneza hewa na mbingu na akaweka maji zaidi katika mbingu**. Mwanzo 1:6 –**
- Sasa wakati Mungu aliwachilia gharika, aliyafungua madirisha ya mbinguni na kwa mara ya kwanza kukanyesha.
- Hii haikuwa mvua ya kawaida, maji yalimwagika.
- Maji mengine yalitoka chini kwenye chemchemi za vilindi. **Mwanzo 8:2** – Mungu anaweza kufanya lolote, hamna lisilowezekana na Mungu. Yeye pekee ndiye mkuu.
- Kwa hivyo mvua ilinyesha kwa siku arobaine hata na usiku pia hadi ulimwengu wote ukafunikwa kwa maji na kila mwanamme, mwanamke na mtoto nje ya safina alikufa. Takribani watu bilioni tatu.
- Mungu ni mtakatifu na mwenye haki. Yeye ni Mungu wa upendo, lakini pia ni Mungu wa hasira kwa dhambi. **War 1:18.**
- Lakini Nuhu na jamii yake walimwamini Mungu, na wakashinda gharika wakiwa salama ndani ya safina.

SOMO LA 7

Mnara wa Babeli –Mwanzo 11:1-9

Abramu anaitwa na Mungu –Mwanzo 11:11-12:5

Mnara wa Babeli .

A.Utangulizi

- Somo la mwisho liliisha na Mungu akileta mvua kwa siku 40 na usiku 40 mpaka dunia yote ikajaa maji ikifunika na milima mirefu na miti.
- Kila mume, mke, mtoto na mnyama aliyekuwa nje ya safina alikufa kwa gharika.
- Tunajua kuwa Mungu ni mtakatifu na wa haki na upendo,lakini pia ni wa hasira kinyume na dhambi **Warumi 1:18**
- Hata hivyo, Nuhu na familia yake walipata neema machoni pa Bwana….Kwa nini? Kwa sababu walimwamini Mungu**. Mwanzo 6:8; Waebrania 11:7.**

B.Watu wa Babeli

- **Mwanzo 11:1-4** Miaka mingi ilikuwa imepita baada ya Mungu kumuokoa Nuhu, mkewe, wanawe watatu na wake wa wanao kutokana na gharika kuu, na mara nyingine tena watu wengi walikuwa wanaishi duniani. Wengi wa hao watu walisahau hukumu ya Mungu kwa dunia kupitia kwa gharika na wakamkataa Mungu tena.
- Hawakutaka kujua kuhusu au kumwamini Mungu kama Habili, Sethi na Nuhu. Walikataa mapenzi ya Mungu juu ya maisha yao.
- Walikuwa chini ya uelekezo wa shetani na kama shetani, wao pia walitaka kuwa wakuu na wakajiinua wenyewe. Hawakuwa na shukurani na hivyo hawakumpa Mungu heshima anayostahili.
- Waliamua kugeuka kutoka kwa kile walikijua ni kweli kumuhusu Mungu.
- Walitengeneza sanamu za watu na kuziabudu. Waliabudu wanyama na ndege. Hii ndiyo shetani anataka; watu wanaoabudu miungu. Kuna watu wengi leo hii ambao bado wanaabudu jua, mwezi, nyota, ndege na jeshi lote la miungu ya uongo. **– (dini ya kihindi ina milioni 33 ya miungu).**
- Ni rahisi kwetu kuangalia watu wanaofanya vitu hizi na tuone ujinga wao.
- Tunafikiria kuwa hakuna watu wengi hapa Merikani ambao wanajihusisha na kuabudu sanamu. Ilihali tunaona kwenue magazeti ya kila siku nyota zimewekwa. Tunaona watu wanaingia zaidi na zaidi kwenye madeni kwa sababu ya kuabudu mali ya dunia. Tunaishi katika jumuia ambayo inaogopa kuvunja kio au kutembea chini ya ngazi au kuvuka njia yap aka mweusi. Je, Mungu anahusika wapi kwa hayo yote?
- Nataka kusema hivi –Ibada hutoka kwa neno “kustahili” na inaonyesha kitu kinastahili. Mungu na ni Mungu pekee ndiye anastahili upendo wetu na ibaada**. Yohana 4:23, 24.**
- Shetani hajali kile tunaabudu mradi hatuabudu Mungu pekee wa kweli na aishiye. Na tunaweza kuwa na uhakika kuwa wajenzi wa mnara wa Babeli hawakuwa wanafikiria kumhusu Mungu wala kumuabudu.

C.Mungu ni mkuu na mtawala.

- **Mwanzo 11:4** Hawa watu walikuwa wanafikiria kumhusu nani? Walikuwa wanamwabudu nani? Hawa watu walikuwa wamejawa na ubinafsi wao. Iliwapasa kuliinua jina la Mungu sio lao. Lakini tukiangalia kifungu cha mwisho cha mstari huu, “tusiche tukatawanywa”.Nini ingine ilikuwa mbaya hapa? Je, unakumbuka amri ambayo Mungu alimpa Adamu na akairudia kwa Nuhu na uzao wake?
- **Mwanzo 1:28, 9:1** –Mzaane muongezeke na muijaze inchi. Ijapokuwa Mungu alimwambia Adamu na Nuhu ya kuwa waongezeke waijaze inchi, hawa watu waliamua kuasi hii amri. Hawakutaka kutawanyika ulimwenguni kote vile Mungu aliamuru. Na hivyo, walikusanyika mahali pamoja, wakajenga mji, na kuanza kujenga mnara mrefu.

D.Mungu aliwaona.

- **Mwanzo 11:5** Mungu alikuwa na haja ya hawa watu ingawa walikuwa wamemsahau. Tumesema haya awali, lakini naamini twahitaji kuisema tena –Hakuna anayemuasi Mungu na akafaulu.
- Wakati shetani alikuwa mbinguni alijaribu kuasi kinyume na Mungu na akashindwa, malaika wengine walioasi na shetani pia walishindwa. Adamu na Hawa pia walishindwa walipoasi na vile vile Kaini na watu wa nyakati za Nuhu.
- Nini itatendeka hapa?

E. Mungu awatawanya waasi.

- **Mwanzo 11:6-9** –Je, unakumbuka kwamba Mungu katika **Mwanzo 1:26** alijadili vile alikuwa anaenda kumuumba mwanadamu? “Wacha na tumuumbe mwanadamu kwa sura yetu”.
- Tena katika mstari wa 6, 7 tunaona Bwana –Mungu baba, Mungu mwana na Mungu Roho Mtakatifu – akijadili kile anaenda kukitenda.
- Bwana aliwasababisha watu waongee lugha tofauti tofauti. (Muujiza mkuu hapa sio kwamba Mungu aliwapa lugha mpya bali aliondoa ile ya kwanza). Na kwa vile hawangeelewana, ilibidi watawanyike kwa vikundi kulingana na lugha zao na kuenda kwa maeneo tofauti ya inchi. Baada ya miaka mingi walitawanyika ulimwenguni kote ambapo illikuwa mpango wa kwanza wa Mungu. Mwanadamu ilikuwa aijaze ulimwengu wote, sio sehemu moja tu.
- Hiki kifungu katika Mwanzo kinatuelezea vile mataifa na makabila yalivyoanzi shwa.

F. Hitimisho

- Agano la kale ni muhimu vile inatuonyesha jinsi Mungu alivyo na vile anavyohusika na mwanadamu. Hizi hadith za kale zaonyesha mtindo wa maisha ya sasa. Waume kwa wake wanaendelea kumuasi Mungu, na Mungu hawezi badilika, bado anahukumu dhambi kwa sababu anataka watu wamwamini.

Mungu alimchagua na kumwita Abramu .

A.Abramu alikuwa ni kizazi cha Shemu.

- Fungua nami katika **Mwanzo 11:11**. Hapa tunaona mwanzo wa kizazi cha mojawapomwa wana wa Nuhu, Shemu. Katika mstari wa 27 tunafahamishwa kuhusu Abramu aliyetokana na uzao wa Shemu. Abramu aliishi karibu na mahali watu walikuwa wameanza kujenga mnara wa Babeli.
- **Mwanzo 11:27-30** –Tunaona hapa, Abramu alimuoa Sarai, lakini hawakuwa na watoto. Na katika siku hizo, kutokuwa na uwezo wa kupata watoto ilikuwa ni aibu. Wale ambao hawakuwa na watoto walidharauliwa katika jumuia. Watoto wa kiume walitamanika sana ili mtu awe na mrithi wa kuendeleza jina la familia. Hata hivo, Abramu na Sarai hawakuwa hata na binti pekee.

- **Mwanzo 11:31,32** – Terah alitoka Ur (Mesopotamia) na akaenda mpaka Harani na Abramu, Sarai na Lutu. Alikuwa amepanga kwenda mpaka Kanaani lakini akafa akiwa bado Harani, **Mwanzo 12:1.** Inafurahisha kwamba, Mungu alikuwa amemwambia Abramu kuacha inchi yake na kwenda kwa inchi ya Kanaani kabla yeye kuondoka na babake hadi Harani –**Matendo Ya Mitume 7:2,3.**
- Kuwa na ufahamu kuwa mahali Abramu aliishi huko Mesopotamia watu waliabudu sanamu. Hawakutumaini, kupenda au kumtii Mungu.
- **Yoshua 24:2** Inatuambia kuwa Terah babake Abramu aliabudu sanamu.
- Lakini Abramu alimwamini Mungu. Hivo basi, mpango wa Mungu juu ya Abramu haungekamilika wakati alikuwa angali anaishi katika inchi na watu wanaoabudu miungu. Hivyo, Mungu alimwambia aondoke kutoka katika inchi yake na aende kwa inchi ambayo Mungu atamwelekeza.
- Je, Mungu alikuwa na haki ya kumuelezea Abramu kile anastahili kutenda? Ndiyo. Kwa nini? Kwa sababu Mungu alimuumba na Abramu alikuwa wake.
- Babu zetu, kizazi cha Nuhu katika mnara wa Babeli walikusudia kugeuka kutoka kwa Mungu na kwa ukweli.
- Waliabudu vitu ambavyo Mungu aliviumba badala ya Mungu muumba wao. Licha ya dhambi zao, Mungu hakuacha mpango wake wa kumwokoa mwanadamu kutoka kwa nguvu za shetani na hukumu ya milele.
- Hakuna mtu au kitu chochote kinachomzuia Mungu kukamilisha mipango yake. Tazama **Isaya 46:8-10; Zaburi 115:3; Zaburi 135:6.**

B.Mungu alimuita na kumuamru Abramu.

- Abramu kuitwa ilikuwa ni hatua nyingine ya Mungu katika mpango wake wa kuwaokoa wanadamu kutoka katika umateka wao wa dhambi. Leo hii bado Mungu ni yule yule vile alivyokuwa katika siku za Abramu. Bado ni wa upendo, rehema na neema. Hajasahau mpango wake wa kuwaokoa watu kutoka kwa hukumu ya milele. Anataka kila mmoja aokolewe kutoka kwa nguvu za shetani na dhambi.

C. Ahadi za Mungu kwa Abramu.

- Hebu tusome ahadi za Mungu kwa Abramu. **Mwanzo 12:1,2**. Tazama kile Mungu alisema…(Nitakufanya taifa kuu). Ijapokuwa Abramu na Sarai hawakuwa na watoto, bado Mungu alimuahidi Abramu kuwa atakuwa baba wa taifa kuu.
- **Mwanzo 12:3** –Mungu hapa, anaahidi kuwabariki wale ambao walimsaidia Abramu, lakini ataleta uovu juu ya wote ambao walimtenda vibaya. Mwisho wa mstari wa tatu unasema, kupitia kwako jamii zote za ulimwengu zitabarikiwa.
- Hii ndiyo ahadi kuu kw azote alizopewa Abramu kwa sababu ni kuhusu Mkombozi. Kumbuka somo letu katika shamba la Edeni, na vile Mungu aliahidi kumtuma mkombozi duniani kuponda ponda nguvu za shetani. Mungu sasa anaahidi kuwa mmoja kutoka kwa uzao wa Abramu ndiye atakuwa yule mkombozi. Jamii zote za ulimwengu zitabarikiwa kupitia kwa uzao wake. **Wagalatia 3:8,9**.

D. Abramu aliamini na kumtii Mungu.

- Kumbuka Abramu alikuwa anaishi kati ya watu waabudu sanamu, ulimwengu wa dhambi na alitoka kwa familia ambayo haikumwabudu Mungu.
- Waume na wake waliomuasi Mungu na kufuata tamaa zao wenyewe walimzunguka, kama ilivyokuwa na Nuhu.
- Pia kumbuka Abramu na Sarai hawakuwa na mtoto na licha ya mazingira yake na hali zake na musukumo kutoka kwa wenzake, Abramu aliamini ahadi za Mungu. Aliamini kuwa Mungu

atatuma mkombozi atakayetokana nauzao wake. **Warumi 4:19-22 ,** mistari mingine ni **Warumi 4:3** na **Mwanzo 15:6**. Haki ni nini? Mungu alimhesabu Abramu kuwa mwenye haki. Alikuwa mwenye haki juu ya nini? Aliamini nini? Aliamini kuwa Mungu atamtuma mkombozi kumuokoa mwanadamu kutoka dhambini. **Wagalatia 3:8,9.**

- **Mwanzo 12:4, 5** –Abramu alikuwa tajiri sana na alikuwa na watumishi wengi, ng'ombe, kondoo na mbuzi. Alichukuwa vyote alivyokuwa navyo pamoja naye.
- Nataka kusema hivi – Abramu aliamua kuenda kwa sababu alimwamini Mungu.
- Je, waweza chukuwa vyote ulivyonavyo pamoja na familia yako na miliki yako yote na kwenda kwa inchi ya kigeni kwa ajili ya kumtii Mungu ambaye majirani wako wote wamemdharau? Kumbuka, Abramu alikuwa mtu wa mali na msimamo. Watu walikuwa wakimtazama. **Waebrania 11:8**.
- Na mbaya zaidi ni kwamba, Abramu alikuwa asafiri na kuishi kwenye mahema. **Waebrania 11:9**.
- Licha ya yote, Abramu alimwamini Mungu na kumtii, akikabidhi jamii yake yote na miliki yote katika ulinzi wa Mungu. Abramu alijua kuwa Mungu anastahili kutumainiwa kwa vyote.
- Lutu mtoto wa nduguye Abramu pia alimwamini Mungu na kumtumainia katika ahadi zake, hivo alienda na Abramu na Sarai.

E. Vita kati ya wachungaji wa Lutu na Abramu.

- **Mwanzo 13:5-7** –Lutu pia alikuwa tajiri kama Abramu na kwa sababu wote walikuwa na kondoo na ng'ombe wengi, haikuchukuwa muda na vita zikazuka.

F.Suluhisho ya Abramu.

- Hata hivo Abramu alikuwa na suluhisho aliomwambia Lutu. **Mwanzo13:8, 9**- Mawazo yenu ni ipi? (**Wafilipi 2:3,4**)

G. Uchaguzi wa Lutu.

- **Mwanzo 13:10, 11** –Lutu alitazama na akachagua inchi tambarare iliyokuwa na nyasi aliyofikiria itakuwa nzuri kwa wanyama wake. Ijapokuwa Lutu aliamini Mungu na kumtumaini, hakuwa anafikiria jinsi kuondoka kwake kutaadhiri familia yake na pia uhusiano wake na Mungu.
- Alikuwa anafikiria kujihusu yeye mwenyewe na kuongezeka kwa utajiri wake ambayo haikuwa na Abramu.

H. Hitimisho.

- Kumbuka uamuzi mbaya wa Kaini kumpuuza Mungu, uzao wake wote ulikufa kwa gharika. **Mithali 14:12**.
- Lazima tuwe waangalifu kwa uchaguzi tunaofanya. Katika jumuia yetu tunasukumwa kufanya uamuzi ambao hauna uthamana wa milele. Tutatengeneza aje pesa nyingi? Tutanunua nini? Tutaenda wapi kwa ligizo?
- Lakini maswala halisi ya maisha haitajwi. Je, uhusiano wetu na Mungu ni upi? Watoto wetu wanajua nini kumhusu Mungu?
- Abramu alipaki mahali pa mawe na milima na penye hapakuwa na rutuba nyingi. Naye Lutu alienda penye palikuwa na rutuba.
- Katika macho ya wanadamu inaweza onekana kama Abramu alishindwa kwa hii.

SOMO LA 8

Sodoma na Gomora. Mwanzo 13:11-13 na 18:20-19:29

Kujaribiwa kwa imani ya Ibrahimu. Mwanzo 21:1-22:19

Sodoma na Gomora .

A. Utangulizi.

- **Mwanzo 13:12,13 –** Ndani ya ponde ambamo Lutu alichagua palikuwa na miji miwili yenye uovu zaidi.
- Watu walioishi kule hawakutaka kujua lolote kumhusu Mungu wala kutenda chochote ambacho Mungu alitaka wafanye.
- Mungu alijua hili na angemweleza Lutu kama tu angemuuliza. Lakini Lutu alipuuza hilo na akafanya kile kilichoonekana sawa kattika macho yake na kwa hilo akafanya jambo hatari la kwenda mbali zaidi na Mungu.

B. Nia ya Mungu kuhusu sodoma na Gomora.

- Fungua nami **katika Mwanzo 18:20,21** tunamwona Mungu akinena na Ibrahimu kuhusu hali ya sodoma na Gomora.
- Tena Lutu alikuwa ameteremka kwenye kuishi kwenye miji hii ya uovu. **Mithali 4:13,14**
- Mungu alikuwa amekasirishwa na watu wa Sodoma na Gomora hata kabla ya Lutu kwenda huko.
- Kwa muda mrefu, alikuwa ameuvumilia uovu huu lakini sasa alikuwa ameamua kuwa hatauvumilia tena. Hawangeepuka hukumu ya Mungu.
- Je, unakumbuka jinsi Mungu aliwavumilia watu kumrejea katika wakati wa Nuhu? Hatimaye wakati uliwadia ambapo Mungu aliamua kuwa hapana tena wakati zaidi wa toba.Hakuna yeyote aliyekataa kukubaliana na Mungu ambaye aliepuka hukumu yake.
- Ni swala la kufikiria kwa kuwa Mungu huwa hahukumu dhambi papo kwa papo. Kwa hivyo yaweza kuonekana kuwa amepuuza tu .
- Lakini hatimaye hukumu yake huwadia**, Mhubiri 8:11, Zab 50:20,21**
- Maandiko ya kunifurahisha ni katika **Mwanzo 18:22-32.** Mungu hakuwa anaenda kuteketeza Sodoma na Gomora kwa sababu ya dhambi bali ni kukosekana kwa watu wenye haki**. Yeremia 5:1 –**

C. Malaika wa Mungu walikuja Sodoma

- **Mwanzo 19:1-3** Wacha tufikirie kuhusu mambo inavyoendelea hapa. Mwanzoni Lutu alikuwa anaishi karibu na mji **Mwanzo 13:10-12.** Sasa ameingia ndani na anaishi na watu waovu. **Zab 1:1-3 (kuendeleza) Waefeso 4:17-19.**
- Biblia anapeana undani Zaidi kuhusu dhambi ya Sodoma. **Ezekieli 16:49,50-** Hao watu walikuwa wa kiburi, wasinzi, walafi ambao hawakujali mahitaji yaw engine.

D. Dhambi ya Wasodomi

- **Mwanzo 19:4-7** Ni tashwira mbaya lakini Mungu ameiweka hapa kwa makusudi. (**1Wakor 10:11, Warumi 15:4**) Je, na jumuia ya leo iko vipi? Neno "ulawiti"(usodomi) bado ni lugha yetu kwa sababu bado hii dhambi ipo katikati yetu (**Warumi 1:26,27**).
- Kumbuka uchaguzi wa kwanza wa Lutu wa inchi nzuri. Sasa inaonekana tofauti katika hali ya uovu. Kama Mungu hangetuma malaika wake, Lutu na binti zake wawili wangekuwa na mwisho upi. Lakini Biblia inatuelezea kuwa Lutu alimwamini Mungu na Mungu akamuokoa. **2 Petro 2:6-9. Mwanzo 19:8-11-** Tazama tamaa iliozidi hata kwa kupigwa na upovu haungewazuia.

E. Lutu, mkewe na wanawe wa kike wanaokolewa kutoka Sodoma.

- **Mwanzo 19:12 – 17 –** Mungu hakuokoa Lutu na familia yake kwa kuwa wema, lakini ni kwa sababu Lutu aliamini ahadi ambazo Mungu aliwapa Ibrahimu na Adamu kuhusu kuja kwa mkombozi.
- Kwa hivyo malaika wa Mungu walimwongoza Lutu na familia yake kutoka Sodoma kabla ya kuuteteza mji .kila wakati Mungu huwaokoa wale wanaomtumainia na kukubaliana naye.
- Kumbuka Habili alikubaliana na Mungu na Mungu akamukubali **Waeb 11:4**
- Nuhu alikubaliana na Mungu na kumtumainia, na Mungu akamwokoa na gharika. **Waeb 11:7**
- Sasa pia Lutu alimwamini Mungu na kumtuminia na Mungu akamwokoa kutokana na kuteketezwa kwa Sodoma.

F. Mungu aliteketeza Sodoma na Gomora.

- **Mwanzo 19:24-25 –** wakati Lutu alifika nje ya mji, Mungu aliteketeza Sodoma na Gomora; kama vile aliuharibu ulimwengu wakati wa Nuhu sasa aliteketeza watu hawa waovu lakini sasa ni kwa Moto.
- Kumbuka **2 Petro 2:6** – akiipendua na kuifanya miji ya Sodoma na Gomora kuwa majivu, akaifanya iwe kama ishara ya wale wasiomcha Bwana. Uharibifu huu ilikuwa kama ishara kwa kile Mungu atakitenda kwa wale wasioamini.
- **MUNGU NI MWAMINIFU; YEYE HABADILIKI**. Bado yeye ni yule yule leo. Bado anachukia dhambi na hakuna yeyote anayeweza kuepuka hukumu yake.

G. Mkewe Lutu alitazama nyuma.

- **Mwanzo 19:26** – wakati malaika waliwachukuwa, Lutu, mkewe na wanao wakatoka nje ya Sodoma, malaika waliwaambia kuwa wasitazame nyuma wakimbie watorokee milimani. Lakini mkewe Lutu aligeuka akatazama nyuma. Mungu alijua kilicho kuwa moyoni mwake. Alikuwa kama Kaini. Yeye hakumtumainia Mungu na alipenda maisha ya Sodoma ya uovu kwa hivyo Mungu alimbadilisha akawa jiwe la jumvi**. Lk 17:32,33; 9:23,24**

H. Hitimisho.

- Kwa nini jiwe la jumvi? Dhambi humsababisha mtu kuwa na moyo mgumu. **Waeb 3:12,13**

Jaribio kuu la imani ya Ibrahimu. .

A. Utangulizi.

- Katika somo lililopita tulisoma kuwa, Ibrahimu alimtumainia Mungu na Mungu akamhesabia haki. **Mwanzo 15:6**
- Sasa tunaenda kujifunza juu ya jaribio kuu la imani ya Ibrahimu. Lakini zaidi ya imani ya Ibrahimu, ni Mungu ndiye mwaminifu zaidi tunayemwamini.

B. Mungu alitimiza ahadi ya kuwapa Ibrahimu na Sarai mwana wa kiume.

- Hata kama Ibrahimu na Sarai walikuwa wamezeeka zaidi ya kutompata mtoto, Mungu alikuwa ameahidi kuwapa mtoto. Hakuna lisilowezekana kwa Mungu**. Lk 18:27; Lk 1:37.**
- Kwa hivyo Ibrahimu na Sarai walimpata mwana wa kiume kama tu alivyoahidi Mungu. **Mwanzo 21:1-3**
- Miaka mingi ilipita na Isaka akawa kijana. Babake na mamake walimpenda na Ibrahimu aliamini kuwa ahadi zote za Mungu kumhusu mkombozi zingetimia kupitia kwa Isaka na uzao wake. Baadaye Mungu akamuuliza Ibrahimu kutenda jambo lisilotarajiwa.

C. Mungu alimwamuru Ibrahimu kumtoa Isaka kama sadaka.

- **Mwanzo 22:1,2** – Mungu alikuwa anamjaribu kuona kama alimpenda Isaka zaidi kuliko yeye. Ninakumbuka miaka yangu ya kwanza katika wokovu. Nilishangaa ni kwa nini hasaa Mungu alitenda hili, lakini fikiria kulihusu. Mungu hupeana uhai kwa kila mtu na kwa vyote vinavyoishi na ana mamlaka kwa vyote. **Zab 24:1**. Tuwarejelee Ibrahimu na Isaka.

D. Ibrahimu alimwamini Mungu.

- Fikiria linalotendeka hapa. Huu ni mshangao wa aina gani kwa Ibrahimu. Lazima alishangaa kuwa Mungu amebadili nia yake juu ya Isaka na ahadi zake .Je, ahadi za Mungu zingetimia vipi kupitia kwa Isaka kama Ibrahimu angemuuwa?
- Unajua, hata kama Ibrahimu aliambiwa na Mungu kumtoa Isaka kama sadaka, ndani ya moyo wake sidhani kama alikuwa na shauku kwa Mungu. Kwa nini? Kwa sababu alimwamini Mungu na kumtumainia.
- Alijua Mungu hawezi kumdanganya. Alijua Mungu hawezi kupeana ahadi kisha akabadili mawazo yake.
- Ni vigumu kufikiria jinsi anavyolitimiza Neno lake. Nia yetu mara nyingi huwa sawa lakini huwa hatufuatilii. Huwa tunajishughulisha sana au tunachoka au tunakosa mwelekeo na tunashindwa kutekeleza lile aliloahidi. Mungu sio kama sisi. Ibrahimu aligundua lile ambalo kila mtu lampasa kuligundua. Mungu hawezi kushindwa kutekeleza lolote ambalo anaahidi. Tunaweza kumwamini Mungu kikamilifu. Hiki ndicho Mungu anahitaji zaidi, sisi kumwamini. **Waeb 11:6**
- **Waeb 11:17-19** – Ibrahimu aliamini kuwa hata kama Mungu angemuuwa Isaka, angemfufua tena kutoka wafu. Alijua haiwezekani kwa mwanadamu lakini kwa Mungu inawezekana.
- Ibrahimu alikuwa tofauti na Adamu na Hawa. Hao hawakuliamini neno la Mungu wala kulitii lakini, Ibrahimu aliamini kuwa Mungu angelitimiza Neno lake. Je, na wewe na mimi? Je, tunamwamini Mungu na Neno lake? Je, twaweza kumtumainia katika maisha yetu? **War 12:1.** Nataka kusema hivi: kwa viwango ambavyo hatumjui Mungu tutavitumainia vitu vingine kama pesa, watu, kazi, nk
- **Mwanzo 22:3-5 –** Ni nini unachokiona hapa ambacho kinaonyesha kuwa Ibrahimu alimwamini Mungu, angemuuwa Isaka au kumfufua kutoka wafu? **Ms 5**

E. Isaka aliuliza swali na Ibrahimu akalijibu.

- **Mwanzo 22:6-7** – tazama hali ya Isaka, bila shaka alikuwa ameona sadaka nyingi. Hapa hakuelewa ni kwa nini hawakuwa na kondoo wa kumtoa kama sadaka. Je, unafikiri kuwa Ibrahimu alikuwa amemwambia Isaka kile Mungu alikuwa amesema? Je, wewe unafikiria nini?
- **Mwanzo 22:8 –** Ibrahimu alikuwa na imani kamilifu na alimtumainia Mungu. Nataka kusema hili nijirudie jinsi niwezavyo…kumwamini Mungu ndilo jambo la muhimu zaidi kwa mwanadamu kutekeleza. **Waeb 4:2**
- Kama tutaugua na twende kwa daktari atuelezee dawa, Je, itatufaidi kama atatueleza kuihusu na jinsi inavyoweza kutuponya? kumsikiliza akitueleza jinsi inavyoweza kutuponya, dawa haiwezi kutuponya. Vivyo hivyo, kulisikiliza tu neno la Mungu haliwezi kutuzaidia. Ni lazima

tuliamini. Kama tutaliamini tutafanya yote ya imani. **Yakobo 2:18 –** Nitawaonyesha imani yangu katika matendo.

F. Ibrahimu alimfunga Isaka.

- **Mwanzo 22:9-10 –** Isaka hakuwa na njia ya kukwepa. Alifungwa na kulazwa madhabahuni. Ibrahimu aliinua kisu kumuuwa.
- Ilikuwa sawasawa na jinsi Mungu alivyofunga mlango wa safina wakati wa Nuhu baada ya Nuhu kuingia. Familia yake, wanyama na ndege walikuwa salama ndani, lakini hapakuwa na pakutorokea kwa wale waliobaki nje. Wale ambao hawakumwamini Mungu walifungiwa nje.
- Na hapakuwepo pa kutorokea kwa watu waovu wa miji ya Sodoma na Gomora wakati Mungu alileta moto juu yao. Hapakuwa na pakutorokea kwa mkewe Lutu wakati alikataa kumwamini Mungu na kutazama nyuma.
- Mungu alimwokoa Nuhu na jamii yake kutokana na gharika. Mungu aliwaokoa Lutu na jamii yake kutokana na moto ulioteketeza Sodoma na Gomora. Ni Mungu pekee angemwokoa Isaka.
- Unajua ni sawa sawa nasi leo hii. Hakuna vile tunaweza kujiokoa kutoka kwa mauti na hukumu ya milele kwa sababu ya dhambi yetu. Isipokuwa Mungu na Mungu pekee anayeweza kututengenezea njia.
- **Mwanzo 22:10-12 –** Ibrahimu alimwamini Mungu kikamilifu. Wakati aliinua kisu ilikumchinja mwanawe Mungu alimzuia kumchinja.

G. Mungu alipeana kondoo ya kiume badala ya Isaka.

- **Mwanzo 22:13 –** Mungu alisababisha kondoo wa kiume kupatikana, vipi? Kwa pembe zake akiwa amenaswa kichakani. Kama angenaswa na sehemu nyingine ya mwili, angejeruhiwa akitaka kujinasua. Kama angepata jeraha hangefaa tena kuwa kama dhabihu ya Mungu. **Kutoka 12:5 ; Walawi 22:19-22**. Mungu angekubali tu mnyama mwenye afya nzuri kama dhabihu. Kwa nini? Kwa sababu Mungu ni mkamilifu, na anakubali tu vitu vikamilifu pekee.Mungu alipeana sadaka inayokubalika kikamilifu badala ya Isaka.
- Unajua Mungu ni mwaminifu, alitimiza ahadi yake kwa Ibrahimu vile aliahidi. Sasa kupitia kwa Isaka Mungu angempa Ibrahimu kizazi kingi. Ibrahimu alimwondoa Isaka madhabahuni na akamweka kondoo ambaye Mungu alimpa. Kondoo alikufa badala ya Isaka, kondoo wa kiume alikuwa kibadala cha Isaka, Mungu alimwokoa Isaka kwa kupeana kondoo afe badala yake.

H. Ibrahimu alimtumainia Mungu kuleta mkombozi.

- **Mwanzo 22:14-19 –** Ibrahimu alimtumainia Mungu na Mungu akapeana kondoo wa kiume akafa kwa niaba ya Isaka. Ibrahimu aliamini pia kuwa Mungu siku moja angemlete mkombozi kuwaokoa wanadamu kutoka kwa utawala wa Shetani na hukumu ya dhambi. **Wagalatia 3:6-9.**

SOMO LA 9

Wana wa Isaka, Yakobo na Esau – Mwanzo 25:19 – 29:1

Mwana wa Yakobo, Yusufu – Mwanzo 37:1 – 46:7

Wana wa Isaka, yakobo na Esau.

A. Utangulizi.

- **Mwanzo 25:19,20** – miaka karibu **20** ilikuwa imepita hivi sasa tangu wakati Isaka alikuwa madhabahuni.

B. Isaka alimwoa Rebeka na kwao Esau na Yakobo wakazaliwa.

- **Mwanzo 25:21, 24-26 –** Ni kwa Muda upi Isaka na Rebeka walikuwa wamemaliza katika ndoa? Miaka 20.

C. Esau hakuamini wala kudhamini ahadi za Mungu.

- **Mwanzo 25:27a** – Esau aliishi maisha yake kama msasi mwituni. Ilikuwa wazi kuwa Mkombozi angezaliwa kupitia uzao wake, ni kwa sababu alikuwa mzaliwa wa kwanza wa Isaka. Haki ya kurithi ilipeanwa kwa mzaliwa wa kwanza kama kiongozi wa familia. Kwa hivyo mkombozi kutoka kwa Mungu ilikuwa wazi kuwa angezaliwa kupitia uzao wa Esau. Lakini Esau hakuwa na haja na ahadi ya Mungu. Hakumwamini Mungu kama vile Isaka na Ibrahimu walikuwa. Esau alikuwa kama Kaini. **Waebrania 12:16 –** Tunaposoma kumuhusu Esau tutagundua ya kuwa alikuwa anaishi maisha yake kwa kujihusisha na mambo ya dunia sana. Mambo ya dunia yalionekana ya muhimu sana kwake kuliko Mungu. **Mwanzo 25:28-34**
- **Warumi 9:13** Kwa nini Mungu akamchukia Esau? Ni kwa sababu hakujali wala kudhamini nafasi aliyopewa na Mungu kama mzaliwa wa kwanza. Nia yake ilikuwa hivi – Ya nini kuhitaji haki ya mzaliwa wa kwanza kunirejesha kwa kumtegemea Mungu. Mimi niko huru na mkamilifu. Mungu hatatenda chochote kwa mtu asijikubali kuwa yeye ni mtenda dhambi na anahitaji Mungu. Esau alikataa neema ya Mungu, alidharau nafasi yake kama mzaliwa wa kwanza, hakuwa tubu na hivyo Mungu hakuwahi msamehe. Hii ndio nia ya msingi ya dhambi ni kuwa inamfanya Mungu kukosa udhamana. Mungu hawezi msaidia mtu aliye na mawazo kama yale ya Esau.
- Esau alikuwa na mjukuu aliyeitwa Amaleki na Malaki anatueleza kuwa uzao wa Esau ulikuwa uzao uliolaumiwa kila mara na Mungu. **Malaki 1:4**
- Pia katika **Kutoka 17:16 –** Mbona? Kwa sababu kuishi kati ya waameleki ilikuwa ni dhambi ya Esau mwana aliyekataa haki yake ya kuzaliwa.
- Katika **Samweli wa kwanza 15:3 –** tunaona hili tena. Walakini, katika msitari wa **7 – 9** Sauli alimsamehe mfalme Agagi.
- Ni la kushangaza kuwa, Hamani katika kitabu cha Esta alikuwa kutoka uzao wa Agagi. **Esta 3:1 –** tazama ni mara ngapi Hamani amerejelewa kama, “adui wa wayahudi” **Esta 3:10- ; 9:10; na 9:24.**

- Na Kama tungefuatilia uzao wake hadi agano jipya, Herodi aliyetaka kumuuwa Yesu na kuamuru uharipivu kwa watoto chini ya miaka mbili katika muji wa Bethlehemu, pia alikuwa muedomi (kutoka uzao wa Esau)**. Mathayo 2:16**

D. Yakobo alinawiri kwa kuziamini ahadi za mungu.

- **Mwanzo 25:27b –** Yakobo Kwa upande mwingine, akiwa kimya Kwa hema lake alikuwa akifuga kondoo na ng'ombe. Kinyume na Esau, Yakobo alikuwa mtu mwenye imani Kama tu Isaka na Ibrahimu.
- Wajua kila mmoja wetu anatakiwa kujiuliza,"Je, nageuka kutoka Kwa Mungu na kwenenda njia nzangu kama Esau na Kaini? Ama mimi ni kama Habili,Enoko, Nuhu,Ibrahimu, Isaka na Yakobo, nikikubali kuwa mimi ni mwenye dhambi na kuzitumainia njia za Mungu, Nakumtumainia yeye kuleta mkombozi, kuliko kujifanyia njia zangu mwenyewe…?"
- Kwa sababu ya utofauti huu mkubwa kati ya Esau na Yakobo, chuki ilizidi kuenea na hata kufikia kiwango ambapo Esau alitishia kumtoa Yakobo uhai.

E. Yakobo alirejea katika mji wa Isaka na Rebeka.

- Kwa hivyo Yakobo akaondoka katika makazi ya wazazi wake na kuanza safari ndefu kurejea Masopatania, nchi ambayo babu yake Ibrahimu alitoka. **Mwanzo 28:10 –** ilikuwa safari ndeefu kutoka Kanani hadi Masopotania, na basi ikampasa Yakobo kulala milimani.

F. Ndoto ya Yakobo.

- **Mwanzo 28:11 –** usiku baada ya nyingine Yakobo alilala hivyo…lakini sasa usiku mmoja alipolala Mungu alimpa ndoto.
- Kabla ya biblia kuandikwa Mungu mara nyingi sana aliwanenea watu kupitia ndoto, lakini kwa kuwa leo hii biblia imekamilika hutunenea kupitia neno lake.
- **MwanZo 28:12 – Kupitia** ndoto hii Mungu alikuwa ikimfahamisha kuwa mkombozi anayekuja atakuwa daraja kati ya mwanadamu na Mungu.
- Ni Mungu pekee anayeweza kutengeneza njia kwetu sisi kumfikia. Kumbuka watu kwa mnara wa Babeli, Kazi yao nzuri haingeweza kuunda daraja ya kupitia ili kwamba wakamfikie Mungu kwa sababu ya pengo kati yetu na Mungu lililosababishwa na dhambi ya mwanadamu.
- Sasa vikiria hapo mwanzoni basi, Adamu na na Hawa walikuwa katika ushirika, na Mungu. Wakitembea pamoja,Walikuwa marafiki wa Mungu , Lakini walipokosa kumutii, pamoja na kizazi chao chote ikiwemo wewe na mimi tulitengwa naye Mungu.Ngazi iliyotuunganisha sisi na yeye ilitolewa na sasa hatukukuwa na njia ya kurudi tena na kukuwa na ushirika na yeye, basi pasipo yeye kutengeneza njia hakuna mwanadamu kujiokoa.
- Lakini Mungu aliahidi mkombozi atakaye haribu kazi ya Shetani na kumupatanisha mwanadamu na Mungu.Mkombozi atakuwa kama ngazi aliyoonyeshwa Yakobo ikitoka ulimwenguni hadi mbinguni.
  Yoh 1:51
- Hata kama watu wote wametengwa na Mungu kutokana na uongo wa Ebilisi na kutoamini kwa Adamu kutoamini na kutotii, Mungu angali na mpango wa kumtuma mkombozi atakaye wesesha mwanadamu kurejeshwa kwa Mungu na kuwa wamoja.
- Wajua kuwa Yakobo alikuwa mwenye dhambi, Kama sisi tulivyo, na kama tungekuwa na wakati wa kuyatadhimini maisha yake, tungeliona hili. Lakini Mungu Kwa neema alimwonyesha kuwa kuna njia moja tu nayo ni hii, na Yakobo amtumainia Mungu kwa kila jambo bali asienenda kwa uweza wake wa kukabiliana na hali.

G. Ahadi ambazo Mungu aliahiti Ibrahimu na Isaka zilipeanwa kwa Yakobo.

- **Mwanzo 28:13 -15** – Mungu alikuwa anaendelea na mpango wake wa kumtuma mkombozi.

- Miaka mingi ilikuwa imepita tangu Mungu kupeana ahadi yake ya kwanza ya kumutuma mkombozi katika bustani ya Edeni. Ibrahimu yule ambaye Mungu alikuwa amemchagua kuwa Baba mtangulizi wa mkombozi, alikuwa amekwisha kufaa. Mungu hakukuwa amesahau mpango yake, ama Neno Lake. **Zaburi 119:89.**
- Kurejea tena katika **mwanzo 28:14** – Mungu alimuahidi Yakobo kuwa mkombozi takuwa kutoka uzao wake.Yakobo sasa alikuwa na uhakika kuwa ahadi silizopeanwa kwa babu yake Ibrahimu na baba yake Isaka sasa ni zake.
- **Mwanzo 29:1** – kwa hivyo Yakobo alirejea tena Haruni, ameoa, na alikuwa na watoto kumi na mbili na Mungu akamupatilisha jina lake likawa Israeli. **Mwanzo 32:28**

Yusufu, Mwana wa Yakobo.

A.Yusufu, mtoto mpendwa wa Yakobo.

- Hebu tukatazame Mwanzo 37 na mutasomu wetu umwelekee Yusufu, Mwana wa Yakobo. **Mwanzo 37:1-3**

B. Nduguze Yusufu wakubwa walimchukia.

- **Mwanzo 37:4 - Kwa** kuwa Yusufu alikuwa mpenzi wa babaye, ndugu zake wote walimchukia.

C. Ndoto ya Yusufu.

- **Mwanzo 37:5-11** - Mungu alijua kihalisi kilichokuwa kitandeka kwa jamii ya Yusufu.Yusufu hangeona maisha yake ya mbeleni, wala hata kujua jinsi ndoto yake ingetimia, Lakini Mungu alijua vyema kuwa Yusufu angekuwa kiongozi juu ya jamii yake.

D. Yusufu aliuzwa utumwani.

- **Mwanzo 37:12 – 14, 18-20,24 28; 39:1** – Yusufu yule ambaye Mungu alisema kuwa atakuwa kiongozi tazama yu matekani katika nchi ya utumwa Misri.
- Kuna vifungu kadhaa za kufurahisha za kuangalia – **Yohana 12:24; Mathayo 20:26-28**. Wajua Mungu lazima atimize kila ahadi anayoahidi. Anajua kila kitu, hakuna chochote kinacho tendeka pila ufahamu wake ama kwa mushangao.

E. Yusufu anafungwa gerezani.

- **Mwanzo 39:1-20 –** Tunapoangalia katika vifungu hivi, kwa muda mchache mambo yalimwendea vizuri sana Yusufu katika mahali pake pa kazi.Mwajiri wake alibarikiwa na Yusufu naye akainuliwa. **Na 1 wakorintho 16:9** – Bila shaka hebu tutazame mbele katika **Mwanzo 50:20.**
- Ni la kushangaza kuwa hata Kama Yusufu alichukiwa na nduguze na kupangiwa uongo na mke wa Bwana wake, alizidi kumtumainia Mungu. Alimtumainia Mungu Kama tu Ibrahimu, Yakobo na Isaka. Wajua hakuna yeyote anayeweza kumpendeza Mungu pasipo kuamini kile anachonena. **Waebrania 11:6** – Jambo kubwa zaidi ni kulikubali Neno la Mungu kuwa kweli na kumtumainia kwamba kile kilichoandikwa ni kweli.
- Tumrejelee tena Yusufu. Sasa Yusufu akawekwa gerezani lakini bado Mungu hakumuacha humo gerezani. **Mwanzo 39:21-23 –** Je, Yusufu alistahili kibali cha Mungu… La hasha, alikuwa mtenda dhambi. Lakini Mungu alimlinda. Ni kwa sababu yeye ni mwenye rehema…**Yakobo 2:13; Maombolezo 3:22, 23; Yeremia 29:11.** Mungu alikuwa na mpango wa ajabu kwa maisha ya Yusufu.

F. Ndoto ya Farao.

- **Mwanzo 41:1-8 –** Farao mfalme wa Misri, hakumtambua wala hata kumwabudu Mungu wa Israeli. Wamisri waliabudu mwezi, Nyota, Jua, Wanyama, Viumbe teule na mto Nile. Lakini hata kama hawakumwabudu Mungu wa kweli, Mungu alimtumia mfalme wao na taifa hili ili kutimiza ahadi zake.
- **Mithali 21:1 –** Mungu wetu ni mfalme juu ya nchi zote na wafalme wote hata kama kuna uwezekano wa wao kutomwabudu wala kumjua. Kwa kuwa yeye ni mpeanaji wa uzima. Kwa hivyo ni haki yetu sisi kuitwa wanawe. **Zaburi 24:1**
- Hapa kuna Mwanzo 41 tunamwona Mungu akitekeleza kazi yake kupitia huyu mmisri na asiyeamini na mfungwa wa misri kuwaokoa watu wote.
- Nlikuwa nikifiria siku ambayo Yusufu alikuwa akimtumainia Mungu kikamilifu akiwa humo gerezani. Hatumwoni akijaribu kujitetea wala kujaribu kutoka katika hali hii. Hakujua wakati ule ni kwa jinsi gani mungu atamwokoa toka hali hiyo lakini alizidi kumtumainia Mungu na kuamini kuwa Mungu angetenda lile lililojema kwake.

G. Yusufu alitafusiri ndoto ya Farao.

- **Mwanzo 41:14-16** – Ni nini mawazo yako katika kistari hii? Unyenyekevu na Imani ya Yusufu. Ni kwa Mungu twapeana utukufu.
- **Mwanzo 41:25-32 –** Mungu alimpa Yusufu ufahamu mkuu wa kushiriki na Farao na kilea ambacho kingetendeka katika taifa hilo.

H. Yusufu alipewa cheo kilichofuatia kile cha Farao.

- **Mwanzo 41:33-43 -** Neno la Mungu ni la kweli **– Zab 75:6 –**
- Kumbuka ndoto ya Yusufu aliyopewa na Mungu akiwa kijana? Ilikuwa karibu kutimia.**Mwanzo 37:7 –** Ndugu zake na jamii wakimsujudia.
- Mungu kila mara hutenda kulingana na ahadi zake. Hakuna anayeweza kumpinga.Wakati wake wa kutekeleza ahadi zake ulipowadia, alimtoa Yusufu gerezani na akampa nafasi kubwa sana gerezani, kama mtu alivyomwonyesha akiwa bado kijana. **Danieli 4:56-57**

I. Nduguze Yusufu walikuja Misri kutafuta chakula.

- **Mwanzo 42:1-3, 6-8 –** Ndugu zake walinunua chakula kadhaa na kuanza safari kurejea nyumbani.

J. Yusufu anajitambulisha.

- **Mwanzo 43:1, 2** – wanarejea mara tena kumwona Yusufu.
  Mwanzo 45:1-9 – tazama mstari wa kwanza na wapili, Yusufu alilia wakati alijitambulisha kwa ndugu zake. Badala ya kuwafanyia kile ambacho walistahili
  Mwanzo 50:20; Warumi 8:28.

K. Israeli alienda Misri.

- **Mwanzo 45:25-28; 46:5-7** – wajua kuwa Mungu kila mara hutimiza ahadi zake. Ni miaka mingi sana tangu kumweleza Ibrahimu kwamba uzao wake utakwenda utumwani. **Mwanzo 15:13 –** hata kama ma mia za miaka ilikuwa imepita tangu ahadi hii ya Mungu kutimizwa. Kila anachosema katika neno lake hutendeka jinsi anenavyo.

SOMO LA 10

Mungu alihifadhi Israeli wakiwa Misri. – Ktk 1:6-11

Mungu alimchagua, akamhifadhi na kumwita Musa kukomboa Israeli. – Mwanzo 1:11- 4:31

Mungu alihifadhi Israeli kule Misri.

A. utangulizi.

- Tumemalizia kitabu cha Mwanzo na maisha ya Yusufu. Tunaelekea katika kitabu cha Kutoka, kitabu cha pili cha Biblia. Neno kutoka lamaanisha ”kuondoka.” Hiki kitabu kimerekodi jinsi Mungu aliwatoa watu wake wana wa Israeli kutoka nchi ya Misri. Tunaposoma hii historia ya kushangaza hebu tutilie maanani haya mambo:
- Kwanza kumbuka kuwa Biblia ni historia ya kweli. Mambo ya Mwanzo na Kutoka yanatajwa mara mingi katika Biblia nzima na habari hii yote imedhibitishwa na wasomi stadi wa Biblia.
- Pili hebu tutazame kile Mungu anafanya. Tutasoma kitu kikuu sana kumhusu Mungu katika kitabu hiki. Kama tu matendo yetu yanaeleza tabia zetu pia matendo ya Mungu huonyesha tabia zake.
- Tatu kumbuka ya kuwa Mungu yule aliyekuwepo wakati wa historia hii ni yule yule hadi leo hii. Habadiliki kamwe. Mungu bado ni mtakatifu, mwenye uweza, anajua vyote, mwaminifu na mkuu.
- Tuliwachana na Yakobo na wanawe 11 na jamii zao wakija Misri kuishi kwa sababu ya baa la njaa. Kwa wakati huo Yakobo Israeli alipokufa, lakini Yusufu, nduguze na jamii zao wakazalia kule Misri na jamii zao hata ingawa njaa ilikuwa imeisha. Hawakurejea tena katika nchi yao, walioahidiwa na Mungu kwa Ibrahimu, Isaka na Yakobo. Baadaye Yusufu na kizazi hicho chote kilikufia kule Misri.
- Takribani miaka 350 ilikuwa imepita kati ya wakati Israeli alienda kuishi Misri, na wakati ambapo historia ya kitabu cha Kutoka inaanzia. Waisraeli wamekuwa wakiishi Misri kwa wakati huo wote.

B. Waisraeli waliendelea kutajirika na kuongezeka kwa idadi.

- **Kutoka 1:6-7** – wana wa Israeli walinawiri kule Misri. Waliongezeka kwa idadi. Pia walimiliki mali mingi. Walikuwa na ng’ombe wengi, kondoo na mbuzi.
- Kulikuweko vyakula vya kutosha vya kulisha wanyama wao. Mfalme pia alikuwa mwema kwao lakini mambo yalikuwa karibu kubadilisha mkondo.

C. Mpango muovu wa mfalme mpya.

- **Kutoka 1:8-11** – Ni nani aliyekuwa akimwongoza Farao kwa mpango huu muovu? Shetani! Kumbuka, anamchukia Mungu tena anamchukia mwanadamu.
- Shetani alijua ya kuwa Mungu alikuwa ameahidi kutuma mkombozi ambaye angemwangamiza yeye na kumkomboa mwanadamu kutoka kwenye utawala wake. Tena alijua kuwa Mungu alikuwa ameahidi ya kuwa huyu mkombozi angezaliwa kwenye taifa la Israeli**. Mwanzo 12:2,3; 28:14,15.** Shetani alijua ya kuwa mkombozi huyo atakuwa wa kizazi cha Ibrahimu, kwa hivyo alitaka kuangamiza taifa la Israeli kwa sababu walikuwa ni watu ambao Mungu alikuwa amechagua kutimiza mpango wake katika ulimwengu.

Mungu alimchagua akamhifadhi na kumwita Musa kuikomboa Israeli.

A. kuzaliwa kwa Musa na mpango wa mamaye.

- **Kutoka 1:11-22; 2:1-4** – Unajua mahali pa mwisho nitakapo mficha mwanangu ni pale kwenye mto ambamo Farao anawazamisha watoto, lakini wazazi wa mtoto huyu walimtumainia Mungu kabisa kumlinda mwanao.

B. Musa anachukuliwa na bintiye Farao

- **Kutoka 2:5-10; Waefeso 3:20 –** Mungu anaweza. Hebu tafakari hili; 1) mto ule ule uliokusudiwa kumwangamiza mtoto huyu unatumika kumwokoa. 2) mama ambaye mtoto huyu anachukuliwa kwake amerejeshewa kisha amelipwa kumlinda mtoto wake mwenyewe. 3) yule anaye jaribu kumuua Musa ndiye anayemlea tena anamuelimisha ili siku moja afanye kitendo kile kile anachojaribu kuzuia kwa kuwazamisha watoto. **1 Wakorinntho 1:19,20; 3:19**
- Mungu alikuwa na mpango kumtumia mtoto huyu Musa kuwaokoa watu wake lakini lazima amwandae kwa kazi hiyo. Alijua kwamba Musa angesoma mambo mengi katika nyumba ya Farao ambayo yangekuwa ya muhimu kwake kujua katika kazi yake ya usoni kama kiongozi ya watu wake. **Matendo 7:22 –**
- Historia ya Misri ya wakati huu inataja kwamba watoto wa viongozi wa Misri walipewa maelezo muhimu ya kusoma na kuandika pamoja na mafundisho ya kazi ya kinyumbani na ya uongozi wa kivita. Yawezekana kuwa Musa alipewa mafunzo hayo alipokuwa akilelewa katika nyumba ya Farao.
- Kama vile tu hadithi ya Yusufu, hapa tena tunamwona Mungu akitenda kazi katika hali ngumu kutimiza kusudi lake kwa watu wake.
- Mungu ni mkubwa kuliko kila mtu na kila kitu. Ni mkubwa kuliko shetani. Hakuna chochote wala yeyote anayeweza kumzuia kutenda anachopanga.

C. Musa alipobalehe.

- **Ktk 2:11-15** – Waisraeli walichukuliwa mateka na Farao mwovu na hawangeweza kutoroka. Musa alifanya yote aliyoweza kuwasaidia lakini hakufaulu. Hakuna mwanadamu angeweza kuwanusuru watu hawa. Ni Mungu pekee angeweza kuwaokoa.
- Wajua, jinsi tu Waisraeli walivyotekwa nyara na Farao ndivyo pia mababu zetu watoto wetu wote na sisi tumezaliwa katika utumwa na kushikwa mateka na Shetani. Hatuwezi kujikomboa sisi wenyewe kutoka kwenye utumwa huu . Hakuna mwalimu wala mhubiri anaweza kutukomboa; hakuna mwanadamu yeyote anayeweza kutukomboa. Mungu pekee anaweza kutukomboa kutoka kwenye minyororo ya Shetani.

D. Musa na msitu unaochomeka.

- **Kutoka 3:1-3** – Msitu huu ulikuwa ni wa kawaida tu; kitu cha ajabu, ni kwamba msitu huo ulikuwa unawake lakini haukuwa unachomeka…kwa nini? Kwa sababu, Mungu alikuwa kwenye huo msitu. Mungu ni mkuu. Hakuna anayeweza kufanya yale ambayo Mungu anaweza kuyafanya. Jinsi tu Mungu alivyokuwa kwenye huo msitu, na akauzuia kuchomeka, hivyo pia alikuwa pamoja na Waisraeli na kuwahifadhi kutoka kwa maangamizi. Shetani na Farao hawangeweza kuwaangamiza Waisraeli wakati Mungu alikuwa pamoja nao.

E. Mungu alipeana ujumbe wake kwa Musa.

- **Kutoka 3:4** – Wajua kuwa Musa alisimama tu kuona maajabu haya. Hakujua ya kwamba Mungu alikuwa humo motoni. Waweza fikiria ni kwa jinsi gani alistaajabu kwa kusikia sauti ikitoka kwenye msitu.
- **Ktk3:5,6** – Mungu alimwamuru Musa kutoa viatu vyake. Kwa nini? Kuwa mguu tupu ilikuwa ishara ya unyenyekefu na utiifu. Watumwa walikuwa wakitembea chini bila vyatu.

- Wajua kuwa Mungu huchagua yeyote anayependa kumwakilisha, na wakati wa Mungu wa kutekeleza ahadi zake ukiwadia hakuna yeyote awezaye kumpinga.
- **Ktk 3:7-10.** Mungu alimweleza Musa kuwa amemchagua yeye kuwaokoa Waisraeli toka Misri hadi nchi aliyowaahidi Ibrahimu na baba zake. Inanishangaza ninaposoma Biblia na kuona watu ambao Mungu anatumia kama vile Paulo, wanafunzi wa Yesu, Amosi…na hapa anataka kumtuimia Musa… mzee wa miaka 80 ambaye hakutaka kazi hiyo.
- Kumbuka ya kwamba kuna wakati ambapo Musa alishindwa kuwasaidia watu wake na hivyo hakuwa na uhiari wa kujaribu tena.
- **Ktk 3:11 –** Musa anaanza na moja wapo ya malalamishi yake tano, lalama ya kwanza; Musa alikosa ukakamafu (mimi siwezi).
- Jibu la Mungu **– Ktk 3:12.**

F. MIMI NDIMI.

- Lalama ya pili – **Ktk 3:13 –**
- **Ktk 3:14 –** Eleza – wakati wa uandishi wa Biblia majina yalikuwa na umuhimu mkubwa sana. Jina la mtu lilisisitiza tabia fulani. Kwa mfano jina Musa lilimaanisha **"chota kutoka."** Hii ni kwa sababu alitolewa kwa maji wakati bintiye Farao alimkuta. Lakini Mungu hangejipea mwenyewe jina moja tu au mbili. Haingewezekana kwa kuwa Mungu ni mkuu zaidi. Yeye ndiye mkuu zaidi, mwaminifu na Mungu asiyebadilika kamwe. Hakimu mkuu na mlipiza kisasi cha dhambi, wa upendo, mwenye haki na mwokozi wa neema ambaye pekee awezaye kupeana njia ya mwanadamu kuokolewa kutoka kwa shetani, dhambi na mauti. Yeye ni haya yote na hata mengi zaidi ya haya.
- Je, Mungu angesema jina gani moja ambalo Waisraeli wangemufahamu vyema? Haingewezekana kamwe. Na hivyo Mungu alimweleza Musa awaambie wana wa Israeli kuwa "**MIMI NDIMI**" amemtuma.
- Hili jina "**MIMI NDIMI"** lina maana nyingi ambazo sisi hatuwezi kuzifahamu kikamilifu. Inamaanisha kuwa Mungu ni yule alikuwepo bila kuumbwa. Je, wakumbuka maneno ya kwanza katika Biblia, "Hapo mwanzo, Mungu…"? Mungu hakuwa na mwanzo na hatakuwa na mwisho. Hakuwahi na hatawahi tegemea yeyote.
- Walakini, kila mtu humtegemea. Yuko na mamlaka juu ya nchi, mvua, jua, mwezi, nyota,upepo na mito. kila kitu ki chini yake. Yeye ndiye "**MIMI NDIMI**"aliye mkuu.
- Farao, Wamisri na hata shetani hawangeweza kushikilia watu wa Mungu wakati "**MIMI NDIMI**" mkuu aliamua kuwaokoa. **Ktk 3:15-18**

G. Mungu alijua kile ambacho mfalme angefanya.

- **Ktk 3:19 – 20 –** Fahamishwa kuwa Mungu alijua kikamilifu jinsi mfalme wa Misri angeitikia. Mungu hujua mawazo yetu, maneno na matendo hata kabla hatuchafikiria, kusema au kuyatenda. **Zaburi 139:1-4 –** Mungu anajua kila kitu kutuhusu tangia kuzaliwa hadi kufa na hata baada ya kifo.
- Baada ya haya yote, Musa bado alikuwa na shauku, kwa hivyo katika **Kutoka 4:1** - Anapeana lalama ya tatu**. Kutoka 4:2-5**
- **Kutoka 4:10 –** lalama ya nne **– Kutoka 4:11-12**

H. Mungu alimchagua Haruni kuwa msemaji wa Musa.

- Mungu hangekubali la kuwa jibu, kwa hivyo Musa alikuwa na wazo moja zaidi. **Kutoka 4:13 –** "kamtume mtu mwingine…mimi siko tayari"
- **Kutoka 4:14- 20; Kutoka 4:27-31.**

SOMO LA 11

Mungu alituma mapigo kwa Wamisri na kuwahebusha Waisraeli . –Ktk 5:1-12:36

Mungu aliwaokoa Waisraeli katika bahari ya Shamu na kuwalinda jangwani. – Kutoka 13:17-17:6

Mungu alituma mapigo kwa Wamisri na kuwahebusha Waisraeli .

A.Utangulizi.

- Tulimalizia na Mungu akiwatuma Musa na Haruni kule Misri. Leo hii tutaona jinsi Mungu aliwatuma Musa na Haruni Misri. Waisraeli walikuwa wameshikwa mateka na mfalme mwenye nguvu wa Misri ambaye ni Farao.
- Sasa hakuna mmoja wetu ambaye kimwili amekuwa utumwani lakini tumekuwa watumwa wa dhambi.

B.Farao alikataa kutii amri ya Mungu.

- **Kutoka 5:1, 2 –** Kumbuka ya kwamba Farao lilikuwa jina la cheo ya kila mfalme aliyeiongoza Misri wakati huo. Hatuambiwa ni Farao nambari ya ngapi aliyekuwa mamlakani wakati Musa alikuwa kiongozi. Lakini katika **mstari wa pili** tunagundua ya kwamba huyu mfalme hakumfahamu Mungu wa pekee aishiye.
- Tulivyojifahamisha hapo mwanzoni ni kwamba Wamisri hawakumwabudu Mungu wa kweli bali waliabudu viumbe alivyoviumba Mungu wa kweli.
- Waliabudu mto wa Nile ambao ndio mto mrefu katika nchi yao.
- Pia waliabudu mwezi, jua na viumbe vingine tofauti tofauti.
- Walikuwa na miungu wengi sana. Juu ya hiyo, pia walimwabudu Farao kama muungu.
- Kitu tunachostahili kufahamu kuwa Waisraeli waliokuwepo Misri wakati Musa alirejea kule hawakuwa wamewahi shuhudia utukufu wa Mungu.
- Walikuwa wamewahi kusikia tu Mungu aliyewatendea Ibrahimu, Isaka, Yakobo na Yusufu mambo makuu.
- Kwa hivyo Mungu aliamua kumtumia huyu mfalme mgumu kudhihirisha ukuu wake na kuwahakikishia Waisraeli kuwa yeye ni yule yule mkuu.

C .kupitia kwa kuasi kwa Farao, Mungu alikusudia kuwaonyesha Waisraeli na Wamisri kuwa yeye ndiye Mungu wa kweli na aishiye.

- **Kutoka 6:1-8** – Mungu pia alikuwa na mpango wa kudhibitisha kuwa, yeye ndiye Mungu pekee aishiye na yuko na mamlaka juu ya dunia nzima na kuwa miungu waliyoabudu Wamisri ilikuwa duni mbele ya Mungu wa Israeli.
- Kumbuka ya kuwa Wamisri walikuwa watu werevu na tajriba kuu: waandishi hodari, wanahisabati, wanakemia,vikozi wa kijeshi na viongozi, wachoraji hodari, wasanii, wajenzi, nk lakini kiroho, walikuwa vipovu na wafu. Hata kama waliwashika mateka Waisraeli katika nchi yao, Wamisri wenyewe ndio waliokuwa mateka na chini ya mwongozo wa Shetani.

D. Mungu akatuma mapigo tisa.

- Hebu tukaone sasa jinsi Mungu alitumia kiongozi huyu mwovu kuonyesha utukufu wake.

- **Kutoka 7:3-5** – Hii yafaa kuwa onyo kwetu sote.
- Hatuwezi mpuuza au kumuasi Mungu.
- Hakuna yeyote anayeweza kupigana na Mungu na akashinda wala kuepuka hukumu yake.
- **Ktk 7:10-14** – kwa sababu mfalme wa Misri alikataa kutii amri ya Mungu, Mungu aliamua kuonyesha utukufu wake.
- Kwa sababu ya wakati, hatutasoma kila kitu kilichotendeka. Lakini kama utapata muda wako**,** utapata ufahamu katika kitabu cha **Kutoka 7:14- 10:29**
- Jambo la kwanza Mungu alibadili maji ya mto wao yakawa damu.
- Pili alituma mapigo ya viura**,** chawa na nzi.
- Kisha Mungu akasababisha mifugo wa Wamisri kuwa wagonjwa.
- Kisha Mungu akasababisha Wamisri wote kuwa na majipu.
- Hii ilifuatiwa na moshi mbaya ya maangamizi, pigo la nzige na kisha siku tatu za kiza totoro kila mahali ambapo Wamisri walikuwa wakiishi.
- Farao na Wamisri hawangeweza kujiokoa kutoka na mapigo haya yaliyotumwa na Bwana. Hata miungu yao ya uongo haingeweza kuwaokoa.
- Makinika hapa; Kila pigo ilikuwa ukiashiria muungu fulani wa Wamisri: kwa mfano; muungu wao wa viura, muungu wao wa jua, na muungu wao wa moshi mkali. Kitu kimoja cha kushangaza ambacho ningependa kukufahamisha ni kuwa Mungu aliwalinda Waisraeli kutokana na mambo haya hata kama wallikuwa wakiishi katika nchi moja. **Kutoka 9:4-6; 9:25-26 nk.**
- Je, Mungu aliwalinda Waisraeli kwa kuwa walikuwa wakamilifu bila dhambi? La hasha! Aliwalinda kwa sababu ya upendo na neema yake kuu. Na pia ni kwa sababu ya ahadi yake kwa brahimu kuwa atafanya uzao wa Ibrahimu taifa kuu na akaahidi kuwa atakuwa Mungu wao.
- Hata kama mamia za miaka zilikuwa zimepita, na sasa Waisraeli walikuwa matekani Misri, Mungu bado aliwadhamini Waisraeli kama watu spesheli na ambao ni kizazi cha Ibrahimu alichomuahidi.
- Pia sababu ya kawaida ambayo alijaribu kudokeza kwa kuwalinda Waisraeli ilikuwa, Farao na Wamisri wajue ya kwamba ni Mungu wa Israeli ndiye Mungu wa kweli na anayeishi.
- Rejelea tena mapigo ya Mungu, kila pigo lilikuwa na mtindo wa mwitikio wake uliokuwa sawa. Kila wakati Bwana alipolituma pigo, Farao alimwita Musa na kumwambia awaondolea akidai kuwa atawaruhusu Waisraeli waondoke.
- Kila mara Farao aliposema kuwa atawaweka huru, Bwana aliliondoa pigo .
- Lakini punde tu alipoondoa, moyo wa Farao uligeuka kuwa mgumu na kukataa kuwaachilia waende. **Kutoka 9:23-35**
- Mungu alijua wazi kuwa Farao atakuwa mgumu.
- Hata kabla ya kumtuma Musa kurejea Misri, Mungu alimweleza kuwa haya yatatendeka.
- Mungu hashangashwi na kile mwanadamu anatenda.
- Kila mara anajua kabla ya kitu kutendeka. Na yuko na mpango wake tayari wa kusuluhisha haijalishi kile mtu atatenda ama kusema.
- Huyu mfalme mwovu hangetenda chochote kumzuia Mungu kutenda kazi yake ya kuwakomboa Waisraeli. Bwana alijua kuwa baada ya pigo la mwisho, Farao angewaruhusu Waisraeli kuondoka.

E. Hukumu ya mwisho ya Bwana kwa Wamisri.

- **Ktk 11:1,4-7 –** Kumbuka ya kwamba Waisraeli pia walikuwa wenye dhambi na walistahili hukumu ya kifo, lakini kwa sababu ya neema ya Mungu walisamehewa kutoka kwa mapigo.
- Na kwa hivyo Mungu alipeana maagizo ambayo Waisraeli walistahili kufanya ili kwamba kuwaokoa wazaliwa wao wa kwanza.
- **Ktk 12:1-5 –** mwanakondoo ama mbuzi alistahili awe bila mawaa(mkamilifu).
- Je, wakumbuka mwanakondoo aliyetolewa kafara badala ya Isaka? Alichukuliwa kwa pembe kutoka kwenye msitu wa miiba. Mbona alichukuliwa hivyo? Mungu ni mkamilifu na kila kitu anachotenda ni kikamilifu. Kwa hivyo hangekubali mnyama yeyote anayetolewa kama kafara aliye mgonjwa ama majeraha.
- **Ktk 12:6 –** mwanakondoo alipaswa kuwekwa hadi siku halisi iliyochaguliwa na Bwana, na hiyo ilikuwa siku ya kumi na nne ya mwezi, na iliwapasa kumuua mwanakondoo yule jioni ya hiyo siku.

- Waisraeli walipoua wanakondoo na damu kutiririka, watu walikuwa wakikumbushwa kuwa hukumu ya dhambi ni mauti. Kama tu kondoo alivyouawa kwa ajili ya Isaka, kondoo wakamilifu waliochaguliwa na kuuawa na Waisraeli, walikufa kwa ajili ya wazaliwa wa kwanza wa Israeli.
- **Ktk 12:7 –** Tanbihi**:** ilikuwa damu ya kondoo kuwaokoa wazaliwa wa kwanza. **Kutoka 12:22,23**
- **Ktk 12:46** – Ni la muhimu kukumbuka hili: Hawakustahili kuuvunja mfupa wa kondoo.
- Haya yalikuwa maagizo ya Mungu kwa Waisraeli.
- Walistahili kufanya kila kitu kama vile Bwana alivyoamwambia Musa.
- Mungu kila mara amezalia jinsi alivyo. Hatawahi ruhusu yeyote kutumia mbinu yake mwenyewe kujiokoa. Wakumbuka akikataa mavazi waliyojiundia Adamu na Hawa katika bustani la Edeni? Mungu pia alikataa sadaka ya Kaini ni kwa sababu haikutolewa kulingana na maagizo yake Mungu. Mungu alimwelezea Nuhu kutengeneza safina kama tu alivyotaka. Vivyo hivyo Waisraeli walitakiwa kutenda kulingana na amri zake alizopeana kwa Musa.
- Mungu bado ni yule yule . Hajabadilika. Hatuwezi mjia Mungu kwa mawazo yetu. Twaweza tu kuja kwa njia yake mwenyewe.

F. Ahadi ya Bwana kwa Waisraeli.

- **Ktk 12:12-14 –** Ungehisi vipi kama haya yangekuwa yanaenda kutendeka kwako? Waweza sasa fikiria uoga uliowaingia wana Waisraeli. Walijua Mungu alimaanisha kile amesema na waliamini na kutii.

G. Imani ya Waisraeli na utiifu wao.

- **Ktk 12:28 –** je, wafikiri ni nini kingetendeka kama Muisraeli angesema," siwezi kumuua mmoja wa kondoo wangu mzuri. Niko na yule mgonjwa, ambaye anaweza tekeleza wajibu huu." Je, wadhani kuwa Mungu angekubali damu ya mwana kondoo mwenye ugonjwa? LA HASHA!
- Fikiria kuhusu hii: Mwanakondoo alistahili kuwa mkamilifu. Ilikuwa afe. Ilikuwa lazima damu imwagwe. Kwa nini? Wasije wakasahau kuwa hukumu ya dhambi ni mauti.

H. Wazaliwa wote wa kwanza wa Misri walikufa.

- **Ktk 12:29,30** – Kila mzaliwa wa kwanza wa Mumisri na wanyama wa kwanza wa mifugo wa Wamisri walikufa.
- Kumbuka ya kuwa hukumu ya dhambi ni mauti. **Warumi 6:23**
- Mungu kila mara hutekeleza kile anachosema.
- Alisema kuwa atawateketeza wazaliwa wa kwanza wa Wamisri na vivyo ndivyo alivyotenda.
- Alisema kuwa ataupita kila mlango atakao ona damu juu yake na akafanya hivyo.
- Nataka kusisitiza hii mara tena jinsi niwezavyo – Mungu wetu anaweza kutumainiwa. Na neno lake ni kweli.

I. Farao aliwaachilia Waisraeli waende.

- **Ktk 12:31-36 –** Twaweza kujifunza kutokana na hali hii mbovu na tukamwamini Mungu.
- Mungu hajabadilika kamwe.
- Bado anataka tumwamini.
- Bado anahukumu dhambi.
- Bado anaziweka ahadi zake.

J. Hitimisho.

- Bwana aliwaokoa watu wake jinsi tu alivyokuwa ameahidi. Mungu atawahukumu wale wanaopigana naye kama Farao, lakini ataonyesha rehema na kuwapa Amani yake kwa wale wamtumainio.

Mungu aliwakomboa Waisraeli kwenye bahari ya Shamu na akawalinda jangwani.

A. Mungu aliwaongoza Waisraeli kwa wingu.

- **Ktk 13:17, 18 –** Tanbihi ya akiolojia: Miaka michache baadaye,waakiolojia waligundua uharibifu wa ngome za Wamisri zilizokuwa zinalinda njia iliyopita kuelekea taifa la Wafilisiti. Ndio maana Mungu aliwaongoza kuondoka kupitia jangwani.
- **Ktk 13:21 –** Idadi ya wana wa Israeli ilikuwa imeongezeka sana.
- Wakati walienda Misri walikuwa tu watu sabini.
- Sasa miaka 430 baadaye walikuwa takribani Waisraeli milioni mbili na nusu.
- Mungu aliwaongoza kila mahali alikotaka waelekee kwa kutumia wingu wakati wote.
- Kumbuka kuwa aliwapenda na hivyo alikuwa mlinzi wao kila mara.
- Aliwapa ulinzi ili kwamba siku moja mkombozi wa dunia aje azaliwe kupitia kwao.
- Kumbuka pia, Bwana aliwapa ulinzi kwa sababu alikuwa amewakabidhi Neno lake ili wapeane kwa ulimwengu. **Warumi 3:1,2**
- Katika haya yote, adui wa Mungu Shetani hakuwa tayari kuwaruhusu Waisraeli waondoke, hivyo aliufanya moyo wa Farao kuwa mgumu na kuwafuata awarudishe.

B. Farao aliamua kuwakamata Waisraeli iliyowafanya wakawa na uoga na kumlaumu Musa.

- **Ktk 14:5-7 -** Sasa Waisraeli walijawa na uoga na kumlaumu Musa.
- **Ktk 14:10-12 –** Hata baada ya kuona mambo makuu ambayo Mungu ametenda kule Misri bado hawakumwamini.
- Walakini, Musa… **Kutoka 14:13,14**
- Je, sisi ni tofauti na hawa wazee wetu? Je, tuko tayari kuliamini neno lake Mungu na kumtumainia yeye pekee.
- Hapa tena, tunaoma rehema za Mungu…hata kama Waisraeli hawakumwamini Mungu, alikuwa mwenye rehema na akapanga kuwakomboa.
- Hawangejikomboa wenyewe.
- Bahari ilikuwa mbele yao, milima pande zote nao maadui wao walikuwa wamewafuata nyuma.
- Ni Mung tu ndiye angewaokoa.
- Kumbuka Adamu na Hawa wakiwa nje ya bustani, mbali na Mungu, hapakuwa na njia nyingine yoyote ambayo ingewarejesha kwenye bustani, na hawangesawazisha uhusiano wao na Mungu. Ni Mungu tu angepeana njia kwao ili tena waweze kukubalika na Mungu. Ni Mungu ndiye aliyepeana njia kwa Habili kukubalika naye. Ni Mungu tu ndiye angemuokoa Nuhu na jamii yake kutokana na gharika. Wakati Isaka alifungwa na kuwekwa kwa madhabahu na babake ameinua kisu juu kummaliza, ni Mungu tu angemwokoa. Waisraeli hawangeweza kuzuia wazao wao wa kwanza kutokana na kifo kama Mungu hangepeana njia mwafaka. Vivyo hivyo Waisraeli hawangeweza kujiokoa kutoka kwa Wamisri pasipo na Mungu kuwatengenezea njia.
- Ni sawa tu nasi leo hii, hatuwezi jitengenezea njia ya kuepuka hukumu ya Mungu. Hatuwezi sawazisha mambo kati yetu na Mungu kwa kazi yetu nzuri. Ni Mungu tu anaweza kutuokoa kutoka kwa hukumu ya milele.

C. Mungu alifungua njia baharini.

- **Ktk 14:15,16 –** Ni Mungu aliumba bahari, kwa hivyo ana mamlaka juu yake.
- Kumbuka: Hapo mwanzo dunia ilikuwa imefunikwa na maji. Kumbuka jinsi Mungu aliamuru maji kujitenga na kuwepo kwa nchi kavu, Mungu hakuwa amebadilika. Hapa pia anaamuru maji kujitenga na watu wake kutembea kwenye nchi kavu ili wafuke ng'ambo ingine. **Ktk 14:19-30**

- **Ktk 14:31** – Tazama, wakati Waisraeli waliona jambo kuu ambayo Mungu ametenda, walimwamini.

D. Israeli walilalamika.

- **Ktk 16:1-3 –** Hata kama Mungu alikuwa amewaokoa Waisraeli kutokana na Wamisri kwa njia ya muujiza mkuu, bado tu hawakumtumainia.
- Walilalamika na kunung'unika na kumulaumu Musa na Haruni.

E. Mungu aliwaahidi chakula.

- **Ktk 16:11,12 –** Hawakustahili chochote kutoka kwa Bwana, lakini kwa neema yake (kipawa cha bure), aliahidi kuwapa chakula.

F. Mungu aliwapa chakula.

- **Ktk 16:13-15** – Mungu huwasaidia wasioweza kujisaidia; Huwakomboa wale wasio na njia yoyote ya kujikomboa. **2 Wakorintho 12:9; Isaya 40:29**
- Wakati Adamu na Hawa walitenda dhambi na kutenganishwa na Mungu, Mungu aliahidi kumtuma mkombozi ambaye angewakomboa.
- Walijaribu kutengeneza mavazi yao wenyewe kwa kutumia matawi, lakini Mungu aliwapa mavazi ya ngozi ya wanyama. Mungu kwa neema na rehema zake kuu, alikubali sadaka ya Habili. Mungu alimuokoa Nuhu na jamii yake kutokana na gharika. Mungu alimwita Ibrahimu kutoka kwa ibada ya miungu, aliokoa jamii ya Yakobo kutoka kwa baa la njaa kupitia Yusufu, alimwita Musa kuwakomboa Waisraeli kutoka Misri na akawatengenezea njia ya kupita kwenye bahari ya Shamu. Na sasa anaahidi kuwapea wana Waisraeli chakula. Hakuna yeyote ambaye alistahili rehema za Mungu kwa hawa watu wote ambao wametajwa. Mungu aliwatendea tu kuwa yeye ni mwenye rehema na neema kuu.
- **Ktk 16:35 –** hata kama Waisraeli walishukuru kwa chakula walichopewa na Mungu, walisahau tena ukuu wa Mungu ghafla na wakaanza kulalamika tena.
- Je, haya yanaonekana ya kawaida kwako?
- Sikiza kilichotendeka mara hii.

G. Israeli walilalamika tena.

- **Ktk 17:1-4** – Zingatia: Ni kwa muda upi mwanadamu aweza kuishi bila maji? Ni kwa siku chache sana. Waisraeli walihofia kuwa walikuwa wanaelekea kufa wote huko jangwani. Waweza fikiria ugumu aliopitia Musa? Hakuwa na njia yoyote ya kuwapa hawa watu maji pasipo na Mungu kuwasaidia.

H. Mungu alimwambia Musa kile cha kufanya.

- **Ktk 17:1-5,6a** – Je, ingefahamika aje kwetu kama Mungu angewaambia watengeze shimo la maji. Sasa "tungeeleza" jinsi alipeana maji. Lakini huu ulikuwa muujiza wa kweli kutoka kwa Mungu. Ni Mungu tu anayeweza kupeana maji kutoka kwenye mwamba katikati ya jangwa. Alitaka Waisraeli na (sisi) tufahamu kuwa ni Mungu tu aliyeweza kuwaokoa kutokana na mauti.
- Musa alistahili kulitekeleza hili kwa njia ambayo Mungu alitaka.
- Kila mara walipopitia janga, Mungu aliwapa njia mbadala ya kuwaokoa.
- Na pia ni vivyo hivyo nasi leo hii; hatuachiii sisi wenyewe kujifanyia njia ya kutuokoa kutoka kwa dhambi, nguvu za shetani na hukumu ya milele. Mungu hutuokoa sisi wote ambao hatujitegemei bali tunamtumainia yeye.

I.Mungu alipeana maji.

- **ktk 17:6b** – Kwa imani Musa aligonga mwamba na papo hapo chemichemi za maji zikatoka.
- Hatujafahamishwa walikuwa watu wangapi kufikia wakati huo lakini Biblia inarekodi tu wale waliokuwa na umri wa miaka ishirini ama zaidi – lakini kwa hii twaweza kusema kuwa walikuwa takribani watu milioni mbili na nusu hivi. Kulikuweko maji ya kuwatosha wao na mifugo wao**!** **Zab 105:41 –** inasema, “alifungua mwamba na maji yakatokelezea. Yalipupujika kwenye nchi kavu kama mto.”
- Ni Mungu mkuu tu angepeana maji kutoka kwa mwamba ulioko jangwani – maji ya kuwatosha watu milioni 2½ na mifugo wao. Utafiti unaonyesha kuwa walihitaji maji ndoo milioni 11 kwa siku moja.

SOMO LA 12

Maandalizi ya na kupewanwa kwa amri kumi.

Kutoka 19:1-20:2

Maandalizi ya na kupewanwa kwa amri kumi. .

A. Utangulizi.

- Katika mawazo yako, ni mtazamo upi tunaopazwa kuwa nao juu ya amri kumi za Mungu kama wakristo?
- Je , ni sheria ambazo zimewekwa ili sisi tuishi kwayo ?
- Tunaelekea kuona jinsi Mungu anavyonena kuhusu amri kumi.
- Lakini kwanza wacha tukatazame jinsi Mungu alivyo waandaa watu wake Israeli ili kupokea sheria hizi.

B. Mungu aliwaleta Waisraeli katika mlima Sinai

- **Kutoka 19:1-2** – Sasa nataka kusema hivi … Waisraeli hawakuamua wenyewe ni wakati upi watasafiri wala ni wapi wataenda.
- Mungu aliwafanyia uamuzi huo.
- Ilikuwa wamkubali kama kiongozi, mlinzi na mpeanaji wao.
- Je , na wewe na mimi ? Mungu anataka kutuongoza / kuyafinyanga maisha yetu? **Mithali 3:5-6.**
- **Kutoka 19:3-4 –** Sijui kama unakumbuka ama la? Lakini mlima Sinai/Horebu ndipo Musa aliona msitu ukiwaka.
- Kwa wakati huo, Mungu alikuwa amemuahidi Musa kuwa atamrejesha tena katika mlima huo. **Kutoka 3:1,2,12**
- Mara tena uaminifu wa Mungu ni Dhahiri.
- Tunaweza kumwamini kikamilifu kuwa kila anachoahidi atatenda.

C. Ahadi ya Bwana kwa Waisraeli.

- **Kutoka 19:5-6** – Huo ulikuwa ujumbe wa Mungu kwa Waisraeli: Aliahidi kuwabariki iwapo wangemwamin na kumtii kikamilifu.
- Kama tu wangetenda kila walicho ambiwa naye, basi angewakubali na kuwapa kila kitu jema walichohitaji.
- Yafaa kusisitiza kuwa sheria inaahidi baraka kwa misingi ya utiifu lakini laana ni kwa wale wote wanaoasi sheria mioyoni na kutotekeleza yote yanayohitajika.
- Wakati sheria ilipendekezwa, Waisraeli waliamua kukataa nafasi yao katika neema. **Msitari wa 4.**
- Mwitikio wao ungekuwa,”hakuna chenye twaweza fanya kati ya hizi vitu,tunataka tupaki katika rehema zako”. Mungu hakuhitaji uamuzi huu.

D . Ahadi ya Waisraeli kwa Bwana.

- **Kutoka 19:7-8** – Watu hawa walifikiri kuwa wangemtii Mungu vyema zaidi ili awape kila walichohitaji.

- Bado hawakukundua ya kwamba mioyo yao ilikuwa yenye dhambi na kuwa hawangeweza kumpendeza Mungu kwa nguvu zao wenyewe. **– Waebrania 11:6.**
- Walikuwa Kama Kaini aliyefikiria kuwa angempendeza Mungu kwa vitu alivyompa Mungu.
- Waisraeli hawakukundua kuwa chini ya hayo makubaliano, Mungu hangewabariki wala kuwapa kila kitu jema walichohitaji bila sheria.
- Makubaliano yalikuwa kuwa , kama wangemwamini ,na kumtii kikamilifu ,Mungu angewabariki na kuwakubali ,lakini kama wangemuasi , basi Mungu angewalaani na kuwaadhibu.
- Watu kipumbavu walikubali makubaliano haya mapya. Wangekataa na kumlilia Mungu kwa Neema na Rehema .
- Tambua ya kwamba sheria inahitaji utiifu kikamilifu. **Yakobo 2:10**

E. Mungu aliwanenea Waisraeli katika mlima Sinai.

- **Kutoka 19:16-25 –** Ni ya kushangaza kuwa Waisraeli walipokubali sheria Mungu akawa hafikiwi.
- Na sasa Musa akawa ameshuka tena kutoka mlima Sinai, Mungu aliwanenea Waisraeli katika mlima.

F. Mungu alinene na kuwapa Waisraeli Amri zake.

- **Kutoka 20:1-2 –** Tazama, mlima ulikuwa bado unatetemeka na kutoa moshi. Miale za radi ziliwaka, radi ikatanda, tarumbeta zikaibamba anga. Bila shaka watu waliingiwa na hofu na wakazalia mbali na mlima. Mungu alizungumza nao na akawapa sheria/amri kumi.
- Kumbuka ya kwamba hukumu ya kutotii amri yoyote ya Mungu ni kutenganishwa naye milele katika kiziwa cha moto ambacho Mungu aliwaandalia Shetani na wafuasi wake waliomfuata kitaka uasi wake. **Mat 25:41 ; Ufunuo wa Yohana 20:15**
- Hebu tafakari hili: Sheria za Mungu ni kama kioo.
- Kama tu tusivyoweza kuziona nyuso zetu chafu pasipo kujitazama katika kioo, vivyo hivyo hatuwezi kuziona mioyo zetu za dhambi paspoi na sheria kutufunulia. **Warumi 3:20-;7:7**
- Lakini, itakuaje kama hatutazitii amri zote za Mungu?
- Na je, Mungu atatukubali kama tutajitahidi kikamilifu kuzitii sheria nyingi kadri ya uwezo wetu? La hasha!
- **Yakobo 2:10 –** Mungu huwahukumu wenye dhambi hata Kama watakosa kutii sheria moja tu ya Mungu wakati mmoja. Je, ni mara ngapi Adamu na Hawa walikosa kutii sheria ya Mungu kabla ya kutenganishwa na Mungu na kutupwa nje ya bustani.
- Walitenda dhambi mara moja tu, na wakapokea hukumu ya kifo.
- Mungu anatuamru kutii sheria zake zote wakati wote.
- Walakini ni vigumu kwa yeyote yule kuzitimiza sheria kikamilifu kwa kuwa wote tulizaliwa wenye dhambi na tukiwa tumetengwa na Mungu .
- **Warumi 3:10-12**- Unajua ni ya kushangaza jinsi tulivyo wenye dhambi hivi kufikiria kuwa tunaweza kumtii Mungu.
- Israeli walikuwa na uhakika wangetimiza nafasi yao ya kuweka agano lao na Mungu.
- Pia sisi leo hii tunafikiria hivo – ni mara ngapi umesikia usemi kuwa, “Lo, naishi tu kwa amri kumi.”?
- Hebu tukazitazame hizo sheria/amri kumi basi.

G. Amri ya Kwanza.

- **Kutoka 20:3 –** Mungu hatawahi kumruhusu yeyota wala chochote kuchukua au kushiriki nafasi yake.
- **Isaya 45:5 –** Inasema, “Mimi ndimi Bwana, na hakuna mwingine, hakuna Mungu mwingine…” Kila kitu tunachokifanya kibao mbele badala ya Mungu kinakuwa Mungu wetu.
- Kitu chochote kisichukuwe nafasi ya Mungu katika maisha yetu.

- Ni baadhi ya vitu gani ambavyo mwanadamu hufidhamini zaidi ya Mungu? pesa, magari, nyumba za kifahari, kazi na watu.
- Hata kama tutamwabudu Mungu kwa vinywa zetu na tusimpe nafasi katika roho zetu kila wakati, tutakuwa bado tumevunja amri hii. **Kumb ya torati 8:17-20** Usiwe na miungu mingine ila mimi.
- Hukumu ya kutotii sheria hii ni kifo na kutenganishwa na Mungu. Na je , wajua kuwa sisi sote tu na hatia ya kuvunja amri hii.

H. Amri ya Pili.

- **Ktk 20:4-6 –** Hii sheria ya pili ilipeanwa na Mungu kwa Waisraeli ili kila mara wakumbuke kuwa yeye ni Mkuu kwao – mkuu kuliko vyote alivyoviumba.
- Zingatia : Mungu ni Roho , hana mwili , hakuwa na mwanzo na hatakuwa na mwisho, yu kila mahala wakati mmoja, anajua kila kitu, ni mwenye uweza wote, ni mtakatifu na mkamilifu . Ni mtukufu – Mkuu kuliko vyote. Hakuna kiumbe chochote cha Mungu au sanamu iliyoundwa na mwanadamu inastahili kuabudiwa – Ni Mung pekee wa kuabudiwa.
- Kitu kingine cha kufikiria ni kwamba hakuna yeyote anayetambua umbo la Mungu, kwa hivyo Mungu anatuonya kutojifanyia umbo lolote la kulinganishwa naye.
- **Isaya 42:8 ; Warumi 1:18-23**

I. Amri ya Tatu

- **Ktk 20:7 –** katika sheria ya tatu Mungu aliwataka Waisraeli kumheshimu, wakikubali kuwa yeye ndiye muumba wao na mfalme wao, na wasilitumie jina lake kwa njia isiyostahili.
- Zingatia: Si halali kunena uovu kuhusu watu wengine wala hata kukataa kuwaheshimu katika viwango vyao. Mtoto yafaa kuwaheshimu wazazi wake. Mke na mume wanastahili kuheshimiana. Wadogo wanastahili kuwaheshimu wakubwa wao.
- Wajua kuwa kutojali na maneno yasiyokuwa ya heshima yamekubalika katika jamii yetu. Lakini nataka kusema hivi … kumtukana mwanadamu ni vibaya, lakini itakuwa najisi namna gani iwapo tutakosa kumheshimu Mungu wa kweli na anayeishi ama kulitumia jina lake kwa njia isiyofaa?
- Wote ambao hawachamheshimu Mungu katika nafasi yake wanastahili hukumu. Mimi ni mhukumiwa. Na wewe je?

J. Amri ya Nne.

- **Kutoka 20:8-11 –** katika amri ya nne, Mungu aliwaambia kuitii siku ya sabato kama siku ya kipekee, ya kumwabudu yule aliyeumba kila kitu kwa siku sita.
- Je, wakumbuka Kile Mungu alitekeleza kwa siku ya saba, siku baada ya kukamilisha uumbaji wa dunia?
- Alipumzika kwa kuwa alikuwa amemaliza kila alichopangia kuumba.
- Tazama: Mungu hatuamru leo hii kupumzika kwa siku ya saba jinsi tu hatuamru leo hii kumtolea dhabihu ya kondoo na wanyama wengine.
- Sheria ya nne ndiyo sheria pekee ambayo haijarudiwa tena katika agano jipya. **Wakolosai 2:16, 17.** Amri zilikuwa kama ishara ya kile kitakachotendeka. Imetekelezwa kikamilifu Kama tu ilivyostahili katika Yesu Kristo.

K. Amri ya Tano.

- **Kutika 20:12 –** katika amri ya tano, Mungu alisema kuwa watoto wanastahili kuwaheshimu na kuwatii wazazi wao. **Waefeso 6:1-3**
- Hakuna yeyote ambaye amewatii wazazi wake kikamilifu.

- Sisi wote tumevunja amri hii na hata zile zingine. Kumbuka hata kama tutatekeleza sheria zote tisa na tukose kutii moja wapo, Mungu bado atatuhukumu.
- Tena, Mungu anatarajia tutekeleza sheria hizi kikamifu kutoka wakati wa kuzaliwa hadi wakati wa mwisho.
- Tendo moja tu lakutotii litatutenga daima na Mungu.

L. Amri ya Sita.

- **Kutoka 20:13 –** Amri ya sita – kumuua mtu ni dhambi mbele za Mungu.
- Yeye ni muumba wa watu wote.
- Hupeana maisha kwa kila mtu.
- Hakuna yeyote anaruhusiwa kuchukuwa uzima wa mwenzake kama Mungu hachasema hivo katika neno lake.
- Mungu pia anasema wazi katika neno lake kuwa, kama mtu anamchukia mwenzake, basi ametekeleza mauaji moyoni mwake.
- Hata kama mtu atafikiria tu kumuua mwenzake, yeye ni muuaji tayari na amehukumiwa na Mungu. **Mat 5:21-22**

M. Amri ya Saba.

- **Kutoka 20:14 –** katika amri ya saba, Mungu anasema kuwa ni dhambi kutekeleza ngono na mtu ambaye si mke ama mume wako. Watu wengi husema kuwa sheria hii ni ya kale na sasa hivi haina mashiko yoyote. Lakini Mungu habadilikiki. Dhambi inapaki kuwa dhambi hadi leo hii. Mungu hajabadili mawazo yake juu ya usinzi. Kama tu uuaji, dhambi zote za usinzi hutekelezwa mawazoni mwetu. **Mat 5:27-28**

N. Amri ya Nane.

- **Kutoka 20:15 –** katika amri ya nane, Mungu alisema kuwa hawakustahili kuchukuwa kitu ambacho si miliki yao.
- Mungu Ndiye hupeana haki kwa mtu kutenda kazi na kuhifadhi mali yake.
- **Matendo 17:25 –** Inasema kuwa Mungu, “Ndiye anayewapa wote uzima na pumzi na vitu vyote.”
- Kama mtu atachukuwa kitu kisichokuwa chake, basi ametenda dhambi mbele za Mungu.
- Mungu hatakubali malipo mengine isipokuwa mauti. Mungu hawezi samehe dhambi yoyote pasipo malipo kamilifu ya mauti kulipwa.
- Hata kama mtu atataka kuiba kitu na asiibe kwa kuogopa kuwa atashikwa, bado analaumiwa kwa kosa la wizi mbele za Mungu.

O. Amri ya Tisa.

- **Kutoka 20:16 –** katika amri ya tisa Mungu anataka tuseme kweli katika kila neno.
- Mungu huwa hadanganyi na basi anatuamru tusidanganye pia.
- **Tazama:** Shetani ni mwongo. Aliwadanganya Adamu na Hawa katika Bustani. Aliwadanganya wazee wetu wa kale na hata leo hii bado anawadanganya watu katika dunia nzima. Shetani ndiye baba wa uongo. **Yoh 8:44**
- Watu wengine huanza rambirambi zao na kuanza hadithi. Wengine huziendeleza na hata kuongezea. Watu wengine hupenda masengenyo. Kinacho anza kama uhalisi hutiwa uongo na ujumbe halisi hupotea. Hii yote ni kudanganya na Mungu anachukia uongo na atawahukumu waongo.

P. Amri ya Kumi.

- **Kutoka 20:17 –** Amri ya kumi, Mungu alisema kuwa tusitamani, yaani, kutaka kile mtu mwingine anamiliki.
- Hii ilikuwa dhambi ambayo shetani alitenda.
- Aliingiwa majisifu na kutamani nafasi ya Mungu.
- Watu wengi ni walafi na wana wivu juu ya miliki za wengine. Wanachukia watu walio na miliki nyingi kuwaliko, na wanatamani miliki za watu wengine. Hawajawahi kutosheka na miliki zao wenyewe. Kila mara wanatamani kuongezeka.
- Mungu hajawahi kubadili mawazo yake juu ya tamaa.
- Atahukumu tamaa yote kwa kuwa ni dhambi.

Q. Hitimisho.

- Hizi ndizo Amri kumi ambazo zilipeanwa na Mungu kwa Waisraeli. Na Amri zake zinatenda kazi kwa kila mtu, kila mahali.
- Hukumu ya dhambi ni mauti na kutenganishwa na Mungu milele katika mahali pa hukumu, alikomwandalia Shetani na malaika wake.

SOMO LA 13

Maskani - Kutoka 24:12 - Mambo ya Walawi 16:3.

Maskani

A. Musa na Yoshua walipanda mlimani.

- **Kutoka 24:12-18 –** Musa alipokuwa mlimani, Bwana alimpa amri kumi zilizoandikwa kwa vipande mbili za mawe, na akamfafanulia sheria zingine alizowaamru wana wa Israeli kuzifuata. Zingatia kuwa Mungu alikuwa mfalme wao na aliwaambia kila kitu alichotaka wafanye.
- Kama wangetii sheria zake, angekuwa pamoja nao, angewalinda na kuwapa kila kitu walichohitaji. Lakini kama wangekosa kuzitii amri hizo, adhabu yao ingekuwa mauti. Hata hivyo, Bwana alijua wana wa Israeli ni wenye dhambi na hawangeweza kuzitii amri na sheria zake kila mara. Alijua ya kuwa kama hawangekuwa na njia ya kuhepuka, angehukumu kila mmoja wao.
- Na hata wakati Mungu alikuwa akimpa Musa maagizo yake mlimani, watu walikuwa tayari wanazivunja amri zake. Hebu turuke mbele kwa sura chache. **(Kutoka 32:1)**
- Walakini, Mungu aliwapenda, hakutaka kuwaangamiza. Kwa hivyo aliwaeleza wakajenge mahali maalumu ambapo wangeshiriki naye pamoja, na ambapo angewafunza jinsi ya kushiriki na Mungu mtakatifu bila ya kuangamizwa.

B. Mungu aliamuru Musa kujenga maskani.

- **Ktk 25:1-8 – (makinika na msitari wa 8)** – hii haikumaanisha kuwa Mungu hangepatikana kila mahali. Hata akija kuishi humo maskani, ataendelea kuwa kila mahali wakati wote.

C. Maskani ni lazima ijengwe kulingana na vile Mungu alimuamuru Musa.

- **Ktk 25:9 –** Neno la Kiebrania lililotumika kumaanisha maskani ni, hema, mahali pa kuishi au nyumbani.
- Kila kitu katika ujenzi wa maskani hiyo, ilikuwa iwe jinsia Musa aliambiwa akiwa mlimani.
- Yote ilipaswa kutendeka kulingana na maagizo ya Mungu.
- Kumbuka Kaini alikataa njia halisi ya Mungu ya kuja mbele zake na hivyo hangekubali kamwe.
- Lakini Nuhu alikuwa tofauti, Tofauti na Kaini yeye alitii maagizo ya Mungu na kujenga safina kama tu alivyotaka Mungu. Mungu alikubali na hivyo kumwokoa Nuhu na jamii yake.
- Hatuwezi mweleza Mungu jinsi ya kwenda mbele zake.
- Inatulazimu kuja mbele zake kulingana na njia yake anayotufunza.
- Hivi sasa Mungu alimweleza Musa jinsi ya kuijenga maskani.
- Ingejengwa hasaa kwa ngozi za wanyama na nywele ya mbuzi na lilistahili kuwa na vyumba viwili.

D. Patakatifu pa Watakatifu.

- Chumba cha kwanza ambacho kiliingiwa kwa mlango wa nje kiliitwa patakatifu.
- Nataka kusema hivi: Mungu ni mtakatifu, mkamilifu, mwenye haki na ametengwe na watenda dhambi. Kumbuka ya kwamba Adamu alitenganishwa na Mungu kwa sababu ya dhambi.
- Hiki chumba kilitengwa hasaa kwa ajili ya Mungu pekee yake, na makuhani wake wakati wakimtumikia.
- Tutasoma kiasi kuhusu makuhani kwa muda mchache.

- Chumba cha pili, cha ndani, kilikuwa hasaa cha muhimu zaidi, hiki kiliitwa patakatifu pa watakatifu. Hiki chumba kilikuwa cha Mungu pekee na kuhani mkuu aliruhusiwa kuingia huko mara moja tu kwa mwaka.
- Kulikuwepo na uwepo wa Mungu katika chumba hiki cha ndani.
- Hiki ni chumba muhimu ambamo Mungu aliahidi kuishi.

E. Sanduku la agano na kiti cha rehema.

- **Ktk 25:10, 11** – Mungu pia alimwongoza Musa kutengeneza sanduku, ambalo lilipaswa kuwekwa katika chumba hicho cha ndani, mahali patakatifu pa watakatifu.
- Hili sanduku ambalo ni sanduku la agano, ilipaswa liundwe kutoka kwa mti Fulani uliochaguliwa na Mungu.
- Baada ya kuundwa kwa sanduku hili la agano walipaswa kulifunika na dhahabu.
- **Ktk 25:17** – Musa aliambiwa kutengeneza kifuniko kwa kutumia dhahabu pekee na kufunikia sanduku la agano katika chumba cha ndani.
- Kifuniko kiliitwa kiti cha rehema.
- Kiti cha rehema kilikuwa cha muhimu zaidi kuliko sehemu zote maskani.
- Hapa ndipo Mungu aliahidi kuishi na Waisraeli wenye dhambi na kuwaonyesha rehema zake.
- Rehema ni njia ya Mungu kwa mwenye dhambi kuepuka hukumu ya dhambi anayostahili. Rehema sio kupewa tunachostahili**. Maombolezo 3:22; Zaburi 136; Yakobo 2:13**
- **Ktk 25:18 –** Je, wakumbuka mara ya mwisho tuliposikia kuhusu makerubi? Mungu aliwaweka makerubi kuilinda bustani la Edeni ili Adamu na Hawa wasirejee tena katika bustani wakakula kutoka kwenye mti wa uzima.
- **Ktk 25:19, 20 –** Makerubi wawili waluwa wawekwa wakiangaliana katika pande zote za kiti cha rehema.
- Mapawa yake ilikuwa itengenezwe kwa njia ambapo yangeweza kufikiana kufunika kiti cha rehema.
- Nyuso zao ilipaswa zitazame kifuniko cha sanduku la agano.
- **Ktk 25:21, 22 –** Sanduku la agano lilipaswa kuwekwa kwenye chumba cha ndani, ndani ya pazia.
- Bwana alimweleza Musa aweke lile jiwe la vipande mbili ndani ya sanduku hilo la agano, chini ya kiti cha rehema. Hizi vipande mbili za jiwe ndizo kulikoandikwa amri kumi za Mungu.
- Mungu aliahidi kuwa baada ya kila kitu kukamilika jinsi alivyoahidi basi ataingia na kuketi kwenye chumba cha ndani.
- Uwepo wake ulionekana kama mwangaza mkubwa katikati ya Makerubi.
- Huu mwangaza mkubwa uliitwa utukufu wa **Shekinah** au uwepo wa Mungu.

F. Pazia.

- **Ktk 26:31-33 –** Mungu alimwambia Musa kuwa alistahili kuweka pazia nzito ya kupendeza katikati ya vyumba hizi mbili.
- Hizi vyumba ziliwakumbusha Waisraeli kuwa walitengwa na Mungu kwa sababu ya dhambi.

G. paa ya Maskani na madhabahu ya shaba.

- Mungu alimwambia Musa kutengeneza ua la vitambaa za pazia na kuiweka tete katikati ya milingoti na aiweka izunguke vyumba hizo mbili.
- **Ktk 26:14 –** vyumba hizo mbili vilifunikwa kwa ngozi za wanyama zilizopakwa rangi na kisha paa la ngozi za wanyama.
- Ndani ya malangoni pa ua ya pazia, ilikuwa iwekwe madhabahu, ambayo Mungu alisema kuwa yatengenezwe kwa mbao na shaba.

- **Ktk 27:1, 2** – Wakati mtu alitaka kusungumza na Mungu, kitu cha kwanza kutenda ilimpasa alete dhabihu/sadaka.
- Ilikuwa ailete sadaka kwenye madhabahu ya shaba, humo ndani mwa lango, aweke mkono wake kwa kichwa cha mnyama na kisha kumuua yule mnyama.
- Kwa kufanya hivi iliashiria kukubali kuwa mtenda dhambi na anayestahili kifo.
- Kwa kuweka mkono wake kwenye kichwa cha mnyama ilikuwa sawa na kujilinganisha na yule mnyama anayekufa kwa nafasi yake.
- Lakini sasa ilikuwa kama kumwomba Mungu akubali kifo cha mnyama badala yake.
- **Mambo ya walawi 1:1-5; 17:11; Waebrania 9:22 –** Nataka kuuliza hivi: Je, damu ya mnyama yaweza kulipia dhambi? LA HASHA**! Waebrania 10:4**
- Damu ya mnyama ilikuwa tu ukumbusho kuwa malipo ya dhambi ni mauti ama kutengana kwa mtenda dhambi na Mungu.
- Kwa kawaida Mungu siku hizi huwa hatuamuru kutoa sadaka ya wanyama, lakini hiyo ilikuwa njia pekee aliyowatengenezea Waisraeli wakati ule.
- Mungu alikuwa anaenda kutengeneza njia mwafaka dhidi na dhambi. **Waebrania 9:23**

H. Haruni na wanawe wafanywa makuhani.

- **Ktk 28:1 –** Mungu alimchagua Haruni na wanawe kuwa makuhani. Ni Haruni tu yaani kuhani mkuu aliruhusiwa kuingia katika chumba cha ndani, mahali patakatifu zaidi ambapo Mungu aliketi.
- Mtu yeyote mwingine alingeingia kule, angeuawa**, Hesabu 3:38**
- Haruni aliruhusiwa kwenda katika chumba cha ndani mara moja kwa mwaka na hiyo ni siku ya utakaso yaani "siku ya kufunikwa" **Waebrania 9:7 - (Neno utakaso linamaanisha malipo ama kuridhisha)**
- Njia moja tu ambayo angeingia ni kwa kuja na damu ya mnyama aliyetolewa kama dhabihu.
- Mambo ya **walawi 16:2, 3** – Kabla ya Haruni kuingia mahala patakatifu alistahili kumuua mnyama na kuingia na damu ya huyo mnyama kwenye basini.
- Tena baada ya kupita pazia nzito, iliyoning'inia, katikati pa vyumba hizo mbili, Haruni alistahili kunyunyisa damu hiyo kwenye kiti cha rehema, kifuniko safi cha sanduku la agano.
- Kama tu kila kitu kingetendeka jinsi Mungu alimweleza Musa basi Mungu angewasamehe dhambi zao za mwaka uliotangulia. **Mambo ya walawi 16:34**
- Je, damu ya wanyama ingewalipia hukumu yao ya dhambi? La!
- Hukumu ya dhambi ni mauti.
- Dhambi lazima ilipiwe kikamilifu.
- Licha ya hayo Mungu aliahidi kutowahukumu kwa dhambi ya mwaka uliotangulia, kama wangemjia kwa njia aliyowaeleza.
- Yawafaa waje mbele zake wakiamini na kuleta dhabihu ya damu kwa sababu ya dhambi zao.
- Mungu huwakubali tu wanaomkubali na kumjia kwa njia anayosema.

I. Maskani ilikamilika na kusimamishwa, na Mungu akaja kuishi ndani mwake kama nyumba yake.

- Hatimaye maskani ilimalizika.
- **Ktk 39:42,43; 40:17** – kama hawangetengeneza kikamilifu jinsi Mungu alitaka basi Mungu hangekuja kuishi nao humo ndani.
- Lakini kwa kuwa Musa na Waisraeli walitenda kikamilifu jinsi Mungu aliwaambia, Mungu alikuja akaishi katikati yao na mahali patakatifu pa hekalu.
- **Ktk 40:34 – 35 -** Waisraeli sasa wangekuja mbele za Mungu kwa njia aliyowaeleza.
- Kila mwaka Haruni angeingia mahali patakatifu pa watakatifu na kunyunyisa damu ya mnyama kwenye kiti cha rehema chini ya makerubi.

- Mbona kuhani mkuu alirudia kufanya hivyo kila mwaka?
- Ni kwa sababu damu ya mnyama haiwezi kulipia dhambi…
- **Ktk 10:4 –** inasema,"…haiwezekani kuwa damu ya fahali na mbuzi yaweza kulipia dhambi zetu."
- Kwa rehema zake Mungu, hakuwa akishikilia dhambi ya Waisraeli kwa mwaka uliofuata.

SOMO LA 14

Kutoamini kwa Israeli ; Hukumu na Ukombozi wa Mungu - Hesabu 13:1- 21:9

Israel katika nchi ya ahadi chini ya waamuzi na wafalme –Yoshua 1:1-2- Mambo ya nyakati wa pili 5:1

Kutoamini kwa Isreli; Hukumu na Ukombozi wa Mungu.

A. Utangulizi.

- Kumbuka jinsi wana Waisraeli walitetemeka kwa hofu ya Mungu aliponena nao kutoka mlima wa Sinai.
- Sasa Mungu alikuwa akikaa katikati yao kwa neema akiwaonyesha rehema waliohitaji na kwa uwaminifu kuendelea kuwapa mana na maji jangwani.

B. upelelezi wa nchi ya ahadi.

- Sasa Mungu alililinua wingu kutoka mlima Sinai ambapo aliwapa amri kumi na watu wakalifuata wingu liliposonga na Bwana akawaelekeza hadi ukingoni mwa nchi aliyoahidi kuwapa.
- **Hesabu 13:1-3 –** Musa alimtii Bwana na akawatuma watu kumi na wawili kuitazama nchi na watu waliokuwa wakikaa pale. Hata hivyo waliporudi walisema hivi…

C. Wapelelezi kumi hawakuamini.

- **Hesabu 13:25-33** – hawa watu walikuwa wanasema ukweli.
- Watu hodari waliimiliki nchi na wengi wao walikuwa majitu.
- Lakini wapelelezi kumi walikuwa wamesahau mambo makuu na makubwa ambayo Mungu alikuwa amewafanyia.
- Walikuwa wamesahau kuwa, hakuna kisichowezekana kwa mungu.
- Walikuwa wamesahau miujiza yote ambayo Mungu alifanya kule Misri na jinsi alivyowakomboa kutoka utumwani.
- Hawakuamini kuwa Mungu anazo nguvu za kutosha kuwashinda watu wa Kanaani na kuwapa nchi.

D. Kalebu na Yoshua walimwamini Mungu.

- Wapelezi wawili Kalebu na Yoshua walimwamini Mungu wao.
- Wao kama wengine walikuwa wameona kuta zenye nguvu zilizozunguka miji ya Kanaani.
- Pia walikuwa wameona kimo cha watu lakini walikumbuka mambo makuu ambayo mungu alijkuwa ameyafanya na wakaamini kuwa atawaondoa watu wa Kanaani na kuwapa wanaisraeli nchi alivyoahidi.

E.Waisraeli hawakuamini Mungu.

- **Hesabu 14:1-4** – Bwana alisikia kila kitu Waisraeli walisema.
- Alijua kuwa hawakumwamini walichokuwa wakisema ni kuwa Mungu ni mwongo.
- Alikuwa ameahidi kuwapa nchi lakini hawakuamini na hawakumtegemea.
- Na sisi je? Tunapolisikia neno la Bwana na tusiamini je, nasi twamwita Mungu mwongo?

F. Mungu aliwaambia wote watafia jangwani.

- **Hesabu 14:26-32 –** wote waliokuwa miaka ishirini na zaidi na hawakumwamini Mungu wangekufia jangwani isipokuwa Yoshua na Kalebu walioamini.
- Na baada ya miaka arobaine baada ya wote kufa, basi Mungu angewapeleka wanao pamoja na Yoshua na kalebu katika nchi kuimiliki.
- Nataka kusema hivi, ni jambo hatari kutomwamini Mungu.
- Kumbuka shetani alipomwambia Hawa kuwa hangekufa akila tunda la mti wa maarifa ya mema na maovu. Shetani alimwita Mungu mwongo, na Hawa akamwamini. Kaini pia hakumwamini Mungu na akamwendea Mungu kwa njia yake. Mungu alimkataa na dhabihu yake. Nuhu alipowaambia watu kuwa gharika kuu inakuja kutoka kwa Mungu walikataa kumwamini Mungu. Hawangeingia kwenye safina na wakaangamia. Wamisri pia hawakumwamini Mungu kuwa yeye ni mwenye nguvu na Mungu wa kweli. Waliamini miungu yao kuwakomboa,lakini Mungu aliharibu nchi yao, akawaua wazaliwa wao wa kwanza na kuwazamisha majeshi yao baharini.
- Mungu atahukumu kila mtu anayekataa kumwamini.
- Kwa sababu ya kutoamini kwao Mungu aliwafanya kuzunguka jangwani hadi watu wote wazima wasioamini wakakufia jangwani. **Waebrania 3:12, 17-19**

G. Wana Waisraeli walimlaumu Musa na Haruni kwa sababu hawakuwa na maji.

- **Hesabu 20:1-2 –** Wana Waisraeli walimulaumu Musa na Haruni nduguye kwa sababu hawakuwa na maji.
- Mbona hawangemuuliza Mungu awape maji?
- Alikuwa amewapa maji kutoka kwa mwamba walipohitaji hapo awali.
- Sababu iliyowafanya wasimuulize Mungu ni kuwa hawakumwamini na kumtegemea.
- Kuna watu wengi leo hii walio kama Waisraeli , hawamwamini Mungu
- Hata ingawa ameumba na kutupa vitu vyote ikiwemo uhai wetu.
- Wengine hata husema hawamwamini Mungu kwa sababu ya majanga/matatizo ambayo yamewatendekea wenyewe au wapendwa wao.
- Baada ya kujifunza Biblia umbali huu, tunajua kuwa sio makosa ya Mungu kuwa watu wanateseka, ni matokeo ya dhambi ya mwanadamu tunateseka kwa sababu ya dhambi za vizazi vyetu na hata viumbe vyote huteseka kwa sababu ya dhambi za wanadamu kinyume na Mungu. **War 8:19-22**

H. Mungu alimwamuru Musa kunena na mwamba.

- **Hesabu 20:7-8 –** Bwana alimwamuru Musa kuunenea mwamba.
- Hapo awali walipohitaji maji Bwana alimwamuru Musa kuugonga mwamba **Kutoka 17:5-6**
- Lakini mara hii, Bwana alimwambia kunenea mwamba tu.
- Zingatia kwamba kila wakati, Mungu alikuwa akiwaambia jinsi walistahili kutenda mambo.
- Sikiliza kilichofanyika.

I. Musa hakutii.

- **Hesabu 20:9-11 –** Musa na Haruni waliitikia kwa hasira badala ya kumtegemea Mungu.
- Mungu alitaka kuwaonyesha watu kuwa yeye ni mwaminifu, kuwapa maji jinsi alivyokuwa ameahidi. Kila wakati yeye hutimiza ahadi zake kwa kuwa yeye ni mtakatifu na mkamilifu.

- Lakini badala ya kuwaonyesha watu uaminifu na utakatifu wa Mungu Musa na Haruni walionyesha hasira yao.

J. Hukumu ya Bwana juu ya Musa na Haruni.

- Kwa sababu hii, Mungu alimwambia Musa na Haruni kuwa hawangeruhusiwa kuingia katika nchi ya Kanaani. **Hesabu 20:12**

k. Wana Waisraeli walinung'unika tena na Mungu akawatumia nyoka wakali.

- Tunapoendelea kulipitia agano la kale kwa uharaka, hebu tuzingatie andiko moja la kushangaza. **Hesabu 21:4-6 –** Waisraeli walikufa kwa sababu ya kuumwa na nyoka. Hii ilikuwa hukumu ya Mungu juu yao kwa sababu ya dhambi zao.
- Mungu akiamua kuwaadhibu wenye dhambi, hakuna mahali ambapo wanaweza kujificha kutoka kwake.Katika siku za Nuhu kulikuwa na mahali pa kujificha na watu kuepuka hukumu baada ya Mungu kufunga mlango wa safina na kutuma gharika? Watu wa Sodoma na Gomora wangeepuka hukumu ya Mungu alipotuma moto na makaa juu yao? Mkewe Lutu angeepuka hukumu ya Mungu alipokataa kumtii Bwana na kutazama nyuma? Mungu anapoamua kuleta hukumu juu ya watu hakuna mahali popote ambapo wanaweza enda kuepuka. **Ufunuo 6:15-17**
- Mungu alipotuma nyoka ya sumu katikati yao Waisraeli walibadili nia yao haraka kumwelekea Mungu na kukubali dhambi zao.
- **Hesabu 21:7 –** Waligundua sasa kwamba ni Bwana pekee angewaokoa kutokana na hukumu yake. Na kwa hiyo wakamuuliza Musa amwambie Mungu awaokoe.
- Hawangejisaidia wala Musa hangewaokoa kutokana na nyoka. Mungu pekee angewaokoa.

L. Nyoka wa shaba.

- **Hesabu 21:8** – Bwana hakuwaambia watafute njia yao wenyewe ya kupona.
- Mungu alimwambia Musa cha kufanya.
- Musa alihitajika kufanya kile Mungu alimwambia na watu walitakikana kutazama nyoka jinsi Mungu alivyomwakiza musa.
- Ilifaa kufanywa katika njia ya Bwana.

M. Hitimisho.

- **Hesabu 21:9 –** Bwana alisema nini walichostahili kufanya ili kupona kutokana na kuumwa na nyoka? Walitakikana tu kumtazama nyoka wa shaba. Je, nyoka wa shaba alikuwa na nguvu ndani mwake kuwaponya? Hapana, Nguvu ilitoka kwa Mungu.
- Bwana aliwaponya kwa sababu walimwamini**. 2 Wafalme 18:1-4.**

Waisraeli katika nchi ya ahadi chini ya waamuzi na wafalme. .

A. Utangulizi.

- Wana Waisraeli walizunguka jangwani kwa miaka arobaini na kizazi cha wote waliokataa kumwamini Mungu kuwa angewapa nchi ya ahadi walikufa**. Waeb 3:17-19**
- Vile Mungu alikuwa amesema, Musa na Haruni pia walikufa kabla Waisraeli kufika katika nchi ya ahadi**. Kumb 34:1-6 -**Mungu alimteua Yoshua kuwa kiongozi mpya wa watu wake.

B. Yoshua aliwaongoza Waisraeli kuingia Kanaani.

- **Yoshua 1:1-2 –** Watoto wa wale waliokataa kumwamini Mungu walikuwa watu wazima sasa na ulikuwa wakati wa Mungu kuwapeleka katika nchi ya ahadi.

- Ingawa shetani na Farao walijaribu kuwazuia Waisraeli wasiondoke Misri na hata ingawa Waisraeli walikuwa na shaka na Mungu mara nyingi, bado alifanya kile aliahidi. Aliwatengenezea njia katikati ya bahari ya Shamu, aliwaongoza, aliwalinda na kuwapa maji na chakula kwa miaka arobaini walipozunguka jangwani.
- Bwana hakushindwa kufanya chochote alichowaahidi.
- **Yoshua 11:23 –"** Yoshua alichukuwa nchi yote".
- Kabla ya kufa kwake, Yoshua alisema haya kwa Waisraeli, **Yoshua 23:14**
- Lakini zingatia onyo la Yoshua kwa watu **Yoshua 23:16**

C. Wana Waisraeli waligeukia miungu baada ya kifo cha Yoshua.

- Yoshua alipokuwa mzima Waisraeli walimkumbuka Mungu. Lakini baada yake na wale walio ona miujiza ya Mungu jangwani kufa Waisraeli walimsahau Mungu.
- Walizifuata njia za mataifa ambayo haikumtambua Mungu wa kweli aliye hai.
- Walijifanyia miungu na kuiabudu badala ya Mungu.
- Mungu alitaka kuwaondoa Wakanaani walioabudu miungu lakini Waisraeli walikataa kumwamini na kumtii Mungu.
- Kwa hivyo Mungu aliwaruhusu baadhi ya Wakanaani kubaki na badala ya kumtegemea Mungu Katika nchi ya ahadi,waliiga njia za uovu wa Kanaani. **Zab 106:34-42**
- Bwana akahukumu Israeli kwa sababu walimsahau na kuabudu miungu.
- Mungu aliruhusu mataifa yaliyozunguka na kuchukia Israeli, kuwapiga na kuwafanya watumwa wao.
- **Waamuzi 2:14-15 –** Bwana alikuwa amewaonya Waisraeli kwa kurudia rudia kuwa, **Hesabu 33:50-53 - ,Kumb 8:19**
- Mungu habadiliki.
- Hata kama miaka mingi itapita, Mungu atakumbuka ahadi zake, zikiwemo ahadi za kuwahukumu wale wasioamini. **Yoshua 23:9-13 , 24:20**

D. Nyakati za Waamuzi.

- Katika kitabu chote cha waamuzi tunaona mfano ufuatao, wana waisraeli wakimsahau na kumtoroka Bwana, Bwana akimwinua adui kupigana nao na waisraeli walipotubu na kukubaliana na Mungu juu ya dhambi zao na kumuita Mungu awasaidie, alimchagua mwanaume au mwanamke kuwakomboa na maadui zao. Hawa wakombozi waliitwa Waamuzi.
- Lakini mara baada ya ingine, waisraeli walimsahau Bwana.
- Kwa hivyo Bwana aliruhusu maadui wao wa washinde mara kwa mara.
- **Waamusi 2:13-19** Ijapokuwa wana Waisraeli hawakumtii Mungu na Mungu aliwaadhibu,kama vile tu wazazi wanavyo wapenda watoto ijapokuwa wamekosa kuwatii.
- Kumbuka katika shamba la Edeni,Bwana aliaiti kumtuma Mwokozi atakaye muharibu Shetani na kuukomboa ulimwengu kutoka kwa nguvu za Sheteni. Pia ahadi ya mkombozi ilipeanwa kwa Ibrahimu,Isaka,na Yakobo na kuwahakikishia kwamba Mwokozi atatokana na uzao wao.Kwa hivyo,Mungu aliwapa Israeli ulinzi maana alikuwa alimiza ahadi ya Mkombozi kupitia kwao.
- Saidi ya hiyo, Mungu alitaka ulimwengu umjue.
- Tunaweza tu kumjua Mungu kupitia Bibilia.
- Nikupitia tu kwa waisraeli Mungu alitupa sisi Biblia. **Warumi 3:1-3**
- Kumbuka waandishi wa Biblia walikuwa Wayahudi isipokuwa mmoja.
- Kwa hivyo Mungu alizingatia sana kuhifadhi Israeli ili neno lake na hadithi ya mkombozi ifunzwe katika vizazi vyote.

E. Nyakati za Wafalme.

- Sasa tusonge kutoka kitabu cha waamuzi hadi nyakati za wafalme.

- Kati ya mataifa yote ulimwenguni, Israeli ndilo lililobahatika Sana, kwa sababu mfalme wao alikuwa Mungu mwenyewe. Hata hivyo baada ya Muda Israeli ilimkataa Mungu na kutaka kuwa na mfalme kama mataifa mengine. **1 Samueli 8:4-6 –** Mungu alikubali haja yao. Mstari wa **7**. Kuanzia wakati huo kwenda mbele, wafalme wengi walitawala Israeli. Wachache kati yao walimwamini na kumtegemea Mungu. Lakini wengi hawakuweza.
- Waliabudu miungu na kuongoza Israelui katika kuvunja amri za Mungu.
- Sasa Sauli alikuwa mfalme wa kwanza na tena mfalme wa kwanza kugeuka kutoka katika njia ya Bwana kwa kutoamini. **1 Samueli 15:1-28**
- Mfalme wa pili alikuwa Daudi

F. Daudi, mfalme mkuu wa Israeli.

- **2 sam 5:3-4 –** Kinyume na wafalme wengine wengi waliotawala juu ya Israeli, Daudi kwa ukweli alimwamini Bwana na alitaka kumtii kwa kila kitu ingawa mara nyingi alishindwa.
- Daudi kama na sisi alizaliwa mtenda dhambi, tofauti kubwa ni kuwa Daudi alijua ya kuwa yeye ni mwenye dhambi na mshahara wa dhambi ni mauti. Alijua tumaini lake la pekee liko katika rehema za Bwana na msamaha. Kwa Imani alitoa dhabihu kwa dhambi zake kwa sababu Daudi alimtegemea Mungu alikubaliwa na kusamehewa kama, Abeli, Enoka, Nuhu, Ibrahimu, Isaka na Yakobo.
- Kitu cha kufikiria ni kwamba Mungu alimpa Daudi Ahadi tu kama alivyo wapa Ibrahimu,Isaka na Yakobo.
- Mungu alimwahidi Daudi kuwa mwokozi wa mwanadamu na mshindi juu ya shetani atatoka katika jamii yake. **2 Sam 7:13b-16**
- Kabla ya kufa kwake, Daudi alimpa mwanawe Suleimani jukumu la kujenga nyumba ya Bwana lakini Daudi mwenyewe alikusanya na kuaandaa vifaa vya kujenga.

G. Mfalme Suleimani mwana wa Daudi ajenga hekalu.

- **Mambo ya nyakati 22:5-6 –** Suleimani alikuwa mfalme wa Israeli baada ya kifo cha babake, Daudi.
- **1 Nyakati 29:26-28** – Suleimani alijenga nyumba ya Bwana Yerusalemu.
- **2 Nyakati 2:1-,5:1 –** Sasa hema la mkutano halikuitajika tena ambalo waisraeli walijenga wakiwa jangwani wakitumia ngozi ya wanyama na nguo
- Hii nyumba mpya ya Mungu iliitwa hekalu.
- Hekalu la bwana lilikuwa na vyumba viwili ndani na vyombo vingine kama hema lla mkutano.
- Pazia nzito iliwekwa kufunika patakatifu pa watakatifu. Chumba cha ndani ambapo Mungu angekaa.
- Lile pazia ilikuwa ishara ya kutoingia mle ndani kwa kila mtu isipokuwa kuhani mkuu pekee.
- Ilikuwa mfano wa utengano kati ya Mungu mtakatifu na mwanadamu mwenye dhambi.
- Wakati hekalu liliwekwa wakufu na dhabihu kutolewa kwa Bwana, Mungu alishuka na kukaa patakatifu pa watakatifu katika hekalu jinsi alivyoingia kwenye hema la mkutano – **2 Mambo ya Nyakati 7:1 – 3**
- Kumbuka hata kuhani mkuu aliruhusiwa kuingia chumba hiki cha ndani mara moja kwa mwaka kwa niaba ya watu. Waisraeli hawakumwendea Mungu wenyewe. Njia pekee ya kukubalika machoni pa Bwana ilikuwa kwa kumtegemea kuhani mkuu na damu ya wanyama aliotoa kwa niaba yao.Waisraeli hawakutakikana kusahau kuwa ni wenye dhambi, Mungu ni mkamilifu na kuwa hukumu ya dhambi ni mauti.kwa kuwa damu ya wanyama haikuweza kulipa deni lao, ilifaa kuwekwa mbele za Bwana kila mwaka
- Kila mwaka kuhani alichukuwa damu Ya wanyama na kuingia nayo mbele za Bwana katika chumba takatifu hekaluni kila mwaka na kuinyunyuza katika kiti cha rehema na kwenye chuma cha dhahabu cha sanduku la agano…**Mambo ya walawi 16:2-3,34.**

- Mungu hakutaka waisraeli wasahau kuwa wao ni wenye dhambi, na kujua kwamba Mungu pekee ni mukamilifu,Na mshahara wa dhambi ni maudi.Kwa sababu damu ya wanyama hainge weza kulipa deni ya dhambi,Damu ilihitajika kuwasilishwa mbele za Mungu kila mwaka. **Waebrania 10:4**
- Kila mwaka Mungu alisamehe dhambi zao na kuzuia hukumu yake akingoja wakati ambapo malipo kamilifu ya dhambi yatakapofanywa.

H. Baada ya Suleimani kufa, wafalme wengi walitawala Israeli.

- Baada ya kufa kwa Suleimani, taifa la Israeli walipishana ni nani akuwe mfalme, na wakatawanyika katika falme mbili – **wafalme wa kwanza 11:9-13 na 31-37**
- Makabila kumi za kasikazini waliitwa Israeli na makabila mawili ya kusini waliitwa Yuda.

I. Hitimisho.

- Tumejifunza historia pana ya Israeli na mahali hapa, tunasonga haraka kupitia agano la kale ili tupate mtazamo mzuri wa ujumbe wa Mungu kwetu.

SOMO LA 15

Mungu aliwatuma manabii wake kwa taifa la Israeli lakini Waisraeli walikataa kuyazingatia maonyo yao Isaya 10:5-6, Yeremia 6:13-14, 2 Wafalme 17:1-8, 25:1-12.

Mungu alitabiri kuzaliwa kwa Yohana mbatizaji na Yesu mapema. Lk 1:5-38

Mungu aliwatuma manabii wake kwa taifa la Israeli lakini watu walikataa kuzingatia maonyo yao.

A. Utangulizi.

- Je, umewahi mwambia mtu kitu ambacho hakutaka kusikia? Sio rahisi, sivyo?
- Je, umawahi onya mtu juu ya jambo ambalo uliona lingewasababishia maafa kama hawangetii maonyo?

B. Mungu alinena na mwanadamu tangu mwanzo.

- Mungu ndiye muumba wa kila mtu duniani.
- Anawapenda wanadamu na anataka kila mtu kila mahali akombolewe, kutoka kwa nguvu za shetani, dhambi na mauti, **2 Petero 3:9.**
- Kwa hivyo tangia mwanzo mungu amekuwa akiwaonya wanadamu, iliwaijua njia yake na mapenzi yake.
- Kumbuka jinsi Mungu alinena na Adamu, Hawa, Kaini na pia Nuhu. Alimpa Nuhu, ujumbe wake ili Nuhu awaambie watu wa nyakati zake kuwa Mungu amewaamuru kubadili nia zake na kumwamini yeye pekee yake.

C. Ujumbe wa manabii

- Pia Mungu alinena na Ibrahimu, Isaka na Yusufu. Alimpa ujumbe wake Musa na Musa akampa Farao na Waisraeli.
- Kumbuka pia kwamba Mungu alinena na taifa la Israeli na kuwapa amri zake kutoka kilele cha mlima Sinai.
- Baadaye Mungu alinena kupitia wajumbe wake waitwao manabii ambao aliwatuma kwa Waisraeli ili wawafunze njia zake na kuwaonya juu ya hukumu yake juu ya dhambi.
- Isaya, Yeremia, Hezekia na Danieli walikuwa baadhi ya manabii wa Bwana waliojulikana zaidi na Mungu aliwatumia kuaandika baadhi ya vitabu vya agano la kale.
- Manabii wa Mungu waliwaambia watu kutubu, kuharibu miungu yao na kumtumainia Mungu peke yake – **1 Wafalme 18:21**
- Walitakiwa kuamua ni nani wangemtumikia.
- Waliomwabudu Bwana wangefanya hivyo kutoka mioyoni mwao, na ibada yao ilitakiwa kufanywa kulingana na neno la Bwana **– Yohana 4:24**

- Manabii wa Mungu waliwakumbusha wana wa Israeli Sheria za Mungu walizopewa na Musa na Waisraeli walikuwa wamekosa kutii sheria hizo kwa kuendelea…**Yeremia 5:1-8,23,25,30,31.**
- Manabii waliwaambia watu kuwa Mungu amesema lazima watubu ama awaadhibu kwa hukumu.
- Angewatumia maadui zao kupigana nao.
- Maadui wao wangewashinda na kuwapeleka matekani katika nchi za kigeni, na Washami walikuwa baadhi ya madui zao.
- Mungu alimtuma Isaya kuwaonya makabila kumi ya Israeli.
- **Isaya 10:5,6 –** Mungu pia alimtumia Yeremia kuwaonya watu wa Yerusalemu na Yuda kwamba Mungu angewatuma raia wa Babiloni kuwaangamiza.
- **Yeremia 20:5** Tutaongea mengi kuhusu hii baadaye.
- Mungu hajabadilika.
- Yeye ndiye Mungu aishiye milele na wa kweli na atawaadhibu wote wanaoabudu na kutumikia miungu mingine.

D. Mungu hakusahau ahadi yake ya kumtuma mkombozi.

- Hata ingawa miaka maelfu ilikuwa imepita, tangu Mungu kupeana ahadi yake ya kwanza ya kumtuma mkombozi katika Bustani la Edeni, hakusahau kumtuma mkombozi ambaye angemwezesha mwanadamu kuwa rafiki wa Mungu tena.
- Kwa miaka hii yote, Mungu alirudiarudia kuwakumbusha Waisraeli kuhusu ahadi yake ya kumtuma mkombozi.
- Miaka mingi kabla ya mwokozi kuja humu duniani, Mungu alifunua mambo mengi kumhusu.
- Aliwaambia wajumbe wake wateule, manabii mambo ambayo yangetendeka kwa mkombozi.
- Waliandika mambo haya katika vitabu vyao ambavyo sasa hivi vimenakiliwa kwenye Biblia.
- Katika masomo yanayofuata, tutaangalia baadhi ya huu unabii na jinsi Mungu aliutimiza.
- Kumbuka kuwa anajua kila kitu kabla hakijatendeka.
- Jambo la kupendeza kwangu ni kuwa, Mungu hakuwachana na mpango wake wa kumtuma mkombozi hata ingawa watu wengi hawakupenda mapenzi yake wala ahadi zake.
- Mungu aliupenda ulimwengu na hakutaka mtu yeyote aangamie katika hukumu ya milele**. – Hezekieli 18:32 , 2 Petero 3:9**

E. Nia ya Israeli kumhusu Mungu; Manabii wake na ujumbe wao.

- Waisraeli walikuwemo mabaki waliomwamini Mungu na kuamini ujumbe wa manabii.
- Lakini wengi wao walikataa kumwamini.
- Waliwasaliti na kuwauwa wajumbe wa Mungu.
- Waliendelea kuabudu miungu.
- Walizifuata njia mbovu za mataifa jirani yaliyowazunguka.
- Wengi walienda hekaluni kumwabudu Mungu na kutoa dhabihu lakini hawakumwamini wala kumtii Mungu katika maisha yao.
- Walimwambia Mungu mambu mazuri lakini hakukubali walichosema kwa kuwa mioyoni mwao hawakumaanisha walichosema. **Isaya 29:13**
- Unajua, hatuwezi mdanganya Mungu?
- Mwanadamu huona nje tu na kusikia maneno pekee.
- Lakini Mungu hutazama mawazo ya mioyo yetu **– 1 Sam 16:7**
- Anajua jinsi tulivyo ndani mwetu. **– Isaya 64:4**
- Anasema sisi sote ni watenda dhambi**. – war 3:23**
- Hakuna yeyote hata mmoja ambaye anaweza kumpendeza mungu kwa kile anachofanya **– Waefeso 2:8-9 Tito 3:5**
- Hebu turudi kwa manabii.

- Kando na manabii waliotumwa na Mungu, kulikuwa na manabii wa uongo waliowaambia waisraeli uongo.
- Walijidai kuwa wajumbe wa Mungu lakini kwa hakika walikuwa watumishi wa shetani.
- Waliwaambia watu uongo.
- Waliwaambia watu kuwa kila kitu kilikuwa sawa na Mungu na hangewahukumu.
- **Yeremia 6:13,14, Yeremia 8:11, Hezekieli 13:10, 2 Tim 4:3,4**
- Shetani bado anafanya hivyo hata leo hii. Anaendelea kuwatumia watu wanaosema kuwa neno la Mungu si kweli ama kusema kuwa Mungu hatawahukumu watu. Wengi wanahubiri kuwa hakuna hukumu ya milele na kuwa Mungu hatamtuma mtu yeyote kuzimu.Wanaweza kutueleza kuwa kila kitu ki sawa. Kila mtu anaenda kuwa na Amani na mwingine na sote tunakuwa jamii moja ya furaha.
- Huu ni uongo tu wa shetani mwenyewe. Nataka kusema hivi, wote wanaokataa kumwamini Bwana na wakuje kwake kupitia njia yake watahukumiwa milele katika ziwa la moto. Mungu anasema hakuna Amani kwa mwenye dhambi **– Isaya 57:20-21.**

F. Hukumu ya Mungu juu ya Israeli na Yuda.

- Mungu ni mvumilivu.
- Yeye hatahukumu tu watenda dhambi haraka.
- **Mhubiri 8:11**
- Mfano mzuri wa hii ni katika siku za Nuhu. kwa miaka 120 kabla ya ghariga kuja na kuwaangamiza. Mfano mwingine ni utumwa wa Washami na Babiloni ambao tulisoma mwanzo.
- Kwa miaka mingi Mungu aliwatuma wajumbe kwa taifa la Israeli.
- Walionya waisraeli juu ya hukumu yao kama hawangetubu.
- Lakini Waisraeli hawakuamini kuwa Mungu angewaruhusu maadui zao kuchukuwa nchi yao na kuwafanya watumwa.
- **2 Wafalme 17:1-8 –** Washami waliwaleta watu wengine na wakaishi kasikazini mwa nchi ya Israeli.
- Hawa watu waliabudu miungu.
- Hawakumjua Mungu aishiye milele na wa kweli wa Israeli.
- Wengi wa wana wa Israeli kutoka makabila kumi ambao hawakuenda Ushami walioana na hawa watu waliotoka mataifa mengine.
- Uzao wa hawa watu uliitwa wasamaria.
- Wasamaria waliendelea kumwabudu Mungu ila sio kwa njia yake aliyompa Musa ila kwa njia zao wenyewe.
- Zaidi ya hayo walikataa kwenda katika hekalu la Mungu Yerusalemu **– yohana 4:20-22**
- Kwa sababu hii, Mungu hakukubali Ibaada yao.
- Yuda, iliyojumuisha kabila mbili za kusini mwa Israeli na watu wa Yerusalemu,pia walikataa kutubu, kwa hiyo Mungu aliwaruhusu Wababiloni kuwachukuwa mateka katika nchi yao **– 2 Mambo ya nyakati 36:15-20.**
- Wababiloni waliangusha kuta za Yerusalemi, **katika mstari wa 19**
- Pia waliharibu na kulichoma hekalu la Yerusalemu ambalo Suleimani alimjengea Bwana.
- Mungu alitekeleza kile alichoahidi kingetendeka kama Israeli hawangetubu.
- Kwa kuwa watu hawakuliamini neno lake, Aliwahukumu.
- Wote wasioamini watahukumiwa na Mungu milele.

G. Kurejea kwa mateka kutoka Babiloni.

- Baada ya miaka mingi, watu wa Yuda waliokuwa Babiloni walitubu na kumlilia Mungu awarejeshe katika nchi yao.
- Bwana alisikia kilio chao na akawarejesha wengi wao Yerusalemu.

- Wakajenga tena Yerusalemu na kuta za mawe kuzunguka mji. (Ezera na Nehemia)
- Wakalijenga tena hekalu.
- Kutoamini kwa Israeli na kukataa ahadi za Bwana kulilelata uchungu na majuto kwa Bwana. **Zab 81:13,14-16**
- Mungu alikasirishwa na Israeli lakini hakubadili wala kusahau ahadi zake.

Mungu alibashiri kuzaliwa kwa Yohana na Yesu. .

A. Utangulizi.

- Nabii wa mwisho kunena ujumbe wa mwisho wa Mungu katika agano la kale alikuwa Malaki.
- Malaki alikumbusha wayahudi kuwa mkombozi ambaye Mungu aliahidi atakuja kuwaokoa.
- Aliwaambia kuwa, kabla ya mkombozi kuja Mungu atatuma nabii mwingine**. Malaki 3:1-**
- Kazi ya huyu nabii itakuwa kuwafunza watu na kuwaandaa kwa kuja kwa mwokozi.
- Baada ya Malaki hata hivyo, miaka mia nne ilipita ambapo Mungu hakunena kupitia kwa nabii yeyote.(Hii inaitwa miaka ya unyamafu)
- Hata hivyo hiyo miaka ya kunyamaza kwa Mungu kwa njia ya polepole Mungu alikuwa anaandaa kutimia kwa ahadi zake kuu za kumtuma mwokozi kwa ulimwengu wote.
- Alifanya lugha ya Kiyunani kutumika katika sehemu nyingi za ulimwengu, akaunganisha miji ya mbali na Roma. Akawatawanya watu wake katika sehemu nyingi za mataifa walikojenga masinagogi na kufunza neno lake.
- Lakini hatimaye wakati ulikuwa umefika.
- Mungu alikuwa tayari kutimiza alichoahidi katika Bustani la Edeni kumtuma mkombozi. **Mwanzo 3:15**
- Sasa tunaenda kuanza mafundisho yetu katika agano jipya na hadithi ya wanandoa wa kiyahudi wakongwe walioamini Mungu na walikuwa wakingojea kutimia kwa ahadi zake.

B. Mungu aliahidi Zakaria na Elisabeti watapata mwana

- **Lk 1:5-6 –** Zakaria na mkewe Elisabeti walikuwa wayahudi walioamini Mungu na neno lake.
- Walitoa dhabihu katika hekalu jinsi Mungu alivyoamuru Musa.
- Kwa sababu walikuwa wamemtegemea Mungu na kumwendea kwa njia aliyowaambia, Mungu aliwakubali jinsi alivyokubali Habili na wengine waliomtegemea Mungu kuanzia mwanzo wa ulimwengu.
- Zakaria na Elisabeti walikuwa wazee na hawakuwa wamepata mtoto yeyote.**Lk 1:7 –**
- Zakaria alikuwa mmoja wa makuhani katika hekalu la Yerusalemu**. Lk 1:8-10.**
- Sikiliza kilichofanyika kwa Zakaria alipokuwa akifanya kazi yake ya ukuhani katika hekalu.

C. Yohana alipewa kazi ya kuenda kumwandalia mkombozi njia.

- **Lk 1:11-17 –** Bwana alijua yote kuhusu mwana wa Zakaria kabla Elisabeti hajashika mimba.
- Pia ni jambo la kupendeza kuwa Mungu alitujua hata kabla ya wazazi wetu kujua tutazaliwa**. Zab 139:13-16**
- Kumbuka Mungu alikuwa amebashiri kuwa mwana wa Zakaria, Yohana, ataenda mbele ya mkombozi kumwandalia njia.
- **Lk 1:16 –** Malaika alimwita mkombozi anayekuja kama Bwana Mungu wao. Kile anachosema hapa ni kuwa mkombozi anayekuja, Mwokozi wa wanadamu atakuwa Mungu mwenyewe.
- **Lk 1:24-25 –** anamaanisha nini akisema, kuniondolea aibu yangu?
- Siku hizo Wayahudi waliwadharau wanandoa ambao hawakuwa na mtoto, Zakaria na Elisabeti walikuwa wanaenda kumpata mtoto kwa umri wao wa uzee.
- Kwa hivyo hawangedharauliwa tena.

D. Mungu aliahidi Mariamu mwana wa kiume.

- Wakati wa Mungu kutimiza ahadi zake ulikuwa umefika, wa kumleta mkombozi.
- Kwa hivyo Mungu alimtuma malaika kumwambia bikira (sio asiye na dhambi, bali bikira tu) aliyeitwa Maria ya kwamba Mungu alikuwa amemchagua kuwa mama wa mkombozi.
- Maria alikuwa tu msichana wa kawaida ambaye pia alikuwa mwenye dhambi aliyemwamini Mungu kuleta mkombozi. **War 3:23**
- **Lk 1:46-47 –** Maria hakuwa bila dhambi. Pia alimhitaji mwokozi.
- Mungu alikuwa amemchagua Maria kuwa mama wa mwokozi kwa kuwa Mungu hufanya chochote anachotaka kukifanya**.Zab 115:3**
- Hamuulizi mtu yeyote wala hataki jibu kwa mtu kwa kuwa yeye ni Mungu mwenye enzi yote na mwenye uweza na hupatikana kila mahali kila wakati.
- Na hivyo tunasoma katika **Lk 1:26-31** – mwana wa Maria alikuwa mkombozi mtarajiwa na kungojwa na jina lake lilikuwa Yesu ambalo lina maana ya mwokozi/mkombozi.
- Unajua miaka mingi ilikuwa imepita lakini Mungu hakuwa amesahau ahadi yake ya kutuma mkombozi.
- Anapenda ulimwengu wote na angependa wenye dhambi wote wakombolewe na hukumu yote wanayostahili kupata.**Yohana 3:16**

E. Mwana wa Maria atakuwa mwanadamu na pia Mwana wa Mungu.

- Malaika Gabrieli pia alimwambia Maria mambo ya kushangaza ya baadaye kumhusu mwanawe.
- **Lk 1:32-** mwana wa Maria hatakuwa tu mwanawe bali pia atakuwa mwana wa Mungu.
- Inashangaza kufikiri kuwa miaka mia sita ilikuwa imepita Mungu alipotangazia nabii Isaya haya mambo.
- **Isaya 9:6 –** tulipoanza kujifunza Biblia pamoja tulijifunza kuwa ingawa tuko na Mungu mmoja ambaye yuko katika utatu ambao ni sawa katika kila njia. Hawa watatu ambao ni Mungu mmoja ni Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu. Sasa, Mungu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, hawakuwa na mwili kama jinsi sisi wanadamu tuko nao, hata hivyo Mwokozi alitakikana kuwa na mwili kama vile tulivyo. Pia alifaa kuwa bila dhambi ili akubalilke mbele za Mungu. Waja tupeane wazo kwa hii. Ili mpango wa Mungu kumhusu mwokozi utimie, Mungu mwana ilikuwa azaliwe kama mwanadamu, na huyu mwokozi ambaye ni Mungu mwana, ilifaa kushuka kutoka mbinguni azaliwe duniani kama mwana wa Maria. Kwa hivyo mwana wa Maria alikuwa mwanadamu na pia Mungu katika mwili mmoja.
- Huyu mwana, Yesu alikuwa mwanadamu kamili na pia Mungu kamili.(Tazama tena katika **Isaya 9:6)**
- Tena malaika alimwambia Maria kuwa kwa sababu Mkombozi atatoka kizazi cha Daudi mfalme, atakuwa mfalme juu ya Israeli**. Isaya 9:7**
- Wacha tuangalie nyuma katika **Luka 1** tena**. Lk 1:32b,33 –** Mungu alikuwa anaenda kufanya kile alichoahidi mfalme Daudi. Tunaweza mtumaini yeye anayetimiza ahadi zake**. 2 Sam 7:12-17**

F. Yesu Mkombozi hatakuwa na Baba wa kimwili.

- **Lk 1:34 –** Maria hakuelewa jinsi atakavyopata mtoto ambaye hatakuwa na baba wa kimwili.
- **Lk 1:35 –** Malaika alisema kuwa Mungu Roho Mtakatifu ndiye atakayefanya huu muujiza, ambayo ni muhumu hapa. Kumbuka nyuma katika kitabu cha mwanzo, tuligundua kuwa kwa sababu sisi wote ni watoto wa Adamu, sisi wote tulizaliwa wenye dhambi. Fahamu kuwa mwanaume ndiye hubeba mbegu. Lakini **Mwanzo 3:15 -** kama Yesu angezaliwa na baba wa kimwili angezaliwa mwenye dhambi.
- Wacha niseme hivi: kila mtu ambaye amezaliwaye katika ulimwengu huu amerithi dhambi ya Adamu.

- Sisi sote ni wenye dhambi kwa sababu dhambi ya Adamu ambaye ni baba ya wanadamu wote ilikuja kwetu kutoka kwake.
- Lakini baba ya Yesu alikuwa Mungu.
- Mungu ni mkamilifu na mtakatifu, bila dhambi
- Yesu hakurithi dhambi ya Adamu.
- Alikuwa mwana mkamilifu wa Mungu, mtakatifu na bila dhambi.
- Tukirudi sasa kwa Elisabeti **Lk 1:36-37**
- Ilikuwa haiwezekani bikira kupata mtoto, jinsi ilivyokuwa haiwezekani kwa Elisabeti mama wa Yohana mbatizaji kupata mtoto katika umri wake wa uzee. Lakini kwa Mungu hakuna lisilowezekana.
- Mungu hushughulikia mambo yasiyowezekana.
- Inaonekana Maria aliposikia kuwa Elisabeti alikuwa ameshika mimba katika umri wake wa uzee, ilimtia moyo. Sikiza vile alivyoitikia.
- **Lk 1:38 –** Maria alimtumaini Bwana na kukubali kuona ilikuwa mapenzi ya Mungu kwake kuwa mama ya mwokozi.

G. Hitimisho.

- Mungu anapoahidi kitu, hutimiza.
- Hata ikuwe ngumu namna gani, hata ionekane haiwezekani, atatimiza.
- Hata ikichukuwa maelfu ya miaka ataitimiza.
- Mungu atatimiza kila ahadi mpaka jambo ya mwisho.

SOMO LA 16

Mungu alianza kutimiza ahadi zake kuhusu Yohana na Yesu – Mat 1:1-2; Luk 1:57 na 67-80.

Mungu alitimiza ahadi zake kwa kupeana Yesu, mkombozi, – Mat 1:18 – 25; 2:1-15, 19-23, Luka 2:40,52.

Mungu alianza kutimiza ahadi zake kumhusu Yohana na Yesu.

A. Yohana alizaliwa.

- **Luka 1:57** – Mungu alitekeleza alichokuwa ameahidi.
- Zakaria na mkewe Elisabeti walikuwa na mwana na walimuita jina Yohana, kama tu walivyoelekeshwa na malaika.

B. Zakaria aliamini kuwa ahadi za Mungu kuhusu mkombozi zilikuwa karibu kutimia.

- **Luka 1:67-69.**

C. Yohana alikuwa awaandae Waisraeli kumwamini Mkombozi.

- **Luka 1:76-77** – Mkombozi, Mwokozi, ambaye ilikuwa atengenezewe njia na Yohana alikuwa awe Mungu mwenyewe.
- Hakuna mwanadamu wa kawaida ambaye angetukumboa kutoka kwa shetani , dhambi na mauti. Bwana ndiye mkombozi mkuu kwa wote wanaomtumainia.
- Nani aliyemkomboa Nuhu na familia yake kutokana na gharika? Nani aliyemwokoa Isaka kutoka kwa kifo na kupeana kondoo kufa kwa niaba yake? Nani aliyemwokoa Lutu kutokana na maangamizi ya Sodoma na Gomora? Nani aliyemwokoa Yusufu kutoka kwa gereza la Misri? Nani aliyewaokoa Waisraeli kutoka kwa utumwa Misri? Nani aliyewaokoa Waisraeli kutoka kwa jeshi la Farao pale bahari ya Shama? Nani aliyewaokoa Waisraeli kutoka kwa kifo kwa kuwapa maji na chakula jangwani**?**
- Mungu pekee ndiye Mkombozi mkuu.
- Hakuna mwokozi mwingine ila tu ni yeye.
- **Isaya 43:11**
- **Luka 1:78, 79** – Mkombozi angekuja Kama jua litokeleazapo asubuhi.
- Tafakari hili kwa muda: Tungejihisi aje kama tungeenda matembezi msituni na tupotelee huko? Jua lilipotua, hatungepotea tu bali hata hatungejua mahali tulipo pia !
- Kwa njia ile ile, dhambi ya Adamu na Hawa ilituweka sisi sote gizani.
- Walipotenda dhambi, dhambi zao ziliwatenga na Mungu. Walifukuzwa kutoka bustani la Edeni. Sasa waliingia gizani na katika hatari ya mashambulizi ya Shetani.
- Wanawo na kizazi chao, ikiwemo wewe na mimi tulizaliwa katika giza la dhambi.
- Lakini Mungu alikuwa anaandaa njia ya kutoka humo gizani!
- Zakaria alisema kuwa mkombozi atakuja tu kama jua lichomozapo baada ya usiku wa giza totoro na kupeana nuru kwa kila mtu, kila mahali.

- Hebu tutafakari juu yah ii: Ni jua ngapi hupeana nuru kwa dunia hii? Moja tu. Jua hiyo hiyo ndio hupeana nuru kwa dunia nzima.
- Ni wakombozi wangapi ambao Mungu aliahidi kuwatuma ulimwenguni? Mmoja tu.
- Mungu hakuahidi kutuma wakombozi tofauti ulimwenguni, mmoja kwetu na mwingine kwa watu wa sehemu zingine za ulimwengu. **Matendo 4:12; Warumi 3:29,30**
- Mungu aliahidi tu mkombozi mmoja ambaye angetuwezesha sisi kumsongea/kurejeshwa kwa Mungu.
- Angeleta "**nuru**" kwa dunia nzima, kama jua lichomozapo!
- Kwa miongo za miaka, Mungu aliwapa manabii ujumbe wa mkombozi mtarajiwa. Alipanga vyote ambavyo vingetendeka kwake kabla ya yeye kuja duniani**. Isaya 9:6,7**
- Yesu , mkombozi mtarajiwa , ilikuwa awe wa kizazi cha Ibrahimu , Isaka , Yakobo na Daudi.
- Mungu alikuwa amewaahidi kuwa, mkombozi atakuwa wa uzao wao.

D.Mungu alitimiza ahadi zake kuhusu Yesu, Mkombozi.

- **Mathayo 1:1,2,6**
- Hii ni kutimizika kwa ahadi za Mungu kwa Daudi na pia kutimizika kwa maneno ambayo Mungu alinena kwa Isaya .
- Mkombozi; Mwokozi; Yesu Kristo.
- Historia yote ni "hadithi yake" .
- Umewahi gundua ya kwamba kila mara tuandikapo tarehe tunanakili kuzaliwa kwa Yesu Kristo?
- **"1997 AD**" inamaanisha **1997**, **Anno Domini** , "**mwaka wa Bwana wetu**".
- Kila tarehe kihistoria huandikwa , **BC (kabla ya Kristo)** na **AD (baada ya Kristo)**
- Yesu ni mtazamo wa kihistoria.
- Sasa kumbuka malaika Gabrieli akimjia binti bikira mdogo aliyeitwa Mariamu akimtabiria kuwa atakuwa mama wa Yesu .Hata hivyo,
- Alikuwa tayari amekwisha ahidi kuolewa kwa mwanamume , Yusufu.
- Sasa Yusufu aligundua kuwa Mariamu alikuwa mja mzito na alijua ya kwamba yeye si baba wa mtoto yule.
- Kulingana na sheria ya kiyahudi, Yusufu angefanya tangazia la adharani, na Mariamu angeuawa kwa kupata mimba ya mwana ambaye hakuwa wa Yusufu. – **Kumb 22:20, 21**
- Lakini Yusufu alimpenda Mariamu, kwa hivyo aliamua kumuacha kisiri.

Mungu alitimiza ahadi zake kwa kupeana Yesu Mkombozi. .

A. Shida ya Yusufu.

- **Mathayo 1:18-19 –** Wazo la kufurahisha hapa latoka katika **Mithali 16:1,9**
- Mungu hakuwa anamwachilia Yusufu amuache Mariamu.
- Alikuwa mtu mwema aliyemtumainia Mungu.
- Naam, alikuwa mtenda dhambi, lakini alimjia Mungu jinsi ilivyompasa kama tu alivyoambiwa na Mungu. (Kutubu dhambi na kutoa dhabihu ya wanyama na kumtumainia Mungu).
- Mungu alitaka Yusufu kumuchukuwa Mariamu kama mkewe ili Yesu awe na baba mzuri wa kidunia.

B. Malaika wa Mungu anatumwa kumwelezea Yusufu.

- Kwa sababu hii, Mungu alimtuma malaika wake kumwambia Yusufu ukweli kumhusu Mariamu.
- **Mathayo 1:20-23** – Manabii walikuwa wamesema kuwa mwokozi atazaliwa kwa bikira.
- Unabii wa Agano la Kale **Isaya 7:14** – ulitimiza **Mathayo 1:18**.
- Wacha tutafakari juu yah ii: **Yesu Kristo ni Mungu**. **Mathayo 1:23**
- Yesu ndiye mkombozi wa pekee na pia ni Mungu! **Yoh 10:30,38; 12:45; 14:7-10; 17:9,10**

- Kumbuka ya kwamba Mungu ni utatu wa nafsi tatu. Mungu Baba, Mungu Mwana, Mungu Roho Mtakatifu.
- Sasa fikiria! Mungu mwenye alikuwa anakuja duniani kama kitoto kichanga.

C. Mwitikio wa Yusufu

- **Mathayo 1:24-25 –** Yusufu alimwamini Mungu na akamuchukuwa Mariamu nyumbani kwake kama mke wake.
- Tunasoma maneno haya lakini ni vigumu kutambua ugumu walioupitia hawa wana ndoa.
- Wajua, yote ni kuhusu imani na tumaini. **Waebrania 11:6; 10:38; Yohana 6:28-29**
- Maandiko ya kufutia kuhusu huu mtembeo wa imani- **Mathayo8:13; 9:27-29; Warumi 5:2; 2Mambo ya nyakati 20:20.**

D. Kristo Bwana amezaliwa!

- **Luka 2:1-7** – Yusufu na Mariamu waliishi Nazareti, lakini maandiko yalitabiri kuwa mkombozi atazaliwa Bethelehemu (**Mika 5:2**). Mungu alitumia Kaisari kuhakikisha kuwa Mariamu na Yusufu wanapatikana Bethelehemu wakati wa kuzaliwa kwa Yesu.
- **Luka 2:8-20** – Wachungaji wanamwabudu mfalme ambaye amezaliwa. Ni ya kushangaza kunukuu unyenyekevu wa Bwana wetu. Hakuchagua jumba cha kuzaliwa ndani wala kufunulia wenye nguvu na walio wakuu kuzaliwa kwake bali ni kwa wachungaji wa chini. (**Wafilipi 2:4-11** inatufunulia ya kuwa unyenyekevu na utiifu wa yesu kwa Mungu Baba yake ulimfanya kuinuliwa juu ya wote milele.)

E. Mamajuzi walimtafuta Yesu.

- **Mat 2:1-2 –**Yesu alizaliwa Bethelehemu kama vile manabii wa Mungu walivyotabiri miaka mingi kabla. **Mika5:2 –** inatimia - **Mat 2**:**1**
- **Mat 2:2,3,8,16** –Angalia sababu Mamajuzi walisafiri kutoka mbali: Kumwabudu yule aliyezaliwa mfalme wa Wayahudi. Tofauti kwa mtikio wao kwa kuzaliwa kwa Yesu na mwitikio wa mfalme Herodi.

F. Hofu ya Mfalme Herodi

- **Mat 2:3,4** - Herodi, kama ilivyokuwa na Farao mfalme wa Misri wakati wa Musa, hakutaka mtu yeyote kuwa mfalme juu yake.
- Herodi aliogopa kuwa angepoteza nafasi yake ya kifalme wakati mtoto yule angekua mkubwa. **Mat 2:5-6**

G.Onyo ya Mungu kwa Mamajuzi na Yusufu

- **Mat 2:7-15** - Awe Herodi au nguvu zozote kule mbinguni au duniani, hazingemzuia Mungu kutekeleza mpango wake na kumuokoa mwanadamu kutokana na dhambi.
- Yesu alipelekwa Misri kama vile manabii walivyonena mbeleni kabla.
- **Hosea 11:1** inatimizwa **Mat 2:14-15.**
- Wakati Herodi alikufa, Bwana alimtuma mmoja wa malaika wake kumwambia Yusufu kumrudisha Mariamu na Yesu katika nchi yao ya Israeli kutoka Misri.

H.Yusufu, Mariamu, na Yesu walirudi Nazareti

- **Mat 2:19-23** –Tena, neno la Mungu lililopeanwa kwa manabii lilitimia.
- Mkombozi aliishi katika nchi ya Nazareti.

I. Yesu, kijana katika Nazareti.

- **Luka 2:40** – Yesu alikua kutoka utotoni na akawa kijana.
- Babake, Mungu, alimlinda na kumwongoza katika jambo alilolitenda, kufikiria na kuongea.
- Alitii kila amri ya Mungu.
- Hakutenda dhambi kwa sababu hakuzaliwa mwenye dhambi.

J. Yesu alikua akawa mtu mzima.

- **Luka 2:52 –** Yesu Kristo , ambaye alikuwa Mungu alzaliwa katika hii dunia kama mwanadamu, katika mwili wa kibinadamu, ili awe Mkombozi, Mwokozi, wa wanadamu!
- Katika kukua kwake katika umbo lake la kibinadamu, alikuwa na hekima. Mungu alipendezwa naye na watu walimpenda.
- Tabia zake kama mwanadamu zilikuwa haswa tabia za Mungu.
- Alikuwa bila dhambi na mtakatifu.
- Alitenda kulingana na Neno Lake.
- Alikuwa kikamilifu mwenye haki.
- Maarifa yake yalikuwa kamilifu.
- Alikuwa mwenye rehema na neema , wa upendo na mwema.
- Ndiyo sababu Yesu alipata kibali mbele za Mungu na wanadamu….. **Isaya 11:1-5.**

SOMO LA 17

Mungu alimtuma Yohana kufunza na kubatiza; Yohana alimbatiza Yesu - Mat 3:1-9 na 13-17; Yoh 1:24-27 na 29-37

Yesu alipojaribiwa alimpinga shetani - Mat 4:1-11

Mungu alimtuma Yohana kufunza na kubatiza; Yohana alimbatiza Yesu.

A. Utangulizi.

- Wacha turejelee nyuma sasa; kumbuka Yohana aliyechaguliwa na Mungu kuwa nabii na kuwaandaa Wayahudi kumpokea Mkombozi. Alikuwa sasa amekomaa.
- Ilikuwa sasa ni wakati wake wa Mungu wa kuanza kuwafunza watu.

B.Yohana alikuwa mjumbe wa Mungu kwa Israeli.

- **Mat 3:1-2 –** Yohana aliwafunza watu kuwa ni lazima watubu.
- Yohana alimaanisha kuwa watu lazima wabadili nia zao kuwahusu wenyewe na kuhusu dhambi na wamwelekee Mungu.
- Aliwaambia kubadilisha mawazo yao wakijiandaa kumpokea mwokozi anaye kuja.
- Unakumbuka tukisoma amri kumi? Ni wangapi wameweza kutekeleza amri hizo kikamilifu?
- Hapa kuna kifungu cha kupendeza- **Yakobo 2:10.**

C. Yohana alikuwa masikini

- **Mat 3:4** –Yohana alikuwa maskini. Alikula vitu alivyopata nyikani na mavazi yake yalikuwa ya mtu maskini.
- Watu wengine husema kuwa, ukiweka Imani yako ndani ya Mungu atakupa pesa yote na vyote unavyotaka. Wanasema mali na milki ni ishara ya baraka za Mungu. Hata wanaweza sema kuwa kama hupati pesa yote na vyote unavyo hitaji, huenda hauna imani ya kutosha.
- Lakini Mungu haahidi kuwa mtu atakuwa tajiri anapomwamini. Wengi wa manabii wakuu wa Mungu na watu walioamini walikuwa maskini. Baadaye tutaona kuwa hata Yesu, mwana wa Mungu, alikuwa mtu maskini alipokuwa hapa duniani.

D. Watu wengi waliamini ujumbe wa Mungu kupitia kwa Yohana .

- **Mat 3:5-6** –Wayahudi wengi waliamini neno la Mungu ambalo Yohana aliwaambia na hata wakamuendea awabatize.
- Ubatizo wao ulikuwa ni tendo la nje, ambalo liliashiria toba yao ya ndani na imani katika ujumbe wa Yohana. Walikuwa wanajitambulisha na ukweli ambayo Mungu alikuwa anawapa kupitia kwa Yohana.
- Ubatizo hautatufanya sisi tukubalike kwa Mungu.
- Hata ubatizo hautatuosha dhambi zetu machoni pa Mungu. Kubatizwa si malipo kwa Mungu kwa ajili ya dhambi zetu. Malipo ya dhambi ni mauti. Ubatizo ni ishara tu ya kuonyesha wengine kuwa unakubaliana na ujumbe wa Mungu na kumtumainia tu Mungu kukuokoa.

E. Maneno la Yohana kwa wenye kiburi na wasio tubu.

- **Mat 3:7 –** Viongozi wengi wa hekalu walikuwa na kiburi.
- Wacha tuwatazame hawa viongozi na kuzingatie kile Biblia inatuelezea kuwahusu.

Waandishi

- Yote ambayo Musa na manabii waliandika ilikuwa sasa imenakiliwa kwa viuo. Watu walionakili maneno ya Mungu kwenye viuo waliitwa waandishi. Pia waliita "**wanasheria"** au **"walimu wa sheria "** Kwa sababu walikuwa ni watu waliostahili kujua na kuweza kueleza kikamilifu ,maana ya maneno ya Mungu**.**
- Waandishi wengi walikuwa na majivuno sana kwa sababu ya usomi wao. Walifikiria kuwa wanampendeza Mungu kwa kuwa walikumbuka na kuelezea kwa ufasaha maana ya sehemu nyingi ya Neno la Mungu. Hawakufahamu kuwa ni ya muhimu zaidi kwa Mungu kama wangeamini na kutii neno lake.

Mafarisayo

- Viongozi wengine wa Wayahudi waliitwa Mafarisayo**.** Mafarisayo walijaribu kumpendeza Mungu ili wakaweze kukubalika na yeye kwa kutii sheria nyingi walizo nakili wenyewe. Mafarisayo waliongezea kwa neno la Mungu.
- Hawakufikiria kuwa walikuwa tu watenda dhambi kama watu wengine. Walijitenga na watu wengine wasiokuwa Mafarisayo. Walikuwa wema wa kutosha kukubalika na Mungu kwa sababu ya mambo yote walikuwa wakitenda.

Masedukayo

- Masedukayo pia walienda hekaluni na kudai kuwa wanamwabudu Mungu. Hata hivyo, hawakuamini vitu vingi ambavyo Mungu alikuwa ameandika kwenye Neno lake. Masedukayo waliondoa ukweli mwingine kutoka kwa neno la Mungu.
- Kwa mfano, Masedukayo hawakuamini kuwa malaika wapo, wala hawakuamini katika ufufuo wa wafu. Walikataa kila kitu isipokuwa vitabu vitano vya kwanza, kuanzia Mwanzo hadi Kumbukumbu la Torati.
- Haja yao ilikuwa kuwa na msimamo bora wa kiserikali ya Warumi na kuhakikisha kuwa wanasalia kuwa viongozi wa Wayahudi. Ukweli ni kwamba hawakumwamini Mungu kutoka mioyoni mwao.
- Wengi wa viongozi hawa hawakukubali kuwa walikuwa wenye dhambi.
- Walifikiria kuwa walikuwa wazuri wa kukubalika na Mungu.
- Kwa sababu Masedukayo na Mafarisayo walikuwa na majivuno/kiburi, maneno la Yohana kwao yalikuwa yenye nguvu.
- Neno la Mungu ni lenye nguvu kwa wote walio na kiburi, na wanao mpinga na kukataa kusikiza ujumbe wake. **Mithali 16:5.**
- **Yakobo 4:6 –** inasema, "… Mungu huwapinga wenye kiburi…. "
- Mungu yu kinyume na wote wenye kiburi ambao hawakubaliani naye.
- Lakini anaahidi kuwasaidia na kuwakomboa wale wanaokubali kuwa ni wenye dhambi na wanao kubali kuwa ni yeye tu anaweza kuwasaidia.
- **Mat 3:8 –** Yohana aliwaambia Masedukayo na Mafarisayo kuwa, kama kweli walikubali mawazo ya Mungu kuwahusu, jinsi ilivyonenwa kupitia kwa Yohana, basi ni lazima waionyeshe kwa matendo yao.
- **Mat 3:9 –** Wayahudi wengi walijisifu kuwa Ibrahimu alikuwa baba wa taifa lao.
- Walifikiria kuwa Mungu atawakubali kwa kuwa wao ni uzao wa Ibrahimu.
- Mungu hamkubali yeyote kwa misingi ya wazazi wake ama kanisa analoshiriki. Mungu humuhukumu kila mtu kibinafsi, sio kwa ajili ya familia yake, au matendo yake, au kanisa lake.

F. Kile Yohana alisema kumhusu Mkombozi.

- **Yoh 1:24-27 –** Nyuma kwa wakati wa Yohana, watu wa tabaka la juu walikuwa na watumishi wao waliowafanyia kazi yao yote. Mtu wa mhimu hangevaa wala kukitoa kiatu mwenyewe. Hiyo ilikuwa kazi ya watumishi. Yohana alisema kuwa hata hastahili kuwa mtumishi wa kumtoa mkombozi viatu. Mkombozi alikuwa Mwana wa Mungu. Alikuwa muumba wa dunia – aliyekuwa Amempa Yohana uzima.

G. Yohana alimbatiza Yesu.

- Katika **Luka 3:23 –** Tunasoma kuwa Yesu sasa alikuwa ametimia miaka karibu thelathini.

H. Kile Mungu alisema kumhusu Yesu.

- **Mat 3:13-16 –** Ijapokuwa Yesu alikuja abatizwe, sio kwamba alikuwa mtenda dhambi aliyehitaji mwokozi kama wale wote waliobatizwa na Yohana.
- Yesu alizaliwa mkamilifu.
- Aliishi katika makubaliano makamilifu na Mungu.
- Yesu alikuja ubatizwe kwa sababu ilikuwa amri ya Mungu kwa Wayahudi wote waliomkubali Yohana kama nabii wa Mungu.
- Kama Yesu hangebatizwa watu wangefikiri kuwa hakutii amri ya Mungu.
- Ama watu wangechukulia kuwa Yesu hakuamini kuwa Yohana hakuamrishwa na Mungu kubatiza.
- Tazama tena **msitari wa 16** – Roho Mtakatifu alikuja kuwa na Yesu ili kumwezesha kutenda yote ambayo Mungu Baba alikuwa amepanga.
- Kumbuka Yesu alikuwa Mungu mwenyewe, lakini alipokuja kama mwanadamu, alichagua kumtegemea Mungu Roho Mtakatifu kwa nguvu za kutekeleza kazi ya ukombozi humu duniani.
- **Mat 3:17** - Tazama Mungu Baba alimwita Yesu mwanawe. Yesu alikuwa mwanadamu, lakini pia alikuwa Mungu Mwana aliyekuja duniani kutoka mbinguni na Mungu aliridhika naye.

I. Yesu, Mwana-kondoo wa Mungu.

- **Yohana 1:29** – Wakati Yohana alimwona Yesu, alisema kuwa Yesu ni mwana-kondoo wa Mungu, aliyetumwa duniani na Mungu.
- **Yohana alijua kuwa Yesu ndiye Mkombozi aliyeahidiwa.**
- **Yoh 1:30-37** – Yohana mwanzoni hakujua Mkombozi atakuwa ni nani, lakini alipoona ishara hii kutoka kwa Mungu, alikuwa na uhakika kuwa Yesu ndiye Mwokozi wa ulimwengu.

J. Hitimisho.

- Je na sisi? Je, tunahitaji ishara kutudhibitishia kuwa Yesu ndiye Mkombozi?
- Hatuona ishara kama hizi wakati huu, kwa sababu Mungu ametupatia Biblia ili tuweze kujua ukweli.
- Kitu kingine cha kuzingatia…. Je, sisi tuko kama viongozi wa kidini waliofikiri kuwa kazi yao nzuri, na misingi yao ya kidini ,illikuwa kamilifu kuwafanya wakubalike na Mungu?
- Waja niseme kwamba: Kila mmoja wetu anahitaji Mwokozi.
- Na Mungu amepeana Mwokozi mmoja tu: Yesu Kristo, mwana-kondoo wa Mungu.
- Ndiye Mwokozi wa pekee kwa dunia nzima, na ni Mwokozi wa pekee wako na wangu.

Yesu, alipojaribiwa, alimpinga Shetani. .

A. Shetani alimjaribu Yesu.

- **Mat 4:1 –** Mwanzoni, Shetani alikuwa nani?
- Kumbuka Mungu alimuumba Lusifa kikamilifu.
- Lakini Lusifa (aitwaye ibilisi au shetani) aliamua kumuasi Mungu hapo mwanzoni. **Ezekieli 28:15,17; Isaya 14:13,14**
- Tangu hapo, shetani ameendelea kuwa muovu .**Yoh 8:44**
- Shetani alimjaribu Adamu ili amuasi Mungu.
- Sasa alikuwa anamjaribu Yesu ili amuasi Mungu. Kwa nini? Alitaka kumweka Yesu chini ya utawala wake ili asiwe Mkombozi wetu.

B. Jaribio la kwanza.

- **Mat 4:2-** Ijapokuwa Yesu alikuwa Mungu, pia alikuwa mwanadamu. Katika ubinadamu wake alihisi njaa.
- **Mat 4:3 –** Tazama nyuma katika **3:17.**
- Shetani alikuwa anajaribu Yesu ahakikishe kuwa alikuwa mwana wa Mungu, kwa hivyo alimuuliza Yesu kutenda jambo ambalo Mungu Baba hakuwa amemwarifu kulitenda. **Yoh 8:28,29**
- **Mat 4:4** Tunahitaji chakula ili miili yetu iwe hai, lakini Mungu anasema kuwa kuna kitu kikuu zaidi cha muhimu kuliko chakula.
- Tunahitaji Neno la Mungu kutuongoza kwa njia ya uzima wa milele.
- Hebu tafakari pia juu ya hii… Miili yetu inahitaji chakula; na bila chakula tutakufa. Lakini ni ya faida gani kama tutakufa na miili yenye afya na bila Mungu na kuteseka kwa hukumu ya milele?
- Pia tunahitaji kusikia na kuamini Neno la Mungu ili tuwezeshwe kuishi milele na Mungu.

C. Jaribio la pili.

- **Mat 4:5-6 –** Shetani alikuwa ananukuu sehemu ya **Zab 91:11, 12**. Inashangaza kuwa shetani anajua maneno ya Mungu kwa Biblia, lakini anayatumia kwa njia mbaya.
- Anayachanganya maneno ya Mungu ili awadanganye na kuwafanyia hila watu.
- Shetani ni mwongo na mdanganyifu. **Yoh 8:44**
- Bado anatumia hii njia hata leo. Anajaribu kuwafanya watu wafikirie ya kuwa yafaa Mungu atenda miujiza kwao ili ajidhibitishe kwao. Anajaribu kuvuta hisia zetu kwa utenzi na miujiza na, kujaribu kutufanya tusiwe waangalifu kwa kile Mungu anasema haswa katika Neno Lake.
- Shetani alimwambia Yesu achitupe chini kutoka tari la hehalu ili kumjaribu Mungu ambaye kwa uhakika anaahidi kumlinda mwanawe.
- Je, Yesu alihitaji kumjaribu Babake ili ajue kuwa atamulinda? La hasha!
- **Mat 4:7 –** Mungu Baba alikuwa ameahidi kumlinda mwanawe, kwa hivyo Yesu alitumainia tu maneno ya Babake. Tangu mwanzoni Mungu alikuwa amedhibitisha yeye ni mwaminifu. Sisi pia kama Yesu twaweza kumtumainia.

D. Jaribio la tatu.

- **Mat 4:8,9 –** Shetani angempa Yesu mamlaka juu ya watu wote humu duniani kwa sababu , wakati Adamu alimuasi Mungu akamfuata shetani, shetani alifanyika mungu wa dunia hii. **2 Wakorintho 4:4; Yoh 12:31**
- **Mat 4:10 –** Shetani alijaribu kumfanya Yesu amwabudu.
- Unakumbuka ya kwamba hapo mwanzo, Shetani alijaribu kuchukuwa nafasi ya Mungu kama mtawala juu ya ulimwengu wote lakini akashindwa, lakini malaika wengi walimfuata? Tena akachukuwa utawala juu ya vizazi vya wanadamu ili waweze kumwabudu na kumtumikie. Shetani alijua kuwa Yesu ni mwana wa Mungu, kwa hivyo alijaribu kuchukuwa nafasi ya Mungu kwa kumjaribu Yesu amwabudu.

- Sisi sote ambao hatujakombolewa na Mungu tunamtumikia shetani badala ya Mungu. **Waef 2:1-3**
- Yesu alimshinda shetani kwa kumwambia kihalisi vile Mungu anavyosema katika Biblia.

E. Yesu ni Mungu.

- Yesu ni mkuu sana juu ya Shetani. Yeye ni Mungu.
- Hapo mwanzo, Mungu Slimuumba shetani kama Lusifa, malaika muhimu na mtanashati ambaye alistahili kumtumikia Mungu, lakini hakufanya hivyo na siku moja Yesu atamrusha shetani kwenye ziwa la moto ambalo Mungu alimtengea na wafuasi wake wote**. Ufunuo 20:10**
- Tazama: waweza kuwa na video na michezo inayoonyesha mapambano kati ya nguvu ziitwazo nzuri na mbovu.
- Mara nyingi haya mapambano yaweza onyeshwa kana kwamba hizi nguvu zinazopigana zinatoshana – aina ya vita vya “kizambamba”.
- Huu ni mtazamo wa binadamu juu ya vita , lakini Neno la Mungu linatuarifu kuwa Mungu ni mkuu; yeye ni muumbaji mkuu, na Yesu ni Mungu.
- Kitu kingine cha kufikiria juu yake - Shetani hangemfanya Yesu atende dhambi. Shetani ni adui mkubwa, lakini halingani na Mungu Mkuu.
- Vita si vile huwa wanadamu wanavyonyesha. Mungu si “**mvuto**”; Yeye ni Roho. Wakati Yesu alitujia, alikuwa Mungu katika mwili wa kibinadamu. Mungu ni mkuu zaidi juu ya shetani katika kila hali. **Luka 12:4-5**

F. Shetani alimwacha Yesu kwa muda mfupi.

- **Mat 4:11** – Shetani alijua kuwa ameshindwa, kwa hivyo akamwacha Yesu ili apate muda mwingine. **Luka 4:13**
- Lakini shetani alirejea tena mara kwa mara na kujaribu kwa njia zote kumjaribu Yesu amuasi Mungu.
- Alimwandama Yesu na kila jaribio ambalo watu wamewahi pitia, lakini Yesu hakutenda dhambi. **Waeb 4:15**
- Ningependa kushiriki wazo hili; Yesu pekee ndiye amewahi kumtii Mungu kikamilifu na kumpinga ibilisi.
- Yesu Kristo alikuwa mwanadamu kamili; na pia ni Mungu.
- Ni yeye pekee anaweza kutukomboa kutoka kwa dhambi, Shetani na mauti.

SOMO LA 18

Yesu alianza huduma yake – Marko 1:14-42

Lazima uzaliwe mara ya pili – Yoh 3:1-20

Yesu alianza huduma yake. .

A. Yohana Mbatizaji.

- Kumbuka kusudi ya huduma ya Yohana mbatizaji.
- Kwa uaminifu alifunza Neno la Mungu kuwaandaa watu kutumaini Yesu Mkombozi.
- Mfalme Herode, aliyekuwa akiishi maisha ya dhambi, hakupenda baadhi ya vitu ambavyo Yohana alisema.
- Kwa hivyo Herodi alimweka Yohana gerazani na hatimaye akamuua. **Mat 4:1-12.**
- Kabla ya kuuawa, Yohana alikuwa amemaliza kazi ya kuandaa njia ya Bwana.

B. Ujumbe wa Yesu

- Ilikuwa sasa ni wakati wa Yesu kuanza kufunza**. Marko 1:14, 15.**
- Vile tulivyotaja, Yesu alikuwa sasa na umri wa kadri ya miaka 30.
- Alianza kuwafunza watu kwa kuwaamuru:
- Kubadilisha nia zao .
- Kukubaliana na Mungu kuwa walikuwa wenye dhambi wasioweza kujisaidia.
- Kuamini habari njema ambayo alikuja kutuambia.
- Kama hatumwamini Mungu, hatuwezi mpendeza, na hata tukubali.
- **Waeb 11:6 –** inasema, “bila imani haiwezekani kumpendaza Mungu.”
- **Waeb 10:38**
- Kama tunataka kukubalika na Mungu, ni lazima tumwamini na kutumaini kwa kile ametuambia katika Biblia.
- Neno **“injili”** linamaanisha **“habari njema”**
- Yesu aliwaambia watu kuwa lazima wakubaliane na Mungu na kuamini habari njema, kwa kuwa utawala wa Mungu duniani ulikuwa karibu kuanza.
- Kumbuka Shetani alikuwa mtawala wa dunia wakati Adamu alimuasi Mungu na kumfuata Shetani**. Yoh 12:31; 2 Wakor 4:4.**
- Sisi sote, wakati tulizaliwa katika ulimwengu huu, tulizaliwa katika ufalme wa Shetani na chini ya mwongozo wake.
- Yesu alisema kuwa njia ya pekee kwa yeyote kuebuka utawala wa shetani ni kukubaliana na Mungu na kuamini habari yake njema.
- Ilikuwa wakati huu ambao Yesu alianza kuwaita watu wamfuate.

C. Yesu aliwaita watu wamsaidie katika kazi yake.

- **Marko 1:16-20**
- Alikuwa anaenda kuwafunza, na kuwatuma waende kuwaambia wengine ujumbe wa utawala wa Mungu ambao ulikuwa unakuja duniani.

D. Yesu alifunza na mamlaka.

- **Marko 1:21 –** Wayahudi walikutanika mahali palipoitwa sinagogi katika miji kote kote Israeli na hata nchi jirani.
- Hapo kwenye sinagogi, maandishi ya Musa na manabii yalisomwa na kufunzwa.
- **Marko 1:22 –** watu waliosikia Yesu akinena walishangaa na njia ya mamlaka aliyotumia kufunza na kuelezea maana ya Neno la Mungu.
- Yesu alifunza tofauti na jinsi Waandishi walivyofunza.
- Waandishi walikuwa ni watu waliotoa chapa ya agano la kale.
- Pia walikuwa walimu wa Neno la Mungu.
- Lakini wengi wao hawakuwa na imani ndani ya Mungu na hawakuliamini Neno lake.
- Waliamini katika matendo yao mema na umaarufu wao katika Neno la Mungu kuwaokoa.
- Walijua mengi kuhusu Neno la Mungu, lakini kwa uhakika hawakumjua Mungu.
- Lakini Yesu ni Mungu.
- Yesu alimjua Babake, na alielewa vyema Neno la Mungu.
- Wakati Yesu alifunza, aliwaambia watu kiuhakika alivyosema Mungu kupitia maandiko ya Musa na manabii.

E. Yesu alikemea roho wachafu.

- **Marko 1:23, 24 –** mapepo hupenda kuishi na kuwaongoza watu ambao ni watoto wa shetani. **Lk 11:24-26.**
- Rejelea tena **Marko 1:24 –** tazama shetani na mapepo wanatambua kuwa Yesu ni Mungu, Muumba wao. **Wakolosai 1:16.**
- Hili pepo katika marko 1 lilijua kwamba siku moja litakuja kurushwa kwenye ziwa la moto, na lilijua ya kwamba Yesu alikuwa na uwezo wa kumrusha motoni papo hapo. **Ufunuo 1:18; 20:10**
- **Marko 1:25 – 26** - Yesu aliamuru pepo kukimya **msitari wa 25**
- Hakutaka mapepo kuwa ndio wakuwambia watu kumhusu (yesu).
- Shetani na mapepo wake ni waongo. Yesu alikuja kunena kweli.
- Yesu mwenyewe angewaambia watu ukweli wa Mungu na awaonyeshe nguvu yake kupitia kwa miujiza aliyotenda.
- Tazama uasi wa mwisho katika **mstari 26**.
- **Marko 1:27-28** –Tena, watu waliona kuwa Yesu alikuwa na nguvu na mamlaka ya kustaajabisha.

F. Yesu aliwaponya wagonjwa

- **Marko 1:34-39** –Yesu Kristo ni mwenye nguvu juu ya vyote, Mungu mwenye huruma na upendo, aliwahurumia wagonjwa na waliopagawa na mapepo. Pia anatujali wewe na mimi. Hajabadilika. Bado ni yule yule hadi leo hii. Tamanio lake ni kutuokoa wote kutoka kwa utawala wa shetani.

G. Yesu alimponya mwenye ukoma.

- **Marko 1:40-42 –**Wenye ukoma walikataliwa katika nyakati za Biblia na hata hakuna yeyote ambaye angewakaribia wala kuwagusa.
- Lakini Yesu alimguza mtu huyu.
- Aliunyosha mkono wake, akamshika mwenye ukoma na akanena, na ukoma ukaisha.
- Angenena tu na mgonjwa angepona lakini hakufanya hivyo. Bali alimgusa, kwa nini? Kwa nini akatenda hivyo? Kuonyesha upendo mkuu na rehema za Mungu.

H. Hitimisho.

- Inastahili tujitambulishe na yule mwenye ukoma.
- Kwa sababu ya dhambi zetu, pia sisi ni wachafu na hakuna chochote tunachoweza kutenda kwetu sisi wenyewe kujiondolea lawama na malipo ya dhambi.
- Ya kuhusunisha watu ambao wangetusaidia waweza kukataa kwa sababu waweza kuwa wametuasi, kama tu mwenye ukoma alivyo kuwa amekataliwa.
- Lakini Mungu hujua kila jambo lolote la kutisha katika maisha yetu na bado anataka kuwa Mwokozi wetu.
- Si tu kutujali na kuwa na uhiari wa kutufikia, bali ni yeye tu aliye na uweza wakutuokoa.

lazima uzaliwe upya .

A .Nekodemo alimjia yesu

- Fungua nami **Yoh 3** na hebu tukatazame **mstari wa 1 na 2**
- Nikodemo alikuwa na uhakika kuwa Mungu alikuwa amemtuma Yesu.
- Alijua yakuwa miujiza mikubwa ambayo Yesu alikuwa akitenda, ingewezekana tu kupitia kwa nguvu za Mungu.
- Mafarisayo wengi walimchukia Yesu na walisema kuwa alitenda miujiza yake kwa nguvu za shetani.
- Tazama **mstari wa pili**…alimjia yesu usiku, kwa nini?
- Nekodemo yawezekana kuwa alimjia yesu usiku ili viongozi wengine wa kiyahudi wasimwone.

B. Kuzaliwa upya.

- **Yoh 3:3** – Wayahudi haswa sana Mafarisayo walijidai kuwa hao ni uzao wa Ibrahimu.
- Walidhani kuwa wamo katika jamii ya Mungu kwa kuwa walikuwa wana wa Ibrahimu.
- Mafarisayo hawakugundua kuwa kila mtu aliyezaliwa duniani humu, amezaliwa chini ya utawala wa shetani (katika ufalme wa Shetani) na kwa hivyo ni mwana wa shetani.
- Kumbuka Mungu alipowaumba Adamu na Hawa, aliwaumba kwa mfano wake. Aliwapa akili ili waweze kumjua na kumufahamu. Aliwaumba ili wampende. Lakini wakati Adamu na Hawa walipotenda dhambi, walikufa kwa Mungu. Walikufa kiroho. Walitenganishwa na Mungu.
- Bado walikuwa na akili lakini kwa sababu ya dhambi, hawakuweza kumfahamu Mungu wala hawakuelewa maneno yake. Hata hawakuweza kumpenda wala kumtii Mungu.
- Mawazo yao, mioyo na nia zao sasa zilikuwa chini ya utawala wa Shetani.
- Kaini na Habili na watu wote waliozaliwa kabla ya hapo, walizaliwa bila uwezo wa kumjua, kumwelewa, kumpenda na kumtii Mungu.
- Yesu alimweleza Nikodemo kuwa njia ya pekee ya mtu kuepuka nguvu na utawala ya shetani, na aweze kujua, kupenda na kutii Mungu ni kuzaliwa tena.
- Kuzaliwa mara ya pili inahusisha kumpokea Roho Mtakatifu ili tuweze kumjua na kumwelewa Mungu, kama Adamu na Hawa walivyokuwa wakati Mungu aliwaumba**.Yoh 14:26**
- Inawezekana aje kwa mtu kuzaliwa tena?
- Ni vipi mtu anaweza kubadilishwa ili awe chini ya utawala wa Mungu na si tena chini ya utawala wa Shetani?
- Je, tunaweza jibadilisha wenyewe?
- La hasha! Hatuwezi : **Yoh 1:12-13**
- Hapa kuna wazo kuu: Je, kuna kitu tulichofanya ili tukazaliwa chini ya utawala wa shetani humu duniani?
- La hasha! Adamu alitenda dhambi, na hivyo kila mmoja aliyezaliwa baada ya Adamu alirithi dhambi yake.
- Sisi wenyewe hatukutenda chochote cha kutusababisha tuzaliwe chini ya utawala wa Shetani.

- Hata hivyo hatuwezi tenda chochote kuepuka utawala wa Shetani.
- Haiwezekani sisi wenyewe kurejesha umoja wetu na Mungu.
- Ni Mungu tu anaweza tenda hilo.
- Yeye ni Mkuu.
- Hakuna kisichowezekana kwake.
- Kwa uweza wake, anawafanya watu kuzaliwa tena upya katika jamii yake.
- **Yoh 3:4** – 'Nekodemo alishangaa wakati Yesu alimwambia kuwa ni lazima mtu azaliwe upya.
- Hadi alipozungumza na Yesu. Alikuwa na uhakika kuwa kuzaliwa kwake kwa mara ya kwanza kungemweka katika nafasi bora ya kuwa na uhusiano na Mungu.
- Alikuwa wa kizazi cha Ibrahimu.
- Alikuwa Mfarisayo na alikuwa mtawala wa Wayahudi.
- Alionekana kuchanganywa hasaa na maana ya neno **"kuzaliwa upya"**. Tazama **ms wa 4** tena.
- **Yoh 3:5 –** Maji yaliyozungumziwa na Yesu sio ubatizo.
- Ubatizo hauwezi tufanya wana wa Mungu, wala kusafisha dhambi zetu.
- Naamini Yesu anazungumzia kuzaliwa mara tena kwa kusafishwa kwa maji kwa Neno.
- **1 Petero 1:23; Waefeso 5:26; Yoh 15:3; Zab 119:9**
- Wakati Yesu alisema kuwa kila mtu anayezaliwe upya ni lazima azaliwe kwa maji kwanza, Yesu alimaanisha kuwa njia ya pekee ya mtu kupokea mawazo mapya, aweze kumpenda na kumtii Mungu, na apewe maisha mpya ni kwa kusikia, kuelewa na kuamini Neno la Mungu.
- Tazama anasema kuzaliwa kwa maji na Roho.
- **Yoh 3:6,7 –** Yesu alimwambia Nekodemo kutoshangaa kwa kile alichomwambia kuwa azaliwe upya.
- Mungu anasema kuwa kuna aina mbili pekee ya watu duniani – sio wale walio tajiri na walio maskini, sio wale walio wazuri na wale walio wabaya; ila ni wale waliozaliwa mara moja na waliozaliwa mara mbili.
- Waliozaliwa mara moja- ni wale ambao bado wako chini ya utawala wa Shetani. Kuzaliwa mara moja na kufa mara mbili.
- Kuzaliwa mara mbili – wale ambao wamezaliwa mara ya pili na hivi sasa wanatawaliwa na Mungu. Kuzaliwa mara mbili na kufa mara moja.
- Nekodemo bado hakuelewa jinsi ya kuzaliwa katika familia ya Mungu. **Mstari wa 8,9**

C. Yesu ni lazima ainuliwe juu.

- Tazama Yesu anaendelea katika **msitari wa 14 na 15** kumfafanulia Nekodemo kwa kumukumbusha kilichotendeka kwa Waisraeli katika jangwa.
- Kumbuka katika **Hesabu 21:5-9,** Waisraeli walikuwa wametenda dhambi kwa Mungu kwa hivyo Mungu aliwatumia nyoka wenye sumu kuwauma, na wakaanza kufa. Wakati walitubu , yaani, kubadili mawazo yao na kukubali dhambi zao, Mungu alimwamru Musa atengeneze nyoka wa shaba na kuiweka juu kwenye mlingoti. Mungu aliahidi kuwa yeyote aliyeumwa na kumtazama Nyoka wa shaba atapona.
- Sasa hapa tunaye Nekodemo, amekuwa akijaribu kutii sheria ya Mungu. Hakutambua ya kwamba juhudi zake hasikukubalika na Mungu. Alistahili kutenda jinsi Waisraeli walitenda kwa kuweka Imani yake katika Bwana.
- Na sisi je? ... hali zetu, pia ni kama ya Waisraeli kule jangwani.
- Shetani, joka zee, ni adui wetu mkubwa.
- Anajitahidi kutuangamiza. **Ufunuo 12:9; 20:2**
- Na kama tu Waisraeli hawangejiokoa kutoka kwa hao nyoka, sisi pia hatuwezi jiokoa kutoka kwa huyu shetani na mauti. Mungu aliwakomboa Waisraeli, na ni Mungu pekee aweza kutukomboa.
- Yesu alisema kuwa kuna njia moja tu ya kuokolewa kutoka kwa shetani, dhambi na mauti na ni kuzaliwa tena katika jamii ya Mungu. **Yoh 14:6; 12:32,33**

- Yesu alisema kuwa ni lazima ainuliwe kama tu nyoka wa shaba kule jangwani, na yeyote amwaminiye atazaliwa katika jamii ya Mungu.
- **Yoh 3:16 –** Biblia iko na habari mbaya na habari njema.
- Habari mbaya – Mwanadamu ni mwenye dhambi. **War 3:23** - kwa kuwa wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.
- Mshahara wa dhambi ni mauti. **War 6:23** – kwa kuwa mshahara wa dhambi ni mauti.
- Habari njema – Kristo alilipia malipo ya mauti ya mwanadamu. **War 5:8** – Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyeewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yatu, tulipokuwa tungali wenye dhambi.
- Mtu aweza kuokolewa kupitia kwa imani katika Kristo. **Yoh 3:16** – kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.
- **Waefeso 2:8-9**
- Wakati mwanamme, mwanamke au mtoto anaamini maneno la Mungu na kutumainia Yesu kama mwokozi wake, Mungu humpa mtu huyo maisha mapya.
- Huyo mtu hatakuwa tena mtoto wa shetani ama hata chini ya utawala wake, lakini atakuwa mtoto wa Mungu na hataangamia bali atakuwa na uzima wa milele.

D. Njia ya maisha na mauti.

- **Yohana 3:17** – hii ni ahadi ya Mungu.
- Je, Mungu aweza kutumainiwa?
- Naam; tumesoma mara kadha wa kadha jinsi ametenda haswa kile ambacho aliahidi.
- Tumesoma ahadi za Mungu kwa miaka elfu na elfu na hakuna yoyote ambayo imekosa kutimizwa.
- **Yoh 3:18 –** hakuna yeyote ambaye anatakikana kungojea hadi afariki ndipo ajue kama atakubalika au atakataliwa na Mungu.
- Wale waliomuasi mwokozi washahukumiwa na kukataliwa na Mungu. **1 Yoh 5:10-13**
- Ni mwokozi mmoja tu ambaye amepeanwa na Mungu kwa wenye dhambi na huyo mwokozi ni Yesu. **Matendo 4 :12**

SOMO LA 19

Yesu ni Kristo, Mwana wa Mungu;

Yesu alibadilishwa Marko 8:27 - 9:8

Yesu ni mlango wa pekee kwa Uzima wa milele Yohana 10:7-11; 14:6.

Yesu ni Kristo; Mwana wa Mungu; Yesu alibadilishwa. .

A.Utangulizi.

- Watoto hufurahia hadith za kupuniwa na hivyo ndivyo ilivyo na watu wazima.
- Lakini tunapozingatia mahali tutaishi milele, tunahitaji kusemezana kweli bali sio hekaya.
- Ulimwenguni kote, watu hufuata imani na mawazo ambayo si kweli bali ni uongo wa Shetani, ambao umeundwa kuwavuta waume, wake na watoto kutoka kwa Mungu. **(kijitu jagina, sungura mjanja, baba wa Krismas).**
- Lakini tunaposoma Biblia, tunasoma kweli ambayo imepeanwa kwetu na Mungu mwenyewe, asiyedanganya.

B. Watu walisema Yesu ni nani?

- **Marko 8:27,28 –** Unakumbuka mfalme Herode alikuwa amemfunga na kumuua Yohana Mbatizaji, kwa hivyo watu wengine walifikiri kuwa Yesu ni Yohana, ambaye amefufuka kutoka mautini.
- Wengine walifikiria kuwa ni Elia.
- Elia alikuwa nabii aliyechukuliwa na Mungu mbinguni karibu miaka **850** kabla ya Yesu kuzaliwa ulimwenguni**. 2 Wafalme 2:10,11**
- Watu wengine walifikiri kuwa Yesu ni Elia ambaye amerejea tena kutoka mbinguni. **Malaki 4:5-6**
- Hata hivyo, Yesu alikuwa amejitambulisha wazi wazi kwa watu yeye ni nani.
- Alikuwa amewaeleza kuwa yeye ni Mwana wa Mungu, Mkombozi ambaye Mungu aliahidi tangia mwanzoni mwa ulimwengu.
- Alikuwa amewaonyesha nguvu zake kwa miujiza mikuu, ambayo alitenda.
- Lakini bado watu wengi hawakumwamini.
- Ni ya muhimu sana kuamini Yesu alikuwa nani. Je, alikuwa tu mwalimu mwema aliyetenda miujiza kadhaa? Je, alikuwa tu nabii kama manabii wengine vile Wayahudi walifikiria? Je, alinena kweli? Kama sio, basi alikuwa mwongo? Nataka kusema hivi, Yesu hakutupea uchaguzi wa kuamini tu Fulani wa kile alisema kujihusu. Kama chochote alichosema hakikuwa cha ukweli, basi hangekuwa Mungu Mwana, kwa sababu Mungu ni mtakatifu na mkamilifu. Kumbuka Yesu alisema kuwa Yeye ni Mungu. **Yoh 1:1,14; 10:30; 14:7,9.**

C. Kile Petero aliamini kumhusu Yesu.

- Hebu tusome tena **Marko 8:27-29** – Yesu alijua ya kwamba Mungu hangewakubali wanafunzi wake kama hawangemkubali kama Mwokozi aliyetumwa na Mungu katika dunia. Wakati huu, angalau mtu mmoja, Petero, alijua na kuamini.

- **Marko 8:30 –** yesu alitaka watu wamsikize na kuamini maneno yake mioyoni mwao. Hakutaka wamfuate tu kwa kuwa wanafunzi wake walisema kuwa yeye ni Kristo. Na hata leo hii amezalia kuwa vivyo hivyo hataki tumfuate tuu kwa kuwa mwalimu au mchungaji, au mtu mwingine yule ametwambia kile anaamini kumhusu Kristo. Hatustahili kumtegemea mtu yeyote yule bali twastahili kuamini Neno la Mungu. Imani yetu inastahili kuwa ndani ya Mungu na Neno lake.

D. Yesu alitabiri kifo chake na ufufuo.

- **Marko 8:31 –** Yesu alijua kuwa ni lazima afe.
- Alijua ya kwamba Shetani atawatumia makuhani wa Wayahudi kumuua kwa kuwa hawakumwamini kuwa ni Mwana wa Mungu, Mkombozi. Pia alijua kuwa, hata kama atakufa na azikwe, atoke kaburini baada ya siku tatu.
- Je, twaweza kujua kile kitatendeka kwetu kesho? Je, tunaenda kuwa wagonjwa kesho? Je, tutakuwa wapi baada ya mwaka mmoja kutoka saa hizi? Tutaishi miaka ngapi duniani humu? Hatuna jibu kwa maswali haya yote, lakini Yesu alijua hatima yake yote/yote ya uzoni.
- Mungu anajua kila kitu.
- Nataka kusema hivi – miaka mingi kabla, manabii walikuwa wamepeana unabii wa yale yote ambayo yatatendeka kwake Yesu.
- Atateseka kwa vitu vingu.
- Makuhani wa Wayahudi watamkataa.
- Atauawa.
- Lakini atafufuliwa kutoka wafu.
- Yesu alijua na kuamini kile kilichoandikwa kumhusu katika Agano la Kale. **1 Petero 1:10-11**
- Yesu alijua ya kwamba yeye ndiye Mkombozi aliyeahidiwa na Mungu na alijua ya kwamba kila kitu ambacho kilinenwa kumhusu kitatendaka, kwa kuwa Neno la Mungu lazima litimizwe.

E. Yesu alibadilishwa.

- **Marko 9:2,3** Yesu alikuwa na mwili kama wetu**.**
- Alikuwa mwanadamu kikamilifu na pia alikuwa Mungu halisi.
- Kila mtu aliyemwona alimwona kama mwanadamu wa kawaida kama wao.
- Lakini kile alitenda na kusema kilikuwa tofauti na watu wa kawaida.
- Ni la kustaajabisha kwangu kuwa, ni huo wakati pekee ambapo Yesu akiwa duniani, sehemu yake ya kiungu ilidhihirishwa katika mwili wake wa kibinadamu.
- Mwili wake wa kibinadamu ulikuwa ukificha "sehemu ya kiungu**". Isaya 53:1-2**
- Je, wakumbuka maskani ambayo Mungu alimwamuru Musa na Waisraeli kumjengea mlimani Sinai wakiwa jangwani? Nje ya maskani hiyo kulifunikwa na ngozi za wanyama. Wakati watu waliitazama, waliona tu ngozi mzee iliyokauka, lakini ndani mwa chumba la ndani, ndani mwa zile ngozi kuling'aa nuru dhabiti iliyoashiria uwepo wa Mungu.
- Je, wajua kuwa katika kitabu cha Mathayo, tunaambiwa ya kwamba Yesu alipokuwa pale juu mlimani, uzo wake ulianza kung'aa kama jua**? Mat 17:2**

F. Musa na Elia waliongea na Yesu.

- **Marko 9:4 –** Elia alikuwa nabii wa kiyahudi.
- Lakini Elia hakufa kama watu wengine.
- Vile tulivyosema hapo mwanzoni, Mungu alimchukuwa mbinguni takribani miaka 850 kabla ya Yesu kuja duniani.
- Biblia katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati inatueleza ya kwamba, Musa alikufa na akazikwa na Mungu**. Kumb 34:5,6**
- Kifo cha Musa kilitokea karibu miaka **1 400** kabla ya Yesu kuzaliwa duniani.
- Mungu hakumchukua mbinguni jinsi ilivyokuwa na Elia.

- Musa alitenganishwa na mwili wake na mwili huo ukazikwa.
- Sasa fikiria juu ya hii… kwa hii miaka yote Musa na Elia wamekuwa na Mungu. Walipokuwa humu duniani walimwamini Mungu na walitumainia kuja kwa Mkombozi humu duniani. Ni kwa sababu ya haya, walipotoka humu duniani, hawakutenganishwa na Mungu kuzimuni.
- Mungu aliwakubali pamoja na Habili, Sethi, Henoko, Ibrahimu, Sarai, Isaka, Yakobo, Yusufu, Yoshua, Daudi, na kila mtu aliyekubaliana na Mungu kuwa wenye dhambi na kumtumainia Mungu kuleta Mwokozi.
- Na sasa Musa na Elia walirudi duniani kuongea na Yesu.
- Nataka niseme hivi; Mbinguni ni mahala halisi na ni makazi ya Mungu.
- Kila mtu anayekubaliana na Mungu na kumwamini Yesu Mwokozi aliyetumwa na Mungu, ataenda kuishi naye wakati atafariki.

  Yoh 3:16; 14:1-6
- Wakati Musa na Elia, manabii wa Mungu, waliishi humu duniani, walijua kuwa Mkombozi mtarajiwa ilikuwa azaliwe na afe.
- Soma **Luka 9:30-31** na uone kile Musa, Elia na Yesu walikuwa wanazungumzia.
- Hata kama Musa na Elia walitoka duniani miaka mingi sana kabla ya Yesu, walijua ya kwamba ahadi za Mungu kumhusu Mkombozi zitatimia jinsi alivyosema. Mungu hawezi kusahau ahadi zake, hata kama maelfu za miaka zitapita kabla ya kutimia.

G. Kile Mungu Baba alinena kumhusu Yesu.

- **Marko 9:5-8 –** Huyu alikuwa ni Mungu Baba akinena.
- Aliwaeleza wanafunzi ya kuwa huyo ndiye aliyeahidi, yaani, Mwanawe aliyempenda zaidi.
- Kwa sababu Yesu alikuwa mwana wa mungu, Mungu aliwaambia wanafunzi ya kwamba ni lazima wasikize na kutii kila kitu ambacho Yesu alinena.
- Hakuchawahi kuwepo na hakutawahikuwepo mtu mwingine Kama Yesu, Mwana wa Mungu.

H. Hitimisho.

- Leo hii Mungu huwa hazungumzi nasi kwa sauti kutoka mbinguni, kwa yote ambayo anataka kutueleza imeandikwa kwenye hiki kitabu, Biblia.
- Maneno yote ya Yesu ambayo Mungu anataka sisi tuyajue na kuyamtii yameandikwa katika Biblia, na Mungu anatarajia sisi kuyasikia na kuyaamini .
- Miaka mingi baada ya Yesu kufa , Petero aliandika haya;
- **2 Petero 1:16-21**
- Biblia ni kweli.
- Manabii wa Mungu walinena kweli ya Mungu.
- Yesu alinena kweli.
- Maneno yake yalipeanwa kwetu ili yatuongoze kwa Mungu na kwa uzima wa milele.

Yesu ndiye Mlango wa pekee kwa uzima wa milele. .

A. Utangulizi.

- Sehemu kubwa ya nchi ya Israeli ni kavu na tasa, na mara nyingi ilikuwa vigumu kupata hata nyasi tu ya kondoo. Mara nyingi watu walikuwa wakitembea mwendo mrefu kutafuta chakula na nyasi. Mara nyingi wangeenda milimani na kukaa huko kwa usiku kucha na mifugo wao. Ilikuwa hatari kulala nje kwa kuwa wanyang'anyi wangekuja usiku na kuiba mifugo na pia kulikuwa na wanyama wa mwituni ambao wangewauwa. Kwa hivyo, kabla ya giza kuingia, mchungaji angetafuta mahali salama ambapo mifugo wake wangelala ama angewaundia mahali pa kulala. Mahala ambapo wachungaji walitengeneza, ilikuwa mahali ambapo palizingirwa na miiba na mawe. Palikuwa tu na mlango mmoja wa kuingilia humo zizini na hapo ndipo mchungaji angelalia ili mwizi asiingie.

B. Yesu ndiye Mlango wa kondoo.

- **Yoh 10:7 –** Yesu alimaanisha kuwa yeye ndiye njia ya kuingia mahala pa salama.
- Nje ya dunia hii wapo Shetani na roho wake chafu, dhambi na mauti.
- Zinafananishwa na wanyang'anyi na wanyama wa mwituni, wanaoua na kula kondoo. **1 Petero 5:8**
- Kumbuka vita za shetani kinyume na Mungu. Yeye ni mwongo na mudanganyifu na anachukia mwanadamu. **2 Wakorintho 11:3; 13-15**
- Anaweza fanya kilicho kiovu kionekane jema na kilicho jema kionekane kiovu. Na hivyo ndivyo ilivyo na wale walio "nje ya zizi", Shetani husambaza ujumbe kuwa ni salama kuwa nje ya zizi katika ufalme wake. Kwani, inambidi mtu kuziacha anasa za ulimwengu ndipo aingie ndani ya mlango huo?
- Watu wengine watafikiria nini kumhusu mtu atakaye anza kumwamini Yesu badala ya kufuata umati? Hiyo ingefanya maisha kuwa magumu kwa kweli. Huyo mtu anaweza pata starehe mingi na hata kuwapoteza marafiki wake wengine.
- Haya ndiyo baadhi ya mawazo ambayo Shetani huwekwa ndani ya watu wanapozingatia kuweka Imani yao ndani ya Yesu Kristo kama Mwokozi wao.
- Fikiria juu ya hili: Itamfaidi nini mtu apate utajiri wote wa dunia hii, na siku moja akifa aingie kuzimuni. (Shetani huwa hataji hilo.)
- Shetani amekuwa akiwadanganya watu kwa muda mrefu sana na asimio lake haswa ni kuharibu ili tutenganishwe na Mungu milele. Huwa anajaribu kila njia kufanya njia zake zionekane njema.
- Lakini ni njia ya kifo, utengano na Mungu na hukumu ya milele.
- Kuna njia moja tu ya kuingia katika zizi, mahala salama na penye ulinzi na uzima.
- Yesu Kristo ni Mungu, yeye ni Mwokozi na ni mlango wa pekee kwa uzima wa milele.
- Hapana njia nyingine.

C. Wakombozi wa uongo.

- **Yoh 10:8**
- Kabla ya Yesu kulikuwepo na watu waliowahadaa Wayahudi kuwa hao ni wakombozi waliotumwa kutoka kwa Mungu.
- Yesu alisema kuwa hawa watu walikuwa kama wezi waliokuja gizani kuiba na kuwauwa kondoo.
- Hebu tutafakari hili: Njia ya pekee ya kutuwezesha kujua kweli ni kwa kujua kile Biblia inasema**. Yoh 8:32,36; 17:3**
- Nataka kusema hivi: mtu anaweza kuja kwa Mungu kupitia kwa njia ya Mungu.

D. Yesu, Mlango wa pekee.

- **Yoh 10:9 –** Jinsi kulikuwepo na mlango mmoja wa kuingia zizini, Yesu ndiye mlango wa pekee wa kuingia kwa uzima wa milele.
- Wajua watu wengine wanaweza kwambia kuwa kile ambacho Biblia inafunza ni sawa kwa wakristo, lakini kuna dini zingine ambazo zinaongoza watu kwa Mungu. Huo ni uongo wa Shetani. Hatuna njia mingi au milango mingi za kukufanya ukubalike na uwe na umoja na Mungu. Kuna mlango mmoja tu wa kutuelekeza kwa Mungu na kwa uzima wa milele.
- Yesu Kristo ndiye huo mlango. Alikuja kuwa Mwokozi wa watu wote, kila mahali licha ya utofauti wa lugha na maisha yanayoishi.
- Kumbuka, Mungu alimwambia Nuhu kujenga safina kwa kuwa alitaka kuwahukumu watu wote. Mungu alimwamuru Nuhu kujenga safina moja tu na aweke mlango mmoja tu. Ni wale watu waliopitia mlango mmoja wa lile safina ndio walio okolewa.
- Kutoka kwa hukumu ya Mungu. Nuhu alimwamini Mungu na akaingia kupitia mlango mmoja.
- **Yoh 10:10** – Yesu alisema kuwa yeye si kama Shetani, anayetaka tu kuwaangamiza watu. Yesu alikuja duniani kupeana uzima kwa kikamilifu.

- Mojawapo wa uongo wa Shetani ni kuwa njia yake ndiyo iliyo bora, njia ya kupendeza na kufurahisha kwa kuishi. Huwapea watu starehe za kuwafanye wafikirie kuwa njia yake ni nzuri kuliko njia ya Yesu kristo. Lo! Ni uongo upi huo wahatari**! Mithali 14:12; Waebrania 11:25.**
- Nataka kusema hili kwa ujasiri jinsi ninavyoweza… Wote wanaokataa njia ya Yesu watachomeka kuzimuni bila kuacha yeyote **Ufunuo 20:15**
- Yesu alisema wazi hapa katika **Yoh 10:10** ya kwamba hupeana uzima na hupeana teletele.
- Ahadi zake ni kweli.
- Maisha anayopeana Yesu ndiyo njia bora ambayo hatutajuta mwishowe.

E. Yesu, Mchungaji Mwema.

- **Yoh 6:35** tena rudi kwa **Yoh 10:11**
- Yesu alikuwa amekwisha waeleza wanafunzi wake kuwa viongozi wa Wayahudi hawataamini kuwa alikuwa Mwana wa Mungu na Mwokozi na kuwa watamuua. Ako anawaambia hapa kuwa yeye ndiye mchungaji mwema anayependa kondoo wake sana ambapo atawafia ili awaokoe kutoka kwa wanyang'anyi au wanyama wa mwituni ambao wanataka kuwauwa.
- Ni la kushangaza kuwa Isaya nabii, alisema miaka mingi kabla ya Yesu ya kwamba, atatezwa na afe kwa ajili yaw engine. **Isaya 53:3-5.**

F. Yesu, Njia, Kweli na Uzima.

- **Yoh 14:6**

G. Hitimisho.

- Kunaye Mungu mmoja tu, Mwokozi mmoja wa ulimwengu wote, wako, na wangu. Hakuna njia nyingine ya kuokolewa**. Isaya 43:11; Matendo 4:12; 1 Tim 2:5-6.**

SOMO LA 20

Yesu alimfufua Lazaro kutoka kwa wafu - Yoh 11:1 – 48

Yesu aliwapenda watoto na kumfunza kijana tajiri mtawala - Marko 10:13-24

Yesu alimfufua Lazaro kutoka kwa wafu. .

A. Utangulizi

- Somo letu leo ni kuhusu kitu ambacho watu wengi hujaribu kukikwepa kuongea juu yake kila mara; kifo.
- Ni la ajabu jinsi watu wengi hujaribu kulikwepa na hata kulitaja tu.
- Tunazungumzia kuhusu afya yetu.
- Hata tunazungumzia umri wetu.
- Wengi hutumia hata pesa nyingi kujaribu kutafuta uponyaji na kuishi vyema, kujaribu kuonekana kuwa bado ni vijana kwa kujaribu wasizeeke. Lakini ni watu wachache ambao wangependa kuzungumzia kifo.
- Yesu alizungumzia…aliizungumzia Sana…Na kile alichozungumzia inadili kubadilisha mawazo yetu daima kuhusu maisha na kifo.

B. Yesu alingojea hadi Lazaro akafa.

- **Yoh 11:1-6 –** Yesu alikuwa upande ule mwingine wa mto Yordani, na ingawa alikuwa mbali kutoka mahali Lazaro alikuwa alijua yote yatakayotendeka kwake, kwa sababu Yesu ni Mungu.
- Hakuna lolote ambalo hajui, na hakuna lolote ambalo hawezi tenda.
- Angeweza kumponya Lazaro bila kuenda mahali alikokuwa.
- Au angeenda haraka na kumponya Lazaro papo hapo, lakini alingoja baada ya siku mbili kwa maana alijua hiyo hali inaenda kumpa fursa ingine kuonyesha nguvu zake za ajabu kama Mwana wa Mungu. Ijapokuwa yawezaonekana kwamba Yesu hakuwapenda Martha, Mariamu na Lazaro, lakini hiyo si kweli. Aliwapenda na kuwachali. Kwa kweli hupenda kila mmoja wetu na nataka kila mmoja wetu amwamini na kumtumainia kama Mwokozi wetu. Lakini kupitia kwa kifo cha Lazaro, Yesu alikuwa anaenda kuonyesha nguvu zake za kupeana uzima kwa watu wamwaminio.

C. Yesu alienda kumfufua Lazaro kutoka kwa wafu.

- **Yoh 11:7-16.** Wanafunzi wake hawakuelewa alichomaanisha.
- Walifikiria ya kwamba Yesu anaenda kuwaruhusu viongozi wa Wayahudi wamuue ili aende awe na Lazaro. **Mstari wa 15.**

D. Yesu ni ufufuo na uzima.

- Yesu hakumaanisha hayo. **Yoh 11:17-22**
- Martha aliamini kwamba Yesu alikuwa na nguvu za kuponya nduguye na ya kwamba Mungu, Babake, angemfanyia lolote ambalo Yesu angemuuliza kufanya. Soma

- **Yoh 11:23, 24. -** Yesu alitaka Martha aelewe kuwa, alikuwa anaenda kumfufua nduguye kutoka wafu wakati huo huo, lakini alifikiria ya kwamba yesu alimaanisha kuwa atamfufua wakati wa mwisho, watakapo fufuliwa watu wote**. Ufunuo 20:11-13**
- Kumbuka sasa kwamba, njia moja ya kuepuka hukumu ya dhambi ni kwa Yesu pekee, Mkombozi. **Soma Yoh 11:25**
- Yesu alitaka Martha kuelewa kwamba, Lazaro hakuitajika kukaa katika wafu, hadi siku ya hukumu ya Mungu kwa watu wote.
- Yesu ndiye hupeana uzima na kwa hivyo, ana nguvu za kurejesha uzima kwa wafu. Ni yeye pekee wakupeana uzima.
- Shetani hawezi peana uzima kwa wenye wamekufa.
- Ni Mungu pekee kupeana uzima kwa sababu yeye ndiye muumbaji mkuu aliyepeana uzima kwa kila mtu na kila kitu. **Wakolosai 1:16**
- Hebu waza hili; watu wengine huamini katika roho za waliokufa. Hufikiria ya kwamba mtu akifa hurudi na kuishi katika dunia tena kama mtu mwingine au mnyama au kiumbe. Huu ni uongo wa Shetani anataka watu wasiwaze kuhusu ukombozi wa dhambi zao. Anataka waamini kuwa hakuna jehanamu na hakuna hukumu. Kama anaweza kupata watu wa kuamini kuwa uzima wao u katika dunia hii basi hawatakuwa na haja ya Yesu Kristo na hawatahitaji kuokolewa kutoka hukumu ya haki ya Mungu. Shetani ni mwongo na mdanganyifu na mabadiliko ya waliokufa ni njia nyingine ya kuwazuia watu kukaa mbali na Mungu na njia ya milele. Haijalishi jinsi huo uongo unavyoelezwa, lakini si kweli. **Waebrania 9:27, Yoh 11:25, 26.**
- Yesu alisema, ingawa wale wanaomtumainia yeye kama mwokozi, hufa kimwili, kwa Mungu hawafi (kutenganishwa kwa kifo)
- Hawatenganishwi na Mungu ili wahukumiwe kwa ajili ya dhambi zao.
- Wao huondoka katika ulimwengu huu na kuenda na kuishi na Mungu mbinguni**. Yoh 5:24; 11:27.**
- Martha hakuwa kama watu wengine jinsi tulivyosema hapo awali.
- Walimfuata Yesu kwa sababu walitaka uponyaji au chakula au uhuru wa kisiasa.
- Hawakuwa na haja ya kumjua Yesu kama mwokozi, lakini Martha hakika alimwamini na kumtumainia yeye kama mkombozi aliyeahidiwa kutoka kwa Mungu.

E. Yesu alikwenda kwa kaburi la Lazaro.

- **Yoh 11:28-38**
- Yesu alijua kuwa anaenda kumfufua Lazaro kutoka wafu. Yesu alilia kwa kuwa alihuzunikia watu waliokuwa wakiomboleza kutokana na kifo cha Lazaro. **2 Wakorintho 1:3.**
- Je, wakumbuka kwamba Mungu alimuumba mtu kwa mfano wake? Alimpa mwanadamu hisia kwa sababu pia ana hisia. Yesu ni Mungu na ana hisia za huzuni na uchungu, ana uwezo wa kuhuzunika pamoja nasi tukihuzunika. Yesu alilia si kwa sababu, hakuwa na tumaini ya kumwona Lazaro akiwa hai katika ulimwengu huu ila alijitambulisha na uchungu ambao watu walikuwa nao kwa sababu ya matokeo ya dhambi.
- Hii ndiyo sababu alikuja katika ulimwengu na kuwakomboa waume, wake na watoto kutokana na mauti na kuwapa uzima wa milele.

F. Yesu alimfufua Lazaro kutoka wafu.

- **Yoh 11:39-44** Yesu ni Mungu.
- Hakujatokea mtu mwingine kama yeye.
- Yeye ni mkuu.
- Hapo mwanzo, yeye pamoja na Mungu Baba na Mungu Roho Mtakatifu waliumba vyote.
- Waliumba vitu vyote kwa kunena tu. Sasa Yesu kwa mlango wa kaburi alisimama na kunena tu.
- Alimwamrisha Lazaro kurudi kwa uzima tena.

- Je, wafikiria nini kingetendeka kama Yesu hangetaja jina Lazaro? **Yoh 5:28**

G. Wengine waliamini na wengine hawakuamini.

- **Yoh 11:45-48.**
- Wayahudi wengi waliamini Bwana Yesu baada ya kuona nguvu zake alizozionyesha kwa kumfufua Lazaro kutoka wafu. Lakini makuhani na Mafarisayo, tamaa yao ilikuwa ya kuendelea kuhifadhi nafasi zao za mamlaka na utajiri wao. Wao waliogopa kwamba watu huenda wakamfanya Yesu kama mfalme wao, kwa hivyo waandishi, makuhani na Mafarisayo walipanga kumuua Yesu. Shetani alikuwa anawaongoza hawa watu.
- Shetani hataki mtu yeyote kuamini Yesu na kuokolewa kutoka kwa nguvu zake.
- Hata sasa angali anawazuia watu kuamini ili waendelee kukaa katika uongo.

Yesu aliwapenda watoto na kumfunza kijana tajiri mtawala.

A. Yesu aliwapenda watoto.

- **Marko 10:13, 14 –** Wanafunzi wa hawakufikiria kwamba Yesu alitaka kuwa na nafasi kuwa na watoto kando na ratiba yake ya kawaida. Lakini Yesu aliwapenda watoto, alitaka wajue Neno lake na kuliamini pia.
- **Marko 10:15,16**
- Kile ambacho Yesu anamaanisha hapa ni ya kwamba yeyote asiyetaka kuja kwa Mungu na kumwamini kama watoto wadogo hawezi kuingia ufalme wa mbinguni.
- Hebu tuwaze kidogo alichosema hapa. Mtoto mdogo hutulia mkononi mwa mamake. Hana wasiwasi wa kuanguka. Anamwamini mama kwa ulinzi na malezi. Lakini tunapokuwa wakubwa tunaanza kujitegemea sana. Hatimaye tunakuwa watu wa kuwajibika. Lakini Mungu hakutuumba tuwe hivyo. Alimuumba mtu kwa sura yake, kumjua, kumpenda na kumtegemea Yeye. Lakini kama wenye dhambi hatuwezi kufanya hivyo kwa sababu tumetenganishwa na Mungu kwa sababu ya dhambi. Kiasili tumekuwa watu wa kujitegemea kwa ubinafsi na kufanya mambo kuwa mabaya Zaidi. Tunafikiria kwamba kama tutakuwa na mabadiliko yatakayotokea katika maisha yetu basi ni sisi tumeyasababisha. Huo si ujumbe wa Biblia; Yesu Kristo alikuja kuwaokoa wenye dhambi. Alisema kwamba lazima tuzaliwe mara ya pili na jinsi ilivyo vigumu kwa yeyote kujizaa mwenyewe kiasili, hivyo ndivyo ilivyo vigumu kwetu kujizaa mara ya pili (kuzaliwa kiroho).
- **Yoh 1:12,13**
- Ni Mungu pekee ana uwezo wa kutupa maisha mapya… ni yeye pekee mwenye uwezo wa kutuokoa kutoka kwa hukumu ya dhambi. Soma tena **mstari wa 13**
- **Yoh 3:16**
- Kwa sababu tunajitegemea sana na tunataka kujiamlia yote yanayotendeka kwetu, watu wengi huona vigumu kukubali injili kwa urahisi. Hiyo ndiyo sababu Yesu alisema lazima tuje kwake kama watoto na kumtegemea. Umati unaelekea jehanamu kwa sababu hautaki kumwamini Mungu na Neno lake. Lakini yeyote anayenyenyekea na kuamini Neno lake kama mtoto mdogo Mungu humwokoa.

B. Swali lake kijana tajiri

- **Marko 10:17 –** Huyu kijana alifikiria kuwa angemfurahisha Mungu na kuingia katika ufalme wake kwa kutenda wema na kutii sheria za Mungu.
- Hii ndiyo sababu alimuuliza Yesu kile anachostahili kufanya ili aingie katika ufalme wa Mungu.
- Kumbuka jinsi Kaini alivyofikiria kuwa, kuleta vitu alivyopanda kwa Mungu angepata kibali kutoka kwa Mungu? Je, Mungu alimkubali Kaini? Hapana!

C. Ni Mungu pekee aliyemwema.

- **Marko 10:18**
- Huyu kijana hakuelewa kuwa hakuna mtu hata mmoja aliyemwema**. Warumi 3:10-18**
- Hakujua kuwa ni Mungu pekee ndiye aliye mwema.
- Yesu alipomjibu, hakuwa anakana kuwa yeye mwenyewe si mwema au yeye si Mungu.
- Lakini Yesu alitaka huyu kijana aelewe kwamba hakuna mtu hata mmoja aliyemwema.

D. Njia ya sheria.

- **Marko 10:19,20**
- Huyu kijana hakujua ya kwamba alizaliwa mwenye dhambi na akiwa chini ya utawala wa Shetani na hangeweza kumtii na kumfurahisha Mungu kikamilifu. **Warumi 3:23; Isaya 64:6**
- Mungu anasema ya kuwa hakuna mtu hata mmoja aliyemwema na anayetenda haki machoni pake. Hakuna hata mmoja ila ni Yesu pekee aliyetii sheria za Mungu kikamilifu. Huyu mtu alidhani kuwa ametii sheria kumi za Mungu kwa sababu alizitimiza kimwili. Lakini hata kama alikuwa amezitii sheria za Mungu kimwili, hakuwa amezitii katika moyo wake. Tazama aliyoyafunza Yesu…**Mat 5:21, 22; 5:27, 28.** Mungu hamhukumu mtu kwa matendo yake ya nje pekee. Anafahamu mawazo ya mtu ya ndani, nia na tamaa.
- Kama mtu anapanga kuchukuwa kitu cha mwenzake, basi ameiba.
- Kama mtu mzima ama mtoto kimwili ananyenyekea chini ya utawala wa mtu lakini awe na hasira katika moyo wake ama atii kwa kulazimishwa, ametenda dhambi mbele za Mungu. **Waefeso 6:1,2** – Si kutii tu bali kutenda kwa nia njema. Mungu hakupeana sheria zake kwa Waisraeli akifikiria kuwa watazitii bali alizipeana ili kuwahakikishia Waisraeli nasi leo hii ya kwamba sisi sote tumetenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu Baba**. Warumi 3:19-20**
- Haiwezekani sisi kumpendaza Mungu kwa nguvu zetu wenyewe kwa kuwa sisi sote ni kizazi cha Adamu na tumezaliwa wenye dhambi na tukiwa tumetengwa na Mungu.
- Mungu hutazama mioyo yetu na kuona uovu.
- Hatutawahi pokea kibali cha Mungu kwa nguvu zetu.

E. Hatari ya kuwa tajiri.

- **Marko 10:21a**
- “Yesu akimkazia macho alimpenda…” Yesu alimpenda huyu kijana hata kama alikuwa na majivuno na kujiona kuwa mkamilifu mbele za Mungu. Mungu anampenda kila mmoja wetu, hata kama anatambua kuwa sisi ni watenda dhambi. Mungu hataki mtu yeyote kutenganishwa naye milele.
- **Marko 10:21**
- Yesu anarejelea tena swali la kwanza la tajiri… Nifanye nini? Yesu alimweleza huyu tajiri kuuza mali yake yote na awagawie maskini.
- Alijua ya kwamba tajiri huyo alikuwa na tamaa na aliipenda mali yake zaidi kuliko mwanadamu mwenzake yeyote yule.
- Alikuwa anajaribu kumfahamisha ya kuwa hakutekeleza amri inayosema, mpende jirani yako jinsi unavyojipenda.
- Alimtaka akubali kuwa yeye ni mtenda dhambi na alihitaji Mwokozi.
- Alijua ya kwamba huyu tajiri alipenda mali yake kuliko Mungu**. Mat 22:37-38**
- Hii amri kuu ya Mungu inayosema tusiweke kitu kingine kwa nafasi ya Mungu. Yesu alikuwa anamsaidia huyo kijana tajiri ajue kuwa, alikuwa ameweka mali yake kwa nafasi ya Mungu.
- Alikuwa amevunja sheria za Mungu, na basi, alikuwa mhukumiwa wa dhambi mbele za Mungu.
- **Marko 10:22-24**
- Huyu kijana tajiri mtawla alikuwa ameufanya uamuzi wake.

- Alichagua kufurahia mali yake katika maisha yake, na akaasi maisha ya milele ya kuwa na Mungu.
- Alikasirika kwa kuwa, hata kama alitaka uzima wa milele, alipenda mali yake kuliko Mungu.

SOMO LA 21

Upumbavu wa kutumainia utajiri- Luka 12:15-16:31

Yesu aliingia Yerusalemu; Yuda alipanga kumsaliti; Siku kuu ya pasaka- Marko 11:1-14:26

Upumbavu wa kutumainia utajiri .

A. Utangulizi.

- Katika maisha tunakabiliwa na shida nyingi. Je, dola **1000,000.00** zaweza kusuluhisha shida zako zote? Wakati mwingine tunafikiria kuwa zinaweza lakini hebu tuchukuwe muda kutafakari anachosema Mungu katika Neno Lake.

B. Upumbavu wa kuziishia mali za ulimwengu huu pekee.

- **Luka Mtakatifu 12:15**
- Watu wengi wanataka vitu za ulimwengu huu zaidi kuliko kitu kingine chochote.
- Wana wivu kwa vitu ambavyo watu wengine wanamiliki.
- Wanafikiria kuwa watakuwa na furaha na kutosheka kama watakuwa matajiri. Yesu aliwaambia watu hawa fumbo.
- Fumbo ni masimulizi kuhusu mambo ya dunia hii, lakini yatufunza kitu kuhusu Mungu na uhusiano wetu na Mungu. Haya ndiyo Yesu anataka tufahamu kuhusu mali.
- Hata kama mtu atakuwa na mali yote katika dunia itakuwa bila manufaa kama ataenda kuzimu. **Luka 12:16-19** Huyu mkulima alifikiria kuwa ana vyote alivyohitaji.
- Alifikiria kuwa hapana wasiwasi yoyote kwake kwa kuwa alikuwa mtu mkwasi sana.
- Alifikiria kuwa angemtupilia Mungu kando na aishi maisha yake jinsi alivyopenda.
- Hakutilia maanani kuwa ni Mungu apeanaye uzima na kuuchukuwa. **Ezekieli 18:4** Tukirejelea tena mkulima tajiri: Alipanga mipango yake jinsi angetenda, lakini Mungu alikuwa na mpango tofauti usiku huo huo.
- **Luka 12:20**
- Wakati Mungu anaamua kuwa ni wakati wa mtu kufa atakufa. Hakuna yeyote anayeweza kutenda chochote kumzuia huyo mtu kufariki. Hebu tafakari haya…hapa palikuwepo na mfanyi biashara mfanisi lakini Mungu alimwita mpumbavu. Kwa nini? Kwa sababu alifanya maamuzi bila kumhuzisha Mungu na akaishi tu kwa mali ya ulimwengu huu. **1 Wakorintho 1:18-20; 3:19;**
- **Luka 12:21.**
- Vitu vya dunia ni vya muda mfupi sana na hatuwezi kujua ni wakati gani tutakapoviacha nyuma.
- Lakini vitu ambavyo Mungu anapeana kwa wale wanao mtumainia vitadumu milele.

C Tajiri na Lazaro

- **Luka 16:19-21**
- Tofauti na masimulizi tuliyosoma, hili si fumbo. Je, tutajuaje hili? Njia moja ni kuwa, Yesu anatumia majina halisi hapa.

- Kwa wakati mmoja kabla ya Yesu kusimulia haya, hawa watu wawili waliwahi kuwepo katika dunia hii.Tunapowatazama hawa watu wawili itaonekana kana kwamba huyu mtu tajiri alikuwa heri kuliko Lazaro.
- Mtu tajiri alionekana kana kwamba alikuwa na vyote alivyohitaji na hata zaidi.
- Lakini Lazaro alikuwa mgonjwa, hakuwa na chakula cha kutosha, na bila shaka mwili wake wote ulikuwa umefunikwa na vidonda.
- **Luka 16:22**
- Hebu tafakari hayo:
- Je, mali ya yule mtu tajiri ilimzuia kufariki?
- Je, mali yake ilikuwa na manufaa yoyote kwake baada ya kufa?
- Je, Lazaro alienda wapi baada ya kufa?
- Alienda mahali ambapo Ibrahimu alikuwa. Kifua cha Ibrahimu kilikuwa ni misimu ya Wayahudi ya uwepo wa Mungu.
- Je, na tajiri naye?
- Je, alienda penye Lazaro alikuwa?
- Yesu alisema kuwa mwili wa mtu tajiri ulizikwa.
- Je, alipoacha mwili wake yeye alienda wapi?
- Wakati watu hufariki aita huende kuwa na Mungu au huelekee mahali pa hukumu papo hapo. **Luka 23:43; 2 wakorintho 5:8**
- Nataka kusema hivi: sehemu yetu tunapokufa itakuwa ni ya umilele…ni lazima tutaishi milele na Mungu mbinguni au tutakuwa kwa moto na hukumu milele. Hebu tutazame mahali mtu tajiri alienda.

D. Kilio cha tajiri cha msaada.

- **Luka 16:23** Lazaro alienda mahali pa raha na kukubalika na Mungu, lakini tajiri alienda mahali pa moto na hukumu ya milele.
- Sasa hivi, na hata labda miaka elfu mbili hapo mbeleni mtu tajiri bado yuko kuzimuni na atateseka milele, na maskini mwombaji wa kale yuko mbinguni na Mungu umilele yote.
- **Luka 16:24**
- Kuna mateso makubwa kuzimuni. Wale wote wanaokataa kuamini kile Mungu anasema katika Neno lake huenda huko na kuteseka. Tafakari kuhusu haya: Mungu anachukia dhambi, lakini hatoi vitisho tu kuhusu hukumu ya dhambi.
- Dhambi zote lazima zilipiwe kikamilifu.

E. Jibu la Ibrahimu

- **Luka 16:25**
- Zingatia**:** Je Lazaro alienda mahali pa furaha na panapo kubalika na Mungu kwa sababu ya kuwa maskini duniani? Je, tajiri alienda kuzimuni kwa sababu ya mali aliyo kuwa nayo duniani? Je, Mungu hukubali maskini na kukataa matajiri? La hasha! Hilo silo lililo leta utofauti kati ya watu hao wawili. Tajiri alienda kuzimu kwa kuwa hakuchukuwa muda kufikiria juu ya Mungu wala kuamini Neno lake. Aliishi tu duniani humu kufurahia mali yake na raha za dunia hii. Alijiishia. Kwa upande mwingine Lazaro alikubaliana na Mungu kuwa alikuwa mtenda dhambi na alimtumainia Mungu na ahadi zake za kumleta Mwokozi kama tu Ibrahimu alivyotenda akiwa humu duniani.
- **Luka 16:26**
- Mara tu mtu anapokufa na kuenda kuzimu hamna njia ya kuokolewa tena. Hakuna njia ya kutoka…amefungiwa kule milele! Wale wanaokufa wakiwa wametengwa na Mungu kwa sababu ya dhambi wanasalia kuishi maisha ya kutengwa milele.

F. Rufaa ya tajiri kwa ajili ya ndugu zake

- **Luka 16:27-28**
- Hata kama alikuwa katika mateso makali tajiri bado aliwakumbuka ndugu zake na jamaa zake.
- Watu walio kuzimu bado wanakumbuka ulimwengu huu.
- Wanakumbuka yale walitenda wakiwa hai, na wanakumbuka jamaa zao na marafiki zao waliosalia duniani.
- Je, mbona tajiri alimwomba Ibrahimu kumtuma Lazaro katika maboma za nduguze watano? Je, Lazaro aliruhusiwa kurudi duniani humu? La hasha! Mungu hawezi ruhusu walio kufa warejee.

G. Jawabu la Ibrahimu

- **Luka 16:29.**
- Ibrahimu alimwambia yule tajiri ya kwamba ndugu zake yafaa wazingatie mambo ambayo Musa na manabii wengine waliandika katika Biblia.

H. Lalama/hoja ya tajiri

- **Luka 16:30-31**
- Kama watu wanakataa kuamini Neno la Mungu ambalo limeandikwa, hawataamini hata kama Mungu atamtuma mtu mwingine aliye kufa kuja kuwaonya. Fikiria nyuma**:** Wakati Yesu alipomfufua Lazaro rafiki yake kutoka wafu, (ndugu ya Mariamu na Martha) Je, viongozi wa Wayahudi waliamini? La hasha!

I. Hitimisho.

- Kwa kweli adui amewadanganya watu kuhusu misha leo hii. Pesa, vitu na hata afya vinaonekana vya udhamana kuliko Mungu. Ni karibu miaka elfu mbili sasa tangu Yesu kuisimulia habari hii ya Lazaro na tajiri. Hawa watu bado wamo katika hali ile ile waliyokuwemo Yesu akisimulia hadith hiyo.
- Lazaro yu na Mungu.
- Tajiri yuko kuzimuni.
- Walikuwa wamechelewa na hivyo hawangeweza kubadilisha nafasi zao tena; Hatima yao iliamuliwa kama wangali duniani.
- Lazaro alimwamini Mungu.
- Tajiri hakumwamini Mungu, alifanya hivyo akiwa bado duniani. Lakini wakati alikuwa kwenye mateso, alimlilia Ibrahimu. Lakini hapakuwa na lolote ambalo Ibrahimu na Lazaro wangetenda. Na sisi je? Na jamaa zetu ambao hawachaokoka nao… umilele ni wakati mrefu! Yesu anaiweka kihalisi wazi katika **Marko 8:36.**

Yesu aliingia Yerusalemu.

A. Utangulizi

- Wacha tuanzie katika **Marko 11**. Jinsi tumetaja hapo nyuma. Umati wa watu ulimfuata Yesu kila mahali alikoenda.
- Wengine walitaka uponyaji wa kimwili.
- Wengine walitaka uhuru wa kisiasa kutoka kwa Waroma.
- Wachache sana walifikiria kuhusu mahitaji yao ya kiroho, na walikuwa tayari kukubali kuwa hitaji lao kuu ni kukombolewa kutoka kwa shetani, dhambi na mauti.

- Wakati Yesu na wanafunzi wake walipokuwa wakienda Yerusalemu, walifikia mji mdogo wa Bethania, nje tu ya mji wa Yerusalemu. Bethania ilikuwa makaazi ya Mariamu, Martha na Lazaro. Ilikuwa ni wakati mfupi tu baada ya Yesu kumfufua Lazaro kutoka wafu.

B.Yesu aliwatuma wanafunzi wake kumletea punda

- **Marko 11:1-6** Rejea nyuma nami katika **Zakaria 9:9.**

C. Watu walimkaribisha Yesu Kama Mkombozi.

- **Marko 11:7-10**
- Umati ulimkaribisha Yesu kama Mkombozi aliyeahidiwa kutoka kwa Mungu.
- Walimsifu kama yule ambaye manabii wa Agano la Kale waliahidi ya kuwa Mungu atawatumia mfalme.
- Lakini, bahati mbaya, watu wengi hawatumainia Yesu kuwaokoa kutoka kwa nguvu za shetani, dhambi zao, na hukumu ya Mungu.
- Walitaka tu Yesu kuwa mfalme wao ili awakomboe kutokana na maadui zao, haswa sana Warumi waliotawala nchi yao.

D. Mipango ya viongozi wa Kiyahudi

- **Marko 14:1-2 –**viongozi wa Wayahudi walikuwa na bidii ya kumuua Yesu, lakini waliogopa umati. Fikiria jinsi alivyokuwa amejulikana kwa sababu ya miujiza aliyokuwa ametenda.

Yuda alipanga kumsaliti.

A. Yuda alipanga kumsaliti Yesu.

- **Marko 14:10-** Yuda alikuwa mmoja wa wale ambao Yesu alichagua kuwa marafiki wake wa karibu sana, lakini Yuda hakujali hali yake ya dhambi mbele za Mungu.
- Hakumwamini Yesu kuwa Mwokozi wa wenye dhambi.
- Yuda alimfuata Yesu kwa faida zake mwenyewe.
- Kumbuka**: Yohana 12:4-6 -**yaonyesha nuru kidogo kuhusu tabia za Yuda.
- Ilipoonekana kuwa Yuda hapati faida yoyote ya kibinafsi kwa kumfuata Yesu, alikuwa tayari kumuuza kwa maadui zake.
- Lile Mungu alikuwa amenena katika Neno lake lilikuwa linatimia **(Zaburi 41:9).** (Rejelea **jedwali la unabii** ukurasa 108**…Zaburi 41:9/Marko 14:10-11)**. Shetani alikuwa akirejelea uchanja wake wa kale tena. Alikuwa anamwongoza Yuda kumsaliti Yesu**. Yohana 13:1-2** Shetani anamchukia Yesu kwa sababu Yesu ni Mungu na anamchukia Mungu.
- Shetani alifikiria kuwa akiwaongoza viongozi wa Wayahudi wamuue Yesu basi atakuwa ameharibu mpango wa Mungu wa kuharibu na kuwaokoa wenye dhambi.
- Mathayo anatueleza kuwa viongozi wa Wayahudi waliahidi kumlipa Yuda vipande thelathini vya fedha **(Mathayo 26:14-16).**
- Hapa kuna kitu cha kutafakari… vipande thelathini vya fedha ilikuwa bei ya mtumwa yeyote wa kawaida wakati ule. Zaidi ya miaka mia tano kabla ya hayo, Mungu alikuwa amemwambia nabii wake Zakariah kuwa haya ndiyo yatakayo tendeka kwa Mkombozi.
- **Zakaria 11:12-13** (Rejelea **jedwali la unabii** ukurasa108**. Zakaria 11:12,13; Mathayo 26:14, 15.**

Siku kuu ya Pasaka.

A. Maandalisi ya pasaka.

- **Marko 14:12-16**

- Yesu alijua ya kwamba wanafunzi watakutana na mwanaume amebeba chombo cha kutegea maji.
- Hili halikuwa jambo la kawaida kwa kuwa kazi ya kutega na kubeba maji ilikuwa imetengewa wanawake.

B. Yesu alijua msaliti wake.

- **Marko 14:17-18**
- Bwana anajua kila kila kitu kabla ya kutendeka.
- Hebu tafakari haya … Mungu alijua, miaka mia tano kabla ya kutendeka, ya kuwa Yesu atauzwa kwa senti thelathini. Anajua hata vitu vidogo kabisa visivyo na udhamana **(Mat 10:29-30).** Yesu alijua bila mtu yeyote kumwambia ya kwamba Yuda anaenda kumsaliti . Lakini Yesu alimpenda Yuda na alihuzunika kufikiria Yuda atatenda hayo.
- **Zaburi 55:12-13**
- **Marko 14:19-21**-Yesu kwa mara nyingi alijiita **"**Mwana wa Adamu**"** hata kama alikuwa Mwana wa Mungu, alikuwa pia mwanadamu halisi. Yesu alijua kwamba ni lazima afe kama vile Mungu alitabiri kupitia kwa manabii wake kwa Agano la Kale **(1 Petero 1:10-11).** Lakini hata kama ilikuwa lazima afe hiyo haikuwa sababu mwafaka kwa Yuda kujitetea. Mungu hakumuumba Yuda kumsaliti Yesu. Yuda lazima ahukumiwe milele kwa dhambi zake: ubinafsi wake, kushiriki kwake kwa mauaji ya mtu alisiye na hatia, na zaidi ya yote kukataa kumwamini Krito kama Mwokozi wa maisha yake. Tendo lake mbaya la kutisha ni dhibitisho kuwa hakuamini.

C. Maana ya mkate na divai.

- **Marko 14:22** -Yesu aliuvunja mkate na akaeleza kwamba, jinsi tu aliuvunja mkate, vivyo hivyo mwili wake ulikuwa karibu kuvunjwa na watu waovu.
- **Marko 14:23-24 -**Yesu alieleza kuwa divai aliyowamwagia ili wakainywe ilikuwa tashwira ya damu yake ambayo wakati atakufa itamwagika kutoka kwa mwili wake ili kulipia dhambi za wanadamu.
- **Marko 14:25-26**

D. Hitimisho

- Ni vigumu kwetu kutafakari juu ya upendo mkubwa wa Kristo.
- Hakuwahi tenda dhambi, na ilikuwa afe kwa ajili ya wenye dhambi.
- Kila mmoja katika ile meza alihitaji kile alichokuwa anaelekea kukitenda, zaidi ni, kila mmoja kila mahali.
- Walio kuwepo, waliopo na watakao kuwepo, pia wanahitaji kile alikuwa anaelekea kutenda.

SOMO LA 22

Yesu alikamatwa na maadui zake Marko14:32-15:19

Yesu alikamatwa na maadui zake.

A. Utangulizi.

- Mara nyingi tunashuhudia watu wakishikwa kwa makosa ambayo hawakutenda.
- Mioyo yetu huurumia yeyote aliye katika nafasi hii.
- Je, umewahi laumiwa kwa kosa ambayo hukutenda? Je, ulihisi vipi? Hebu sasa tugeuze hali hii. Wacha sasa niulize, Je, mtu mwingine amewahi laumiwa kwa ajili ya kosa ambalo wewe umefanya? Je, mtu mwingine amewahi hukumiwa kwa kosa ambalo wewe umetenda? Fikiria kuhusu hii kwa kukamatwa kwa Yesu.

B. Yesu akiwa Gathesamane

- **Marko 14:32-36** -Hata kama Yesu alikuwa Mungu alikuwa pia mwanadamu, na katika ubinadamu wake ilikuwa vigumu kwake kukabiliana na hali ngumu aliyojua atateseka. **(Luka 22:41-44).**
- Yesu alijua ya kwamba, ili yeye awe Mwokozi wetu, ilikuwa apitia mateso mengi ambayo hakuna yeyote ambaye amewahi kupitia. Tunapoendelea kujifunza, tutaona kilichomletea Yesu huzuni mwingi.

C. Yesu alisalitiwa na kukamatwa.

- **Marko 14:37-46** -Kwa kweli hata hawakugundua, lakini Shetani alikuwa anawaongoza Yuda na watu wote waliokuja kumshika Yesu Kristo.
- **Marko 14:47-49 -**Yesu alitambua kuwa kila kitu kilichotabiriwa (**unabii**) kumhusu yeye katika Agano la Kale yangetendeka tu jinsi Mungu alisema.

D. Wanafunzi walitoroka

- **Marko 14:50-52** -Wanafunzi wote walitoroka wakamuacha Yesu, Kama tu alivyotangulia kuwaeleza. (Kwa hakika hiki ndicho kifungu cha kuhusunisha sana katika Biblia.)
- Walikuwa na hofu, wakasushwa moyo na kuchanganyikiwa.
- Walidhani kuwa Yesu ni Mwokozi aliyetumwa kutoka kwa Mungu, lakini hawakuelewa ni jinsi gani angewaokoa kama anaenda kuawa na maadui zake.
- Hawakuelewa kwa jinsi gani kifo chake kingewaokoa kutoka kwa dhambi, shetani na mauti. **Zekaria13:7/Marko 14:27.**

E. Yesu Alijaribiwa na Viongozi wa Wayahudi.

- **Marko 14:53-55** - Yesu alisimama mbele ya Makuhani wakuu, mahakama kuu ya wayahudi.
- Yesu hakukuwa ametenda uovu lolote. Kwa hivyo, hawangepata sababu yoyote kisheria ambayo angehukumiwa kwayo. Hawakuwa na sababu yoyote isipokuwa ya kwamba walipenda njia zao usinivu na hawakutaka kutii neno la Mungu, ambalo Yesu aliwaambia.
- Tasama: hili ni jaribio moja wapo yay ale sita aliyo yapitia Yesu. Jaribio la tatu lilitendeka mbele ya viongozi wa kidini; Tatu mbele ya viongozi wa Roma. Hukumu hizi zote hazikuwa halali kulingana na jinsi ziliendeshwa na/au kutumiwa kwa mashahidi waongo.

- **Marko 14:56-59**_Manabii wa Mungu walisema kuwa mashahidi wauongo watanena kinyume na Mkombozi. **Zaburi 27:12**
- Rejelea **jedwali la unabii kurasa 108.** Funua **"Alihukumiwa na mashahidi wauongo"** na andiko la **Marko 14:56-57** Mkabala **Zaburi 27:12**. Soma unabii na utimilifu wake.
- Mungu alimsababisha Daudi kuandika unabii huu karibu miaka elfu moja kabla ya kutendeka.
- Sasa Yesu alisimama mbele ya kuhani mkuu, maneno halisi ya Daudi yalikuwa yanatimizwa.
- **Marko 14:60-62**-wakati walinena uongo kumuhusu Yesu alipaki kimya na hakujibu.
- Alikuwa akimtumainia Mungu, Babake kutekeleze yale alikuwa amempangia**.1 Petero 2:23**. Alijua ya kwamba kila kitu ambacho kingetendeka kwake ingekuwa ni kwa mapenzi ya babake ili kwamba tukakombolewe kutoka kwa nguvu za shetani, dhambi na mauti.
- Lakini walipomuuliza kwamba kwa kweli alikuwa Kristo (**kumaanisha mkombozi mtarajiwa**) na mtoto wa Mungu, Alijibu wazi kuwa ni ukweli.
- Hebu niulize hivi; je, unakumbuka jina Mungu alimpa Musa Pale ambapo Musa alimuuliza kile angewaambia watu kule Misri kumhusu yule aliyemtuma ? Katika **Kutoka 3:14** Mungu Alisema **"…MIMI NDIMI MIMI…waambie Waisraeli kuwa MIMI NDIMI Amenituma…"**
- Tilia maanani; Katika kitendo cha Yesu kushikwa katika **Yohana 18**, watu walisema kuwa wanamtafuta Yesu wa Nazareti, **Yohana 18:6**- inasema, "**mara tu Alipowaongelesha MIMI NDIMI, walirejea nyuma na kuanguka sakafuni**." Viongozi wa wayahudi walikuwa wamelifahamu vyema jina la Mungu **MIMI NDIMI**. Na pia walikuwa na uhakika kuwa Yesu anawaambia kuwa yeye ni Mungu.
- **Marko 14:63, 64**-Wakati wayahudi walitaka kuonyesha kukasirishwa kwao, ilikuwa tamaduni Yao kurarua mavazi. Kuhani mkuu alikasirishwa sana kwa kuwa, kwa jibu lake Yesu alikuwa anajilinganisha kuwa yeye ni Mungu.
- **Marko 14:65-** Haya ndio mambo halisi ambayo manabii wa Mungu walinena kuhusu mkombozi kuwa yatamtendekea.
- **Isaya 50:6**
- Rejelea tena **jedwali la unabii** katika kurasa 108**.** Fungua, "**Alipikwa na kutemiwa mate**,"na uandike kando yake **Marko 14:65** kando ya **Isya 50:6**.Soma unabii na utimilifu wake. Na jua ya kuwa huu ndio utimilifu wa Neno la Mungu.
- Isaya aliandika haya karibu miaka mia Saba kabla ya Yesu kuyatimiza. Na Yesu Alistahimili na kwa uhiyari mateso haya jinsi tu Isaya alitabiri.

F. Yesu Alijaribiwa na Pilato

- **Marko15:1-17** Warumi walioongoza Israeli hawakuruhusu mtu yeyote awawe bila ruhusa yao.
- Kaisari kiongozi wa warumi, alikuwa amechagua Pilato kuwa gavana wa Samaria na Yuda.
- Kwa hivyo viongozi wa wayahudi wakampeleka Yesu kwa Pilato, wakitarajia kuwa, kwa misingi ya hukumu za uongo walizokuwa wamepanga, Yesu angehukumiwa kifo.
- **Marko 15:2-** Kumbuka Yesu alikuwa uzao wa Daudi na angeweza kuwa Mfalme wa wayahudi.
- **Marko 15:3-5** Nabii Isaya alikuwa amesema kuwa Mkombozi angekuwa kimya wakati angenenewa uongo.**Isaiya 53:7.**
- Rejelea jedwali la unabii **kurasa 108**. Fungua **"…kimya wakati angenenewa uongo,"** na uandike **Marko 15:3-5** kando **Isaiya 53:7-**

G. Baraba au Yesu?

- **Marko 15:6-11** Ilikuwa tamaduni kuwa katika siku kuu Pasaka Pilato, gavana awafungulie mmoja ambaye wayahudi waliyemtaka.
- Pilato alijua kuwa Yesu hakutenda kitu kibaya. Alijua kuwa makuhani wa wayahudi walitaka kumuua Yesu kwa sababu ya vivu na wingi wa kujulikana na watu wengi .Pilato alidhani kuwa wayahudi wangemruhusu Yesu kuwekwa huru badala ya Baraba ambaye alikuwa muuaji.

H. Viongozi wa Wayahudi walitaka Yesu Asulubishwe.

- **Marko 15:12-14_**Kusulubishwa kulitumiwa na wayahudi kuwaadhibu wafungwa wabaya hii yaweza kulinganishwa na chemba ya gesi / ama kiti cha umeme .lakini hata kusulubiwa kulikuwa kubaya Zaidi kwakuwa mtu aliyesulubiwa hakufa papo hapo; aliyapitia mateso ya ukatili kwa masaa mengi na hata wakati mwingine siku kabla yake ndiposa afariki.
- Moja kwa moja unabii wa agano la kale kuhusu Mkombozi ukitimia kupitia kwa Yesu kristo.
- Mungu alikuwa amenena kupitia kwa Nabii Isaya yakuwa Wayahudi wangemchukia mkombozi hata kama hapakuwa na lolote la kusababisha kuchukiwa kwake.
- Alisema kuwa wange mkataa.
- Kila kitu alichokisema Mungu kupitia kwa manabii wake kuhusu kuja kwa Mkombozi kulitendeka kupitia kwa Yesu**.Isaya 53:3**
- **Mark 15:10**
- Rejelea **jedwali la unabii** ukurasa 108. Funua **''Atakataliwa na Wayahudi''** na uandike **Marko 15:9-14** kando **ya Isaya 53:3**.Fungua "**mtachukiwa bila sababu**,"na uandike **Marko 15:10 kando ya Zaburi 69:4.**

I. Yesu Alipigwa na kukejeliwa.

- **Marko 15:15 –**Kulingana na rekodi tangu wakati huu zinatueleza juu ya kupigwa kwa mijeledi.
- Viboko vilikuwa na mijeledi kadhaa ya ngozi .visehemu vya viuma na hata mifupa zilikuwa zimefunganiswa kwa mijeledi hiyo ya ngozi ili kwamba ikamkwaruze mfungwa wakati alikuwa akipigwa. Na ili kumzuia kutoroka mfungwa alifungwa mikono ikiwa imetapakazwa. Mijeledi ya mara kwa mara ilirarua ngozi ya kila mfungwa, ikikata nyama, misuli na mizizi ya damu mara nyingi ikimwacha mhusika na mirubuko mikali.Wafungwa wengi walikufa kwa mirubuko hiyo tu . Kuna andiko la kufurahisha katika **Isaya 52:14.**
- **Marko 15:15-19**. Baada ya viboko hatari, Askari walimkejeli Yesu walimvalisha vazi la zamawadi, (Hii ni rangi aliyovalishwa mfalme wa wakati ule.) walimtengenezea jabali/kofia ya matawi iliyo kuwa na miiba yenye makali na kumtwiga Yesu kichwani.

Nakili: Mwanzo 3:17-18 Wakati Adamu na Hawa walitenda dhambi, Mungu Alilaani dunia na akasema kuwa miiba itachipuka. Yesu alikuja kuteseka na kufa ni kwa sababu ya kutukomboa kutokana na laana za Mungu. Mungu Aliruhusu maadui wa Yesu kumvalisha taji ya miiba kichwani kwa Yesu, ni ishara ya kwamba Yesu anaenda kufa kwa sababu ya dhambi zetu.

J. Hitimisho.

- Tunahisi vibaya na hata kukasirika tunapofikiria mtu anayeteseka kwa jambo asilolitenda. Lakini tuseme nini kuhusu Yesu? Alikuwa anateseka kwa ajili yako na mimi …kwa kosa tulilotenda sisi. Alipitia cheche za matusi, kukejeliwa na uchungu wa mwili; Na bado hakulalamika.

SOMO LA 23

Yesu Alisulubiwa na Kuzikwa - Marko 15:20-46

Yesu Alisubiwa na Kuzikwa .

A. Utangulizi.

- Katika historia nzima, kile tunayeelekea kusoma juu yake ndicho cha maana zaidi. Hakuna chochote ambacho kimeweza kuadhiri maisha ya waume kwa wake kama hiki kitendo kimoja.

B. Yesu Alisulubiwa.

- **Marko 15:20-22.**
- Golgotha (neno lenye maana “fuvu”) ilikuwa tu nje ya kuta zaYerusalemu. **Waebrania 13:11-13.**
- **Marko 15:23 –** Kinywaji hiki kiliandaliwa na wanawake wa Yerusalemu kama kitendo cha huruma kutuliza uchungu wa wale ambao wamesulubiwa.
- **Marko 15:24 –** Tazama, walipomaliza kumsulubisha Yesu… misumari ilikongwa kwa mikono na miguu ya Yesu iliyopita mpaka kwa msalaba wa mbao. Msalaba mara uliwekwa imara juu.
- Je, wakumbuka Yesu akimweleza nekodemo kuwa, kama vile Musa alivyoinua nyoka wa shaba, hivyo ndivyo Yesu, Mkombozi, alikuwa ainuliwe ndipo wenye dhambi waokolewe kutoka kwa hukumu.
- **Yoh 3:14**
- Karibu miaka elfu kabla, Mungu alimwongoza mfalme Daudi kunakili kuwa, mikono na miguu ya Mkombozi itajeruhiwa. Nataka kusema hivi;
- Vile tunajua, kusulubiwa hakukuwepo wakati wa Daudi, ambapo unafanya unabii wake uwe wa kushangaza zaidi.
- Daudi pia alisema, mavazi ya Mkombozi itakuwa ya tuzo katika mchezo wa kupishania/kamari.
- **Zab 22:16-18.**
- Rejelea tena **jedwali la unabii** ukurasa wa 108.
- **Marko 15:25-26** – Kwa kawaida ishara iliwekwa juu ya mhukumiwa ili kuonyesha ni nini hasaa alichotenda. Lakini Yesu hakuwa na kosa lolote. Pilato hakupata chochote cha kumhukumu juu yake.
- **Lk 23:4 na 13-15; Yoh 19:6**
- Tafakari hili; Yesu alikuwa anakufia dhambi: dhambi zangu, dhambi zako, na dhambi za dunia nzima. Wewe na mimi ndio tuliostahili kuwa kwenye huo msalaba. Alikuwa anachukuwa gadhabu yetu. Alikuwa anachukuwa aibu na hukumu yetu yote. Alikuwa analipia hukumu ya kifo…kwa ajili yangu na wewe.
- **Marko 15:27, 28 –** Kupitia kwa Isaya nabii, Mungu alisema kuwa Mkombozi atakuwa kati ya watu waovu. **Isaya 53:12 (**Rejelea tena **jedwali la unabii** ukurasa wa 109**)**

C. Yesu alikejeliwa akiwa Msalabani.

- **Marko 15:29-32.**
- Kifungu kingine cha kufurahisha ni katika **Yoh 2**
- **Yoh 2:18-21** – Hata kama walimsulubisha, alipanga kutoka humo kaburini siku tatu baadaye.
- Wayahudi hawakutambua kuwa Yesu alimaanisha mwili wake.
- Walifikiria kuwa anazungumzia hekalu la Yerusalemu. Wajua kuwa, miaka mingi kabla ya mfalme Daudi kuandika kwamba maadui wa mkombozi watamkejeli na kumchekelea kwa mateso

atakayopitia. Mungu alijua haswa nini kitamtendekea mwanawe muda kabla ya yeye kuja humu duniani.

- **Zab 22:6-8**

D. Yesu alilipia dhambi zetu kwa kifo chake.

- Mungu hangetusamehe dhambi zetu na kutukubali kama hukumu ya dhambi zetu haingelipiwa kikamilifu.
- Je, mshahara wa dhambi ni nini? Kifo**. Mwanzo 2:15-18; War 6:23a**
- Hii haimaanishi kifo cha kimwili tu bali hata kutengwa na Mungu kuzimu. Kwa hivyo, njia pekee ambayo Yesu angetuokoa ni kutuondolea hukumu…ambayo ni kifo. Hapa pana jambo jingine cha kutafakari; Yesu mwenyewe hakuwa na dhambi yoyote ambayo ingemsababisha afe.
- Alikuwa mkamilifu.
- Wakati Yohana alimpatiza, Mungu baba alisema kutoka Mbinguni ya kwamba amependezwa na Yesu. **Mat 3:17**
- Kutoka wakati mwanadamu alitenda dhambi, Mungu alisema, wakati wowote mwanadamu angetoa dhabihu ya mwana-kondoo au mnyama yeyote, yule mnyama hakustahili kuwa na doa lolote. Hakutakikana awe mgonjwa au na jeraha lolote. Alikuwa awe mkamilifu. **Kutoka 12:5; 2Wakorintho 5:21** – Kumbuka kondoo aliyekuwa mbadala wa Isaka. kwa kuwa Yesu alikuwa bila kosa mbele zake Mungu, aliweza kujitoa mwenyewe kama dhabihu kwa ajili yetu.
- Kama vile kondoo alivyo kufa badala cha Isaka, Yesu naye alikuja humu duniani kuchukuwa nafasi yetu mbele za Mungu na kufa kwa niaba yetu.
- Wacha tuongee kwa uchache yale yote ambayo Yesu aliyapitia: Alisalitiwa na mwanafunzi wake mwenyewe, akashitakiwa kwa uongo, akahukumiwa kwa uongo, akajaribiwa bila sababu mwafaka… akakataliwa na watu ambao walistahili kumpokea kama Mfalme wao na Bwana.
- Bila huruma alichapwa, akachipuliwa ngozi na kusulubishwa.
- Kwa hivyo akatundikwa msalabani, amechoka, akitokwa na damu, na kwa uchungu mwingi. Lakini hakukuwa na lolote ngumu kati ya hayo kuliko kile angepitia ili kikamilifu kutuondolea hukumu ya dhambi.
- **Marko 15:33 -** Mbona mwangaza wa jua ulipotea? Kwa nini kulikuwa na giza kwa masaa matatu? Je, ni kwa sababu Mungu alimgeukia Yesu? Je, Mungu alimgeuka Yesu mwanawe mpendwa na kumwacha pekee yake?
- **Marko 15:34 –** Kwa nini Mungu alitenda jambo hili mbovu kwa Yesu? Yesu alimtii Mungu wakati wote. Yesu hakutenda lolote mbaya. Alikuwa ametii sheria zote za Mungu.
- Mbona Mungu alimwacha hivyo? Kwa sababu Mungu alikuwa anamhukumu Yesu kwa sababu ya dhambi zangu, zako na za dunia nzima. Je, mshahara wa dhambi ni nini…kifo/utengano… kama Yesu angelipia dhambi zetu, ilikuwa lazima atenganishwe na Mungu…kumbuka **War 6:23a**.
- Yesu aliteseka kwa hukumu kikamilifu kwa ajili ya dhambi zetu ili Mungu kwa bure (bila malipo yoyote kwetu) atusamehe na kutukubali kama watoto wake sisi tunaokubali Mungu na kumtumainia Yesu pekee.
- Fikiria nyuma basi…hapo mwanzo, Mungu alimwambia Adamu ya kwamba, kama atakula kwa mti wa maarifa ya Mungu ya mema na mabaya, atakufa. Adamu angetenganishwa na Mungu aliyempa uhai. Dhambi lazima zilipiwe kwa kutenganishwa na Mungu. Hivyo ndivyo ilibidi Yesu atenganishwe na Mungu. Ilikuwa ni njia ya pekee ya kulipia dhambi zetu.
- **Marko 15:34-36** – Watu waliokuwa karibu na msalaba, hawakuelewa kile Yesu alisema.
- **Marko 15:37** – Yesu alikufa na akapeana maisha yake kwa ajili yetu. Alifanya yote iliyohitajika kwa ukombozi wetu kutoka kwa shetani, dhambi na mauti.
- Marko anatueleza kuwa Yesu alilia kwa sauti kubwa na akakata roho yake, lakini hatuelezi kile Yesu alisema. Lakini katika kitabu cha Yohana tunaelezewa kile Yesu alisema.

- **Yoh 19:30** "….yamekwisha**…."**
- Je, wafikiria Yesu alimaanisha nini kwa usemi huo? Je, alimaanisha kuwa amekwisha? La hasha, alikuwa ameshasema kuwa atafufuka baada ya siku tatu. Sasa ni nini ilikuwa imekwisha? Kazi aliyokuja kutekeleza ulimwenguni ilikuwa imekamilika kikamilifu.
- Yesu alikuja ulimwenguni kukomboa wenye dhambi kutoka kwa shetani, dhambi, na mauti.
- Alikamilisha kazi hii kwa kutenganishwa na Mungu na kupeana damu na uzima wake kama malipo dhabiti ya dhambi zetu.
- Wajua, ni ya faraja kujua kwamba hakuna haja mtu yeyote kutenganishwa na Mungu. Yesu Kristo alitutendea lile ambalo hatungetenda wenyewe.
- Kazi aliyotenda Yesu kwa kutufia msabani kwa ajili ya dhambi zetu ndiyo kazi pekee ambayo Mungu anakubali kama malipo ya dhambi zetu.
- Kumbuka nyuma; katika bustani la Edeni Mungu aliahidi kuwa atamtuma mkombozi, na Mungu alitimiza ahadi yake. Yesu alikamilisha kazi yake aliyopewa na Mungu Babake ili aitende kwa ajili yetu. Dhambi ya Adamu iliwatenganisha wanadamu wote na Mungu. Lakini kifo cha Yesu Kristo msalabani kiliwaunganisha na Mungu milele wale wanao weka imani yao ndani ya Kristo **War 5:12-21.**

E. Pazia ya hekaluni iliraruka.

- **Marko 15:38**
- Kumbuka pazia nzito/kitambaa kilikuwa kimening'inia mbele ya chumba cha ndani hekaluni lililojengwa na Waisraeli kama nyumba ya Bwana jangwani. Baadaye wakati hekalu lilijengwa, hili pazia lilining'inwa mbele ya chumba cha ndani humo hekaluni. Mungu alikuwa amewaambia Wayahudi kuliweka lile pazia mbele ya chumba cha ndani hekaluni ili wasisahau hiyo, kwa sababu ya dhambi, walikuwa wametenga kwa uwepo wa Mungu (Walitenganishwa na Mungu). Nyuma ya pazia kulikuwa utukufu wa Shekina wa Mungu, na hapa ndipo kuhani mkuu alikuja kila mwaka kunyunyuzia damu ya wanyama.
- Je, wafikiria ni nani aliyerarua hiyo pazia kutoka juu hadi chini? Mungu Mwenyewe alitekeleza hilo! … Na alitenda hilo kuonyesha kuwa alikuwa ameridhishwa kikamilifu na malipo ambayo Yesu amekamilisha kwa ajili ya dhambi zetu.
- Njia ya kurejea tena kwa Mungu ilikuwa imefunguka kwa sababu Yesu alitoa damu yake kama malipo kamilifu ya dhambi zetu. Mungu ameahidi ya kwamba, wale wote wanaokubaliana naye na kumtumainia Yesu pekee na malipo yake kwa dhambi zao watakubalika na Mungu kikamilifu, na hawawahi ingia kuzimuni.
- **Yoh 3:16**

F. Akida; wanawake waliokuwa karibu na msalaba; na kuzikwa kwa Yesu.

- **Marko 15:39-46 –** Hata wakati Yesu alipokuwa anazikwa, unabii ulikuwa unatimia.
- Yusufu wa Arimathaya alikuwa mtu tajiri.
- Yesu alizikwa kaburini kwenye pango iliyomilikiwa na yule Yusufu.
- **Isaya 53:9**
- Rejelea jedwali la unabii **kurasa wa 108.**

G. Hitimisho.

- Yesu Kristo aliishi duniani bila kutenda dhambi yoyote. Alitekeleza amri zote takatifu za Mungu. Alihukumiwa hukumu kali tuliyoistahili wewe na mimi. Msalabani alitengwa na Mungu kwa kuwa malipo ya dhambi ni mauti (**Kutenganishwa**), na basi yote imekwisha. Malipo kamilifu yametimizwa. Hakuna kingine kinachostahili kutendeka kulipia dhambi zetu. Pazia iliraruka. Njia imefunguka kumwendea Mungu kupitia kwa Yesu Kristo kwa wale wote wanaomwamini.

SOMO LA 24

Yesu Alifufuliwa kutoka Wafu, Akawaonekania Wanafunzi Wake, Akarejea Mbinguni naAkaahidi kurudi tena. – Marko 14:61 ; Lk 24:1-48; Matendo ya Mitume 1:9-11

Yesu Alifufuliwa kutoka kwa wafu. .

A. Utangulizi.

- Tulipoanza haya mafunzo tulisema kuwa Biblia ni historia ya kweli, na Yesu ndiye mhusika mkuu. Ni vyema kufahamu ya kwamba hatuzungumzii kiongozi wa dini yoyote hapa bali tunasoma historia halisi ya Mungu mkuu aliyekuja humu duniani kuwa mkombozi wetu.

B. Wanawake walikuja kwenye kaburi.

- Sasa kumbuka Yesu alikuwa amezikwa kwa siku tatu baada ya kufa. Na sasa kwa siku ya kwanza ya wiki, wanawake kadhaa waliokuwa wamemwamini Kristo, na walikuwepo akizikwa, walirejea tena alipozikwa.
- **Lk 24:1** - Ilikuwa tamaduni ya Wayahudi kuupaka manukato mwili wa marehemu kabla ya kuzikwa. Lakini Yesu alikuwa amezikwa kwa kuharakisha.
- Kumbuka ya kwamba: Wayahudi walikuwa katika siku zao za pasaka kuu hawakuwa na wakati wa kuupaka manukato mwili wa Kristo. Na pia siku iliyofuata ilikuwa siku ya sabato ambapo hawakustahili kujihuzisha kwa kazi yoyote ile. Na hivyo iliwabidi wangojee hadi siku ya kwanza ya wiki ili waje wampake manukato. Hawa wanawake waliingia kaburini Jumapili na walitarajia kuupata mwili pale. Lakini ya ajabu ipi…
- **Lk 24:2** – Wanawake hawakujua ya kwamba Mungu alikuwa amewatuma malaika wake kusongesha jiwe lile lililokuwa limewekwa langoni mwa kaburi ambapo mwili wa Yesu ulikuwa umelazwa**. Mat 28:1-4**
- **Tanbihi ya akiolojia**: Ni la kushangaza kuwa katika Yerusalemu hadi sasa kuna makaburi yaliyokuwepo tangu enzi za Yesu Kristo. Baadhi ya makaburi haya ni mapango kwenye mwamba, na yako na lango kubwa la jiwe ya mviringo, iliyozungukwa ili kwamba jiwe liwe likipingirishwa na kuwekwa mlangoni, kama tu imeelezwa katika haya Maandiko.

C. Ujumbe wa malaika

- **Lk 24:3,4** – Mwili wa Yesu haukuwa kaburini! Na la kushangaza kwao tena, malaika wawili waliwasalimia! Sikiza kile malaika waliwaeleza**: Lk 24:5-7**. Yesu amefufuka kutoka wafu, kama tu alivyosema! Kumbuka sasa, Yesu ni Mungu na alikuja duniani na kufanyika mwanadamu ili atukomboe sisi kutoka kwa Shetani, dhambi na mauti.
- Alijua Kabla kutoka mbinguni kuwa ni lazima atoe maisha yake ili atukomboe, na pia alijua kuwa atafufuka tena.
- **Zab 16:10.** Angalia **jedwali la unabi** ukurasa wa 108.
- **Lk 24:8-12** – Wajua, wanafunza wake wote ilifaa wamungojee na kumtarajia kufufuka kutoka kwa wafu kwa sababu alikuwa amewaeleza mara nyingi sana kabla ya kufa kuwa atafufuka siku ya tatu.

- Inawezekana hawakukumbuka wala kuelewa kile alisema, au ni wazi kuwa hawakuamini kuwa kuna uwezekano yeye atoke kaburini akiwa hai.
- Lakini lija ya vile inavyooneka haiwezekani, Mungu kila mara hutenda kile alichoahidi.

D. Yesu ni Mwana wa Mungu.

- Tuna uhakika kuwa Yesu ni mwana wa Mungu na mkombozi aliyeahidiwa kwa kuwa, Mungu alimfufua kutoka wafu. **War 1:3,4; 10:9**
- Kumbuka sasa kuwa viongozi wa kiyahudi walimsulubisha Yesu kwa kuwa alijidai kuwa Mwana wa Mungu na Mkombozi. Lakini Mungu alimfufua, ili kila mtu ajue kwamba ni kweli kuhusu madai yake. Mungu alifunua wazi kuwa aliridhishwa kikamilifu na malipo ambayo Yesu alilipa kwa ajili ya dhambi zetu. Njia mojawapo aliyotufunulia ni kwamba, kabla ya Yesu kufa, Alisema, ”yamekwisha”na papo hapo Mungu akairaruwa pazia ya hekalu toka juu hadi chini. Alifanya hivyo kuonyesha kuwa njia ya kumrudia tena imefunguka, kwa sababu alikuwa ameridhishwa na malipo ya dhambi kupitia kwa damu ya Yesu.

E. Mungu ameridhishwa na malipo ya Yesu.

- Lakini kuna kitu kingine kinacho tuhakikishia kuwa Mungu alikuwa ameridhishwa na malipo, na hii ni wakati alimfufua Yesu kutoka kwa wafu.
- Mungu hangemfufua kama hangeridhishwa kikamilifu na malipo hayo aliyokuwa ameifanya.
- **Tafakari:** kama mtu atapelekwa mahakamani na hakimu, ni lazima aishi pale hadi siku atawekwa huru. Kama atatoroka basi polisi watamfuata na kumrejesha tena mahakamani, lakini kama atazalia tu mahakama na kuhukumiwa kifungu chake chote, basi atawekwa huru kwa kuwa amehukumiwa kikamilifu kwa hukumu ya makosa aliyotenda. **War 4:24,25**
- Mungu alituonyesha kuwa hakuna malipo mengine ya kulipwa kutoka kwetu kwa kumfufua Yesu na kumrejesha tena kwenye uzima.
- Kama Mungu, hakimu, hangeridhishwa, hangemfufua kutoka kwa wafu.
- Sasa ni kwa jinsi gani twaweza kukombolewa tena kutoka kwa dhambi, Shetani na utengano wa milele na Mungu? Ni kwa kuweka tumaini letu kikamilifu kwa Bwana Yesu, tukiamini kuwa alitoa damu yake kama malipo kamili ya dhambi zetu na akafufuka tena kutoka wafu kutupa uzima wa milele.

Yesu aliwaonekania wanafunzi wake. .

A. Yesu aliwaonekania baadhi ya wanafunzi wake.

- **Lk 24:13-24** - Hata kama Yesu alikuwepo pale na wao**,** hawakumtambua. Biblia haituelezi ni kwa nini hawakumtambua; lakini hawakumtambua. Ni la kufurahisha kuwa Yesu aliwafunza, jinsi tu tumekuwa tukifanya hapa kwa kutumia agano la kale, kwa utaratibu akiwafungua macho yao ili ajifunue kwao.

B. Kwa kutumia maneno ya manabii katika agano la kale, Yesu aliwafunza kujihusu.

- **Lk 24:25-27 –** Na hata baada ya hayo yote, bado hawakutambua kuwa ni Yesu alikuwa akiwaongelesha.

C. Wafuazi wa Yesu wanamtambua Kristo aliyefufuka.

- **Lk 24:28-32 –** Mara nyingi kabla ya kuketi na Yesu na kumtazama akiumeka mkate! Sasa, alipoumeka mkate tena, walitambua kuwa alikuwa ni Yesu! Baadaye wanafunzi walipokuwa wamekusanyika pamoja, Yesu aliwaonekania tena.
- **Lk 24:35-44 –**

Yesu alipaa mbinguni na akaahidi atarudi tena. .

A. Maneno ya mwisho ya Yesu kwa Wanafunzi wake.

- **Lk 24:45-48 –** Hii ilikuwa amri ya Yesu ya mwisho na sio tu kwa wanafunzi wake wa wakati huo, bali ni kwa wote wamwaminio na kukubali malipo yake kwao.
- Alikufa kwa ajili ya watu wote, na kwa hivyo Mungu anataka kila mtu ajue kwamba anaweza kukombolewa kutoka kwa Shetani, dhambi na mauti. Mungu hataki yeyote kuteseka katika hukumu ya milele. **2 Petro 3:9**
- **Yoh 3:16** – Hii ndio maana tumejifunza Biblia pamoja ili tuweze kusikia na kufahamu na kuamini hii habari njema na kuweza kushiriki na wenzetu.

B. Ni lazima tuamini Neno la Mungu.

- Huu ni ujumbe wa Mungu kwa dunia nzima, lakini si kila mtu anayofursa ya kuusikiza**. Marko 16:15; Mathayo 28:19,20; Matendo ya Mitume 1:8; 2 Wakor 5:18-20.**

C. Yesu alipaa juu Mbinguni.

- Baada ya Yesu kuwaamuru wanafunzi wake kupeleka Habari Njema kwa kila mtu, aliwaacha na kurudi kwa Babake mbinguni.
- **Matendo 1:9; Zab 68:18;** Rejelea **jedwali la unabii**, ukurasa wa 108.

D. Yesu atarudi tena.

- **Matendo 1:10 –** Hawa walikuwa malaika wawili wa Mungu.
- **Matendo 1:11 –** Yesu anarudi tena hapa duniani, lakini anaporudi, haitakuwa kuwakomboa tena wenye dhambi kutoka kwa Shetani, dhambi na mauti- Yesu amemaliza hiyo kazi. Kumbuka, imekwisha!
- Mungu sasa anamuamru kila mtu kutubu__yaani hiyo ni kukubali kwa Mungu kuwa ni watenda dhambi dhaifu wanaostahili hukumu yake, na kutumainia tu katika malipo ambayo Yesu alikamilisha kwa ajili yao.
- Wakati mwingine Yesu akirudi, itakuwa kama hakimu mkuu wa ulimwengu mzima. **Matendo 17:30,31**
- Tazama kile aliwaelezea viongozi wa Wayahudi kabla ya kumsulubisha.
- **Marko 14:61-62 –** Wakati Yesu atarudi tena kama hakimu mkuu, wale ambao hawakumtumainia yeye na malipo yake kamilifu wala kutubu dhambi zao watarushwa pamoja na shetani na malaika wake katika ziwa la moto wa milele. **Ufunuo 20:15**

E. Hitimisho.

- Ujumbe wa Mungu kwetu ni wazi.
- Wanafunzi wote wa Yesu, (isipokuwa Yuda, aliyemsaliti kwa senti 30) walimwamini.
- Walijua kwamba yeye ndiye Mungu aliahidi kumleta. Waliona miujiza yake, walimwona akifa; walimwona akiwa hai tena; walimwona akipaa juu angani. Baada ya haya yote, wanafunzi walienda nje na kuambia wengine kuhusu habari ya Yesu, na maelfu waliamini ujumbe. Lakini wengine waliwapinga vile walivyompinga Yesu pia.
- Wanahistoria wanarekodi kuwa, manabii wa Yesu wote walikufa baada ya kuadhibiwa na watu kwa sababu ya imani yao ndani ya Kristo. Baadhi ya wanafunzi waliteswa; baadhi wakasulubiwa; mmoja akafa gerezani. Je, hawa watu walikuwa wamepeana maisha yao kwa uongo? La, Walikufa kwa kile walishuhudia kuwa kweli. Na sasa tunaweza weka imani yetu imara ndani ya Neno la Mungu kwa kuwa ni kweli.
- **Yoh 3:16**

(JEDWALI LA UNABII)

KILE MUNGU ALISEMA KITATENDEKA KWA MKOMBOZI.

Isaya 9:7	Kizazi cha Daudi	**Mathayo 1:1,6,17**
Isaya 7:14	Kuzaliwa na bikira	**Mathayo 1:18**
Mika 5:2	Mzaliwa wa Bethelehemu	**Mathayo 2:1**
Hosea 11:1	Mkimbizi Misri	**Mathayo 2:14**
Isaya 11:2	Tabia zake kadhaa	**Luka 2:52**
Isaya 53:4-5	Atateseka kwa ajili ya wengine	**Mathayo 8:17**
Zaburi 41:9	Atasalitiwa na rafiki wake wa karibu	**Marko 14:10 – 11**
Zekaria 11:12,13	Atauzwa kwa senti 30	**Mathayo 26:14-16**
Zab 27:12	Atahukumiwa na mashahidi waongo	**Marko 14:56-57**
Isaya 50:6	Atapatwa na fedheha na kutemewa	**Marko 14:65**
Isaya 53:7	Kimya wakati wa hukumu	**Marko 15:3-5**
Isaya 53:3	Atakataliwa na Wayahudi	**Marko 15:9-14**
Zab 69:4	Atachukiwa bila sababu	**Lk 23:4, Yoh 19:6**
Zab 22:16	Mikono na miguu yake kujeruhiwa	**Marko 15:24**
Zab 22:18	Mavazi yake kukanyagwa	**Marko 15:24**
Isaya 53:12	Kufa na waovu	**Marko 15:27**
Zab 22:6-8	Tukanwa na kukejeliwa	**Marko 15:29-32**
Isaya 53:9	Kuzikwa kati ya wakwasi	**Marko 15:43-46**
Zab 16:10	Atafufuka toka wafu	**Lk 24:6**
Zab 68:18	Atarejea mbinguni	**Matendo 1:9**